ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
41.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
42.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
43.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
46.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
50.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
52.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
54.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
56.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
57. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
61.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
62.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
64.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
66.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
67.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
68.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
71.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
75.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
77.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim **Katibu wa Baraza la Wawalishi**

Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 11 Julai, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 77

Alama za Barabarani

Mhe. Shadya Moh'd Suleiman - Aliuliza:-

Serikali ya awamu ya sita imejitahidi kuimarisha miundo mbinu ya barabara Mijini na Vijijini lakini barabara nyingi hazikuwekwa alama za barabarani .

(a) Mhe. Waziri huoni kwamba kutokuwepo kwa alama hizo kunaweza kuchangia kuongezeka kwa ajali za barabarani.

(b) Ni kwa muda gani alama hizo zitawekwa ili ziweze kuwaongoza vyema madereva ili waweze kuendesha kwa uhakika na usalama zaidi.

(c) Mhe. Waziri huoni kwamba kwa kukosekana alama hizo barabara zetu haziendi na wakati na kiwango cha kimataifa.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano) - Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako na naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 77 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake naomba kutoa maelezo yafuatayo:

Kukamilika kwa ujenzi wa barabara ni pamoja na kuiwekea alama zote zinazohitajika katika barabara hiyo. Aidha, hapa Zanzibar baada ya muda mfupi wa ukamilishwaji wa ujenzi wa barabara, alama nyingi hutolewa tena kwa makusudi na baadhi ya wananchi kwa sababu wanazozielewa wao wenyewe. Hili ni tatizo na tabia hii siyo nzuri.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba kutokuwepo kwa alama za usalama barabarani kunachangia kuongezeka kwa ajali.

(b) Wizara yangu kwa kutumia fedha kutoka Mfuko wa Barabara *(Road Fund)* inategemea fedha maalum kwa ajili ya kuzirejesha alama ambazo aidha zimeharibika au kuibiwa.

(c) Kutokana na maelezo yangu ya utangulizi, nathibitisha kwamba barabara zetu zinaenda na wakati pamoja na kiwango cha kimataifa.

Mwisho natoa wito kwa Wajumbe wote wa Baraza tusaidiane katika kuwaelemisha wananchi umuhimu wa alama za usalama barabarani.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, nataka kumuuliza Mhe. Waziri kumekuwa na kilio cha muda mrefu kwa wananchi wa Shehia ya Mchangani na Mlandege katika kukata barabara eneo la Benki ya *NMB* karibu na ofisi ya Baraza la Mji watoto wao kuelekea chuoni.

Je, wizara yako itasaidia vipi kujenga *zebra* kuwanusuru watoto na ajali? Kama mfuko hautoruhusu kutokana na bajeti, wananchi wako tayari kusaidia suala hilo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano): Mhe. Spika, kilio hicho tumekisikia na tuko katika shughuli za kujaribu kutizama. Kwa sababu sio kila pahala tunaweza kuweka alama za barabarani, lakini lazima tutizame utaratibu uliowekwa na tukikubaliana tutafanya hivyo. Kama kutakuwa na matatizo mengine basi tutawaita wananchi na tutashauriana ili tuweze kuliondoa tatizo hilo.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa madhumuni makubwa ya alama za barabarani ni kujaribu kuchunga usalama wa watumiaji wa barabara hiyo, na kwa kuwa barabara inayotoka Mazizini kwenda Mbweni katika kuchunga ule usalama wa wanaotembea katika barabara hiyo wameweka yale matuta ambayo ni kero kubwa kwa waendeshaji wa gari. Mhe. Waziri haoni kuna haja ya kuyabadilisha matuta yale na kuyaweka mengine yenye usalama kidogo kwa vyombo vya moto.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano): Mhe. Spika, mwisho sikusikia vizuri.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Nimesema kwa kuwa matuta yale yaliyowekwa katika barabara ya Mazizini kuja Chukwani ni kero kubwa kwa wanaotembea na vyombo vyao mule, haoni kuna haja ya kuyabadilisha na kuweka yaliyokuwa hayana bughudha kama yale.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano): Mhe. Spika, ni kweli kumekuwa na mfumko wa kuweka matuta mengi ambayo hayana utaratibu maalum, mengine utaona ni membamba, mengine mapana, lakini sasa hivi wizara yangu tumekaa na kujadili na utaona baadhi ya sehemu tumeshaanza kuyatoa yale matuta ambayo yanakera wananchi na kuweka matuta ya viwango ambayo ni mazuri na yanayosaidia kwa vyombo vya moto. Tutazidi kufanya hivyo kila pale ambapo tutahisi hapa pana kero kwa wananchi.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Napenda kumuuliza Mhe. Waziri kwa kuwa alama hizi ni muhimu barabarani kwa wananchi na madereva, na kwa kuwa Kisiwani Pemba bado alama hizi hazijakuwepo. Je, Mhe. Waziri ni lini alama hizi zitawekwa Kisiwani Pemba ili wananchi waweze kuepuka ajali za mara kwa mara.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano): Mhe. Spika, alama za barabarani Pemba ziko lakini sio nyingi. Lakini tunamhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba katika barabara hizi mpya ambazo zinajengwa zote tutaziweka alama za barabarani kwa utaratibu ambao unajulikana.

Nam. 86

Wageni Kumiliki Ardhi

Mhe. Asha Abdu Haji – Aliuliza:-

Kwa kuwa sekta ya utalii inakua kwa kasi hapa nchini kutokana na wawekazaji katika sekta hii na wazalendo na wageni. Wawekezaji hawa wote watumia ardhi kuendesha biashara zao.

(a) Je, kuna sheria yeyote inyomruhusu mgeni kumiliki ardhi hapa Zanzibar.

(b) Katika maeneo mengi ya utalii, wawekezaji wamejenga uzio (*fence*) kuzungushia maeneo yao, na hivyo kuziba njia za asili zilizokuwa zikitumiwa na wananchi wa maeneo hayo. Je, serikali haioni kuwa kitendo hicho ni usumbufu na kuwanyima haki wananchi katika maeneo hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 86 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, hakuna sheria inayomruhusu mgeni kumiliki ardhi katika Visiwa vya Unguja na Pemba, badala yake wageni hukodishwa ardhi kwa mikataba maalum inayojulikana kama *"Land Lease Agreement".* Aidha, wageni wanapotaka kutumia ardhi kwa matumizi mbali mbali hukodishwa kwa mkataba maalum kama Sheria ya Ardhi Nam. 12 ya mwaka 1992 inayoelekeza.

(b) Ni kweli ujenzi wa uzio (*fence*) unaleta usumbufu mkubwa kwa wananchi katika maeneo ya utalii, sheria inaruhusu ujenzi wa uzio ili kuzuia uvamizi na kuweka usalama katika maeneo ya uwekezaji. Serikali huwalazimisha wawekezaji kutengeneza njia mbadala kabla ya kufunga njia za asili zinazotumiwa na wananchi wa maeneo hayo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moija la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akitoa majibu alieleza kwamba hakuna sheria inayomruhusu mgeni kumiliki ardhi hapa Zanzibar, isipokuwa kuna mkataba wa makubaliano ambao unategemea ule muda alioweka.

Sasa Mhe. Spika, swali langu ni kwamba tumeona sasa hivi kuna mahoteli makubwa ya kisasa tena ya gharama kubwa, kwa mfano Kempinski, Lagema na maeneo mengine. Je, wale wawekezaji katika majengo yale baada ya kufika huo muda uliowekwa mkataba majengo yale yatarudi serikalini au yatarudi kwa wale wananchi ambao walikuwa wanamiliki ardhi hapo mwanzo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, wawekezaji hao baada ya kumalizika muda wao wa kodi basi majengo yale yanarudi serikalini.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru sana na baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu a na b.

(a) Kwa kuwa amesema majengo hayo baada ya kumaliza muda yanarudi serikalini. Je, anaweza kutupa mfano wa majengo mawili au matatu ambayo yamerudi serikalini.

(b) Wastani wa umri wa kuishi Wazanzibari ni miaka 42, lakini wizara yako inakodisha ardhi mpaka miaka 99. huoni kwamba hiyo si haki.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ni kweli uhai wa Wazanzibari ni miaka 55, 52, mpaka 50. Hiyo ndiyo *average* ya uhai wa Wazanzibari. Kuna maeneo yanakodishwa mpaka miaka 99. Maeneo hayakodishwi kwa kufuata uhai wa Mzanzibari maeneo yanakodishwa kwa kufuata uzito wa *investment* iliyofanywa katika eneo lile. Kwa hivyo, tunaanza na miaka 44, 66, na mwisho wake 99 kwa kutegemea uzito wa ile *investment* iliyofanywa katika lile eneo.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri kwa kuwa miaka 99 ni muda mrefu sana ambao wawekezaji hukodishwa ardhi hiyo. Huoni Mhe. Waziri kwamba suala hili linaweza kupelekea ubabaishaji kwa watu wanaohusika na mkataba huu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, sikumsikia vizuri naomba alirejee tena swali lake.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Mhe. Spika, nauliza kwa kuwa ukodishwaji wa ardhi kwa muda wa miaka 99 ni muda mrefu sana. Mhe. Waziri haoni kwamba suala hili linaweza kusababisha ubabaishaji kwa wahusika wa mkataba huu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, anavyosema Mhe. Mjumbe ni kweli muda wa miaka 99 ni muda mrefu. Nilipojibu swali mama nilisema tunaanzia miaka 44 na ni wengi wamekodishwa kwa muda wa miaka 44. Akionekana kwamba amefanya vizuri, uwekezaji wake unaleta faida katika nchi na akiomba aongezewe tunamuongezea miaka 66, akiendelea kuomba tena tunafanya tathmini amefanya vizuri ndio tunaongezea miaka 99. Kwa hivyo, miaka 99 ni *maximum* sio kama ndio chanzo chenyewe hapana.

Nam. 36

Kukosekana na Malipo ya Posho ya "*Call*" kwa Madaktari

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Ni muda mrefu sasa madaktari wa zamu za usiku hawalipwi posho za "*call*" ambazo zimekubalika na ambazo zilikuwa siku za nyuma.

(a) Ni kwa sababu gani posho hizo zimesita kulipwa kwa madaktari wanaoitwa kufanya kazi za dharura.

(b) Je, wizara yako haioni kuwa kusitishwa kulipwa kwa posho hizo kunasababisha kuwavunja moyo madaktari wetu.

(c) Kwa nini serikali isichukue hatua za dharura kuzilipa posho hizo ili kuwarejeshea moyo wa kuchapa kazi kwa bidii madaktari wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 36 lenye kifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wizara yangu inakiri kwamba kwa muda mrefu imesita kulipa maposho mbali mbali yakiwemo maposho ya "*calls*" za madaktari, hali hii imetokana na uhaba wa fedha tunazopata kutoka Serikali Kuu. Aidha, kwa vile madaktari wetu ni wazalendo, wanaijua hali ya uchumi wa nchi yetu ndio maana wakaendelea kutustahamilia na tunawaomba waendelee na moyo huo huo na wizara inaendelea kufanya mawasiliano na wizara inayohusika na masuala ya fedha ili tatizo hili liweze kupatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba hivi sasa madaktari wamestahamili kwa kipindi cha miaka mitatu na utawaambia wastahamili kwa muda gani mwengine ili madaktari hao wafanye kazi kwa uadilifu.
Pili, wizara yako kutoshinda kuwatekelezea haki yao hio, huoni kwamba wizara yako imeshindwa kutekeleza wajibu wake kwenye wizara yako.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, sisi tumeshafanya mawasiliano na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, tunajua deni letu kwao na Wizara ya Fedha imetuahidi tukimaliza bajeti watatutengea kifungu kinachohusika ili kuweza kuwalipa madaktari wetu. Madaktari wetu tunazungumza nao na hilo wanalifahamu, kama kuna utendaji wowote

hauhusiani na hilo kama ni mbaya, sidhani kama hayo yanahusiana na masuala ya posho.

Nam. 83

Elimu bila Malipo

Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa.

Nam. 213

Kufa kwa Usasi wa Kitaifa

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Hapo siku za nyuma kulikuwa na huduma ya usasi wa kitaifa, jambo ambalo liliwasaidia sana wakulima kuokoa mazao yao kutokana na wanyama waharibifu.

(a) Je, Mhe Waziri ni kwa sababu gani huduma hiyo sasa imekufa.

(b) Kwa vile huduma hiyo ilionekana kuwasaidia wakulima, Wizara ina mpango gani wa kuirudisha huduma hiyo.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 213 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa kadri tunavyokumbuka ni kuwa suala la usasi wa kitaifa halijawahi kusimamiwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili au Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka. Idara hii majukumu yake zaidi ni kuhifadhi, kulinda na wala sio kusaka wanyama, pengine ni kutoa ushauri pale inapohitajika na ikiwa ulazima wa usasi huo upo.

Mhe. Spika, suala la usasi wa kitaifa lilikuwa likiratibiwa na Wizara ya Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ chini ya Kamati ya Usasi wa Kitaifa. Wizara ya Kilimo pamoja na idara nyingine za serikali mara nyingi huwa zikiombwa kusaidia masuala ya usafiri au huduma nyengine pale zinapohitajika.

Nam. 215

Mchezo wa Mpira wa Pete Ndani ya Baa

Mhe. Nassor Salim Ali - Aliuliza:-

Mchezo wa Mpira wa Pete (*Netball*) ni mchezo unaopendwa na mashabiki wengi hapa Zanzibar na hivi karibuni tulishuhudia mashindano ya mchezo huo hapa Zanzibar kwa Timu za Afrika Mashariki, mashindano hayo yaliyofunguliwa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, waliyofanyika kwenye Uwanja wa Gymkhana, sehemu ambayo inatumiwa kuuza pombe.

Kwa kuwa Serikali imepiga marufuku kwa makampuni ya pombe kudhamini mchezo hapa Zanzibar. Je, Wizara haioni kuwa ipo haja ya kujenga kiwanja cha kisasa cha mchezo huo wa Pete na kuondoa mchezo huo kuchezwa ndani ya ukumbi wa baa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 215 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa ni kweli mashidano hayo yalifanyika sehemu hiyo na ni kwa sababu sehemu hiyo inaonekana kuwa ndiyo sehemu pekee na maarufu ya kuendeshea mashidano hayo ya kimataifa na serikali imeliona hilo. Kwa hivyo, watendaji wakuu wa masuala ya michezo kujadili matatizo ya viwanja vya michezo yote sio mchezo wa pete tu. Kwa hivyo, wizara kwa kupitia Baraza la Taifa la Michezo iko mbioni kutafuta maeneo mazuri ya kujenga viwanja vya michezo mbali mbali vyenye hadhi ya kimataifa vikiwemo vya Mpira wa Pete.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, mbali na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mchezo huu wa Pete unachenzwa pale katika uwanja wa Baa (Gymkhana), na kama majibu yake alivyojibu kwamba, viongozi wakuu wanakwenda pale kushuhudia mchezo ule na Zanzibar suala la udhamini serikali kama alivyojibu kuwa imepiga marufuku udhamini wa michezo kwa kampuni hizi za pombe.

Je, haoni kwamb aipo haja sasa serikali kuruhusu makampuni haya ya pombe ambayo yana vinywaji baridi kuruhusu mashindano haya kutumia vinywaji baridi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, hilo ni kweli, lakini wanaokuja kucheza timu za kitaifa kwenye eneo lile ni dini tofauti. Hatuwezi tukaondosha, lakini Mhe. Mwakilishi tutafuatilia ili kutafuta viwanja vyengine kujenga na kuondosha usumbufu huo.

Mhe. Nassor Salim Ali: Katika swali langu nimeuliza kuhusu udhamini wa makampuni hayo ya pombe ambayo yanatengenezwa vinywaji baridi kama vile *Vita-malt* na vinywaji vyengine ambavyo havihusiani kabisa na pombe, sio suala alilolijibu na naomba alijibu. Ipo haja sasa serikali kuangalia kuruhusu kampuni hizo kudhamini michezo ili kuondoa umasikini wa vilabu vyetu na kuinua michezo hapa Zanzibar kwa kutumia huo udhamini wa vinywaji baridi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakubaliana na wewe suala hili tutalifuatilia.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kiwanja kile kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri, ni maarufu kwa kuchezewa Mpira wa Pete, na kwa kuwa atakubaliana nami Mhe. Naibu Waziri kwamba wizara hii ndio wizara husika ambayo ilijenga kiwanja kile kwa gharama kubwa pamoja na mwenye kumiliki sehemu ile. Kwa kuwa sasa hivi swali mama limeuliza kuwa pahamwe pale. Je, atakubaliana na mimi kuwa ni bora tumuhamishe muuzaji pombe kuliko kuhama wachezaji wa Mpira wa Pete.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nitakubaliana naye Mhe. Mwakilishi hayo masuala yote ni kweli, lakini kama nilivyomjibu Mwakilishi aliyeuliza mwanzao kwamba tutalifuatilia na tutalifanyia kazi kwa hatua ambazo zinakidhi haja kwenye uwanja ule.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri nina swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, lugha za watu wanaokwenda katika vilabu vya pombe ni tofauti kabisa na lugha ambazo viongozi wetu wanatumia na wamezowea. Je, Mhe. Naibu Waziri kuanzia sasa atakubaliana na mimi kwamba ni marufuku viongozi wetu kwenda kufungua michezo katika vilabu vya pombe, kwa sababu lugha zile ambazo watazisikia pale ni lugha ambazo haziendi sambamba na viongozi wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, swali lake amelila katika mdogo sikulisikia.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, ni kwamba lugha ambazo hutumika kwenye vilabu vya pombe in tofauti kabisa na lugha ambazo hutumia viongozi

wetu. Kuanzia sasa huwezi kupiga marufuku kwa viongozi wetu wakuu wa nchi hii kufungua michezo katika vilabu vya pombe.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi hilo ni kweli, lakini wakati kiwanja kile ni cha zamani na hali ile ipo, kwa kweli tunashindwa kwenda kwenye viwanja vyengine ni kwamba tubakie pale pale. Lakini Mhe. Mwakilishi na wewe mwenyewe huwa unafika kwenye maeneo yale na ile hali unaiona, unatakiwa wewe mwenyewe uhamasishe na uweze kusimama kwenye majukwaa kuyazungumza kuhusu hali hiyo.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 - Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati

(Majadiliano yanaendelea)

TAARIFA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwaombe radhi kidogo kabla ya kuendelea na majadiliano kuna taarifa mbili. Waheshimiwa Wajumbe mtakumbuka kwamba Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora imo katika maandalizi ya utayarishaji wa Sera ya Utawala Bora pamoja na mkakati wa utekelezaji wa sera hiyo. Aidha, ofisi hiyo imo katika maandalizi ya mswada wa sheria ya kuzuia rushwa na maadili ya viongozi, ili kazi hii iwe na mafanikio inabidi ufanyike utafiti wa hali ya utawala bora ilivyo nchini na matokeo yake yaweze kusaidia katika ukamilishaji wa kazi hiyo.

Utafiti huo unafanyika kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Chuo cha Sera na Sheria cha Norway ambao wapo nchini kwa ajili ya kazi hiyo. Utafiti huo utafanyika kwa njia kuu mbili. Moja ni ya mahojiano na ya pili ni ya kujaza madodoso, madodoso yatahusu Baraza la Wawakilishi, watumishi wa umma na wananchi wa kawaida. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe tunaomba kusaidia utafiti huu kwa kujaza dodoso ambazo mtapewa na kuzirudisha kabla ya tarehe 15/07/2011 ili utafiti huu ukamilike kwa ufanisi wa hali ya juu. Waheshimiwa Wajumbe majibu yatakuwa ni siri kabisa na tafadhali tuyajibu maswali kwa umakini na kwa ukweli.

Waheshimiwa Wajumbe punde tu madodoso haya yatagaiwa kwenu ili tuweze kuyajaza na kuyaresha kama vile ilivyoombwa. Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru sana kwa ushirikiano wetu katika suala hili la utafiti.

Waheshimiwa Wajumbe tangazao la pili kama ilivyo kawaida wananchi wetu wanapenda sana kuja hapa ili kuona wawakilishi wao wanajadili mambo gani kwa ajili yao. Kwa leo tunao wageni ambao wapo ukumbi wa juu na wageni hao ni wanafunzi wa Chuo cha Elimu Chukwani, nawaomba wasimame. Wageni wetu karibuni sana muone Waheshimiwa Wajumbe wanavyoendelea na shughuli kwa ajili ya wananchi. Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni sana, ahsanteni sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii kumaliza dakika zangu kumi na mimi nitajitahidi kufanya hivyo.

Mhe. Spika, nilipokuwa nimemalizia hoja yangu kuna maneno nilikuwa sijayamaliza naomba niendelee kuyamaliza halafu ndio niendelee na hatua nyengine.

Mhe. Spika, nilikuwa nazungumzia suala la Mhe. Waziri tulimtaka kwamba atuambie lini atatuletea ile sheria yakuwezesha kufanya utafiti wa mafuta Zanzibar pamoja na uchimbaji wa mafuta hapa Zanzibar. Kwa hilo kwa sababu Mhe. Spika, tunasema kwamba katika Baraza lilopita tulitoa azimio Barazani la kuiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuondoa suala hili la mafuta. Lakini chakusikitisha Mhe. Spika, hadi leo hakuna jawabu yoyote tuliyoipata, hivyo labda Mhe. Waziri atakapokuja hapa aje atusaidie maelezo labda baada ya barua iliyotoka kwa Mhe. Waziri Kiongozi kumpelekea Mhe. Waziri Mkuu ili kuitaka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupeleka suala hilo Bungeni na kuondolewa, lakini mpaka leo kuko kimya. Kwa hivyo, tulikuwa tunataka tujue kwamba je, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweza kutoa jawabu kuhusu suala hili au vipi. Kwa sababu Mhe. Spika, hapa ndio pale wananchi wetu wakati mwengine wanapolalamikia masuala ya Muungano ndio masuala wenyewe yanakuja kama hapa.

Mhe. Spika, kwa mfano ni hivi karibuni tu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipeleka hati ya dharura Bungeni kwa ajili ya kuzungumzia suala zima la Katiba mpya wakati ni suala muhimu ambalo ilikuwa kwanza kabla wananchi wapate nafasi ya kujadili kabla ya mswada ule kupelekwa Bungeni. Kwa hivyo, suala la Katiba mpya lilionekana ni muhimu sana likapewa kipaumbele, lakini suala la mafuta kwa Zanzibar mpaka leo limefumbiwa macho na hatuju nini ambacho kinaendelea.

Kwa hivyo, kwa vile wenzetu hawakuliona umuhimu wake ndio maana tukamtaka Mhe. Waziri atuletee sheria na pia aje atwambie hiyo sheria itakuja mwezi gani kwa sababu tulitegemea kikao cha Januari ingelikuja lakini sheria haikuja, kikao cha Machi sheria pia haikuja na hiki kikao cha Bajeti tunajua

hawezi akatuletea sheria hiyo, lakini tunaamini kikao cha Oktoba anaweza akatuletea sheria hiyo. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nilikuwa nataka nipate maelezo katika hili.

Mhe. Spika, juzi nilipigiwa simu Wazanzibari wanaoipenda nchi yao wakaniambia mheshimiwa hebu nenda katika mtandao halafu fungua website ya mzalendo angalia kuna nini. Mhe. Spika, nilipoangalia nikamkuta Mhe. Waziri Mkuu Mizengo Pinda anakagua meli ambayo itakayokuja kufanya utafiti wa mafuta katika pwani ya Tanzania.

Mhe. Spika, mimi ndio nikaona mbona hili suala sisi liko kimya lakini wenzetu wanaendelea nalo. Lakini katika suala hili humu ilizungumzwa kwamba mtaomba ninukuu maneno yaliyozungumza. “Kwa mujibu wa taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu ilitoa kauli hiyo jana baada ya kutembelea eneo la kujengea viwanda ili kuona hatua mbali mbali za ujenzi na kuikagua meli ya uchimbaji wa mafuta, meli hiyo inajengwa katika Bandari ya George Kusini Mashariki yaani Korea ya Kusini Mhe. Waziri Mkuu anatarajia kuzindua meli hiyo kuanzia leo tarehe 4 asubuhi katika Bandari ya George”.

Mhe. Spika, kuhusu hili mimi nitaitoa photocopy ili niweze kuwa na kumbukumbu halafu na wewe Mhe. Spika, na wewe uweze kumuona Mhe. Waziri Mkuu anavyokagua meli hii.

Mhe. Spika, na sisi tunataka Mhe. Makamo wa Pili wa Rais na yeye apate nafasi akakague meli yakuja kutafuta mafuta Zanzibar, kwa sababu tunajua mamlala ya Mhe. Waziri Mkuu kuna baadhi ya maeneo mengine yanakuwa hayafiki Zanzibar. Kwa hivyo, ndio maana tukamtaka Mhe. Waziri aje atuletee hii sheria ili na sisi tuweze kuwa na maamuzi yetu katika masuala ya kutumia rasilimali zetu.

Mhe. Spika, mimi naomba nitoe mfano na nawaomba Wazanzibari kwamba hapa tulipitisha azimio la Baraza la Kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa baada ya uchaguzi. Mhe. Spika, Wazanzibari walilipokea kwa kauli moja suala hilo na tunawashukuru sana mashehe walikwenda katika uwanja wa Maisara pale wakaomba dua kubwa sana ili uchaguzi uende vizuri, kura ya maoni iende vizuri na baada ya uchaguzi Serikali ya Umoja wa Kitaifa iweze kuundwa. Mhe. Spika, dua ya mashehe wale Mwenyezi Mungu ameikubalia, hivyo tunawaomba mashehe wale wale waende tena Maisara wakatuombee dua ili mafuta Zanzibar yaweze kupatikana. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kwa kuokoa muda kitu ambacho ninachotaka kukisema ni kwamba Zanzibar ni nzuri sana tena sana hivyo kama tungekuwa tuna mafuta yetu hizi fukwe ambazo sasa hivi watu wanatujengea vihoteli vya kiajabu ajabu

tungeweza kuwa na uwezo tungejenga mahoteli mfano kama Kempisiki, Lagema serikali ingetafuta mwekezaji wa kuja kuyaendeleza na wananchi wetu wangepata ajira. Mhe. Spika, hapa Zanzibar tungeondokana na tatizo lilokuwepo sasa hivi kwamba hata zile ajira za mahoteli hatuzimiliki sisi, basi hata vijana wetu wanashindwa kupata ajira wanaambiwa hawana ujuzi. Sasa hivi kuna vijana wetu wanataka kwenda Qatar vijana wetu wengi tokea walipomsikia Mhe. Waziri wa Uwekezaji kwamba Qatar wanataka kujenga basi kila kijana akikuona anakuuliza vipi hiyo safari ya Qatar.

Mhe. Spika, siku moja Mhe. Rais Moi alipokuwa anakaribia kumaliza uongozi wake alisema sisi bwana viongozi wa Kiafrika tunadharauliwa sana Ulaya, wakisikia Rais anakuja wanasema hao wanakuja kuomba. Kwa hivyo, hebu na sisi tuombwe tunataka Zanzibar tuje tuombwe sisi tukiwa na mafuta tutakuwa na uwezo tutaweza kuwasaidia wenzetu.

Mhe. Spika, kwa kumalizia nakuja na suala dogo tu hili nitamuomba Mhe. Waziri aje anisaidie ufafanuzi kuna eneo hili la Kinu cha Taa. Mhe. Spika, katika eneo lile kuna eneo la wazi kwa miaka mingi palikuwa panatupwa taka na uchafu mwingi, kipindi kile tukafanya jitihada tukaweza kutengeneza pale tukasafisha lile jaa kuna mwekezaji mmoja ambaye amejenga hoteli pale maarufu anaitwa Turky aliweza kuweka ile *garden* pale. Mhe. Spika, sasa hivi pale pamebadilika pana *garden* nzuri sana.

Mhe. Spika, juzi amenilalamikia kanambia mheshimia ile garden pale tuliweka jina la Turky *square* tumeambiwa lile jina tulifute. Mimi nikamuuliza kwani hayo majina si yanakuwa yanashughulikiwa na Manispaa, akaniambia mimi niko tayari kwa vyovyote lakini nimeambiwa niliondoe nimeshaliondoa. Hivyo mimi nauliza mtu amejenga *garden* kama ile ya kisasa pahala palikuwa pana jaa leo pana bustani nzuri kuweka lile jina hivyo itaharibu kitu gani katika Mji Mkongwe.

Mhe. Spika, mimi nadhani Mhe. Rais anazungumza kauli nzuri sana ukiangalia katika vipindi anasema kwamba tutaongoza katika utawala bora, haki za binadamu, hakuna upendeleo, hakuna ubaguzi wowote. Mimi nadhani hebu twende na ile haki ambayo anaitaka Mhe. Rais.

Mhe. Spika, nafikiri suala la jina sio kitu cha kubadilisha kitu chochote, nadhani kwa kuwa yule mwekezaji ametumia fedha zake nyingi na bustani ipo nzuri basi lile jina tungelipata maelezo, kuna sababu gani au lile jina lingeharibu mandhari ya Mji Mkongwe. Pale pale Mhe. Spika, kulikuwa kuna lile eneo jengine la wazi ambalo walipewa timu ya Malindi pale katika eneo la wazi kwa mujibu ya maelezo ya wenyewe Mamlaka ya Mji Mkongwe wanasema eneo lile kwa majibu wa masharti ya *UNESCO* kwamba

haliruhusiwi kujengwa ujenzi wowote unaozidi zaidi ya mita 4 kwendea juu. Lakini Mhe. Spika, sasa hivi naona kama kumezungushwa mabati pale sijui panataka kujengwa bustani nyengine au vipi. Je, haya masharti ya Mji Mkongwe wakati gani yatakiwa yafuatwe na wakati gani yanatakiwa yavunjwe.

Kwa hivyo, sisi tunatetea haya kwa sababu *UNESCO* inatupa pesa nyingi kwa kuhifadhi ile Mamlaka ya Mji Mkongwe. Mhe. Spika, juzi Mhe. Jussa alizungumza kwamba leo Mji Mkongwe kila siku kuna majengo ya kiajabu ajabu yanaongezeka, ule Mji Mkongwe utakujakupotea utakujakuwa Mji Mpya. Mimi nadhani kama kweli Mji Mkongwe hayo wanayotwambia kama ni ya kweli basi wayasimamie isiwe leo sio sheria, halafu kesho yake inakuwa ni sheria.

Hizi sheria mimi hujiuliza zinabadilika vipi nitakuja kumuomba Mhe. Waziri aje anipe maelezo mimi safari hii nimekusudia kuzuia kifungu kimoja tu, hivi vifungu vyengine sitaki kuvizua lakini naamini Mhe. Waziri akinipa maelezo yakutosha nitakuwa sina haja yakuta kuzuia vifungu. Baada ya hayo machache Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, pia nawashukuru sana wananchi wangu wa Kwamtipura kwa kuniruhusu kuendelea kuja kuwatetea kwa maslahi ya Wazanzibari wote. Ahsante sana Mhe. Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 70 na asilimia 30 nazisubiri kidogo nikipata maeleozo mazuri nitaachia, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nikumbushe kuhusu utaratibu wa kanuni zetu suala hili la kuachia simu zikawa zinalia ovyo ovyo kwa kweli linatutaabisha zinaingilia na mazungumzo ambayo yanaendelea ndani ya Baraza. Niwaombe sana ama simu tufunge au tuziache katika maeneo yetu mengine, lakini tukiachia hii kwa kweli tunavuruga utaratibu maelezo ya mwisho Mhe. Hamza nimepata tabu sana kuyasikia kwa sababu ya maingiliano ya simu pamoja na mawasiliano yetu humu ndani. Nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe tutekeleze kanuni hiyo ili twende vizuri.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Kwanza Mhe. Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutuwezesha na kutupa uwezo kuweza kuja kuchangia wizara hii nyeti inayoongozwa na jemedari mkuu Mhe. Ali Juma Shamuhuna. Kabla sijachangia nachukua fursa hii kumpa pole jana kufungwa timu yake na Yanga.

Mhe. Spika, baada ya kuzungumza hayo pia nachukua fursa hii kuwapongeza watendaji wake akiwemo Katibu Mkuu pamoja na watendaji wengine wa wizara hii katika kuandaa kitabu hiki chenye maelezo mazuri na yenye

mpangili mzuri wa kuwaondelea shida wananchi wetu kupitia ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Spika, mimi mambo mengi yameshazungumzwa hapa na wenzangu lakini nitachangia machache hususan suala la maji. Mhe. Spika, suala la maji limekuwa ni kero kubwa kwa wananchi wa Zanzibar hasa maeneo ya Mjini na hasa katika Jimbo langu la Rahaleo. Mhe. Spika, Jimbo la Rahaleo ni jimbo la historia na ndio liloleta mambo mazuri haya ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 na sote tunafahamu hivyo.

Mhe. Spika, Rahaleo imepungua kutokana na upungufu wa maji katika jimbo hilo. Mhe. Spika, Rahaleo katika maeneo ya Shehia ya Makadara, Gulioni, Kundemba pamoja na majumba mawili ya jumba Nam. 2 na Nam. 4 kwa kweli kuna matatizo makubwa ya maji. Mhe. Spika, ingawa kuna maelezo mazuri hapa ya Mhe. Waziri na mipango mizuru ambayo tunaitegemea, lakini katika taarifa yake hapa ukurasa wa 50 kuna majaribio ambayo yamefanywa katika Shehia ya Makadara kwa kufungwa mita. Mhe. Spika, baada ya kufungwa mita zile basi ndio matatizo ya maji yamekuwa ni kero na ni tatizo sugu la wananchi kupata maji katika maeneo yale.

Kwa hivyo, majaribio yale baada ya kuleta tija lakini imekuwa ni tatizo na maji wananchi hawapati. Hivyo ningemuomba Mhe. Waziri atakapokuja kutoa maelezo yake atupe taarifa sahihi ambayo wananchi wa Jimbo la Rahaleo hasa Makadara baada ya kufanya majaribio yale ya mita katika kipindi hicho kinachokuja cha miundombinu wizara inategemea kuyafanya kwa kupitia wafadhili wa Japan, ningemuomba sana Mhe. Waziri akaangalia sana maeneo ya Makadara ili kuondokana na matatizo haya ya maji. Vile vile katika maeneo mengine niliyoyataja.

Mhe. Spika, jumba namba 4 ambalo limo katika jimbo langu ni jumba ambalo hawapati maji hata kidogo mpaka hivi leo. Ukiangalia sasa hivi tunaelekea katika mwezi wa Ramadhani wananchi wetu katika kipindi ambacho tunataka tuwaangalie sana hasa katika kipindi cha Ramadhani. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aliangalie sana suala hili na hasa watendaji hawa ambao ni mafundi wa Idara ya Maji wawajibike ili kuweza kuhakikisha kwamba matatizo ya maji yanaondoka.

Mhe. Spika, katika tatizo hili la miundombinu ndio linaleta matatizo makubwa ya maji, kuweza kuthibitisha hilo mimi pamoja na Mbunge wangu tumejitolea kuweza kutoa fedha pamoja na vifaa vya kubadilisha mifereji na mabomba makubwa ya maji katika maeneo ya Mwembeladu pamoja na jumba namba 2 kuna sehemu ambayo tayari wananchi wanapata maji. Kwa hivyo, ningeiomba

wizara ili kutuunga mkono kuhakikisha kwamba tatizo la maji linaondoka kabisa katika Jimbo la Rahaleo.

Mhe. Spika, pia nije katika suala la umeme. Mhe. Spika, jana usiku tulikosa umeme katika mji wa Zanzibar hili tatizo la umeme limekuwa ni kubwa sana. Kwa hivyo, mimi ningeiomba serikali kupitia wizara husika kuliendea mbio suala hili la umeme ili Zanzibar tuwe na umeme wetu.

Mhe. Spika, nimewahi kutembea katika visiwa vya Madagascan, Shelisheli pamoja na Mauritius na hivi vyote ni visiwa. Lakini visiwa vyote Mhe. Spika, vina umeme wake kwa nini sisi Zanzibar hatuwezi kuwa na umeme wetu na nyenzo za kupata umeme zipo. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri na mimi namuamini sana kuwa anao uwezo huo, anayo nia hiyo asijali katika kipindi cha 2010-2015 basi Zanzibar tuwe na umeme wetu. Mhe. Spika, nina hakika kwamba uwezo huo upo ni suala tu la kulivalia njuga.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo sasa nije katika suala la viwanja. Mhe. Spika, mwenzangu hapa Mhe. Hamza amelizungumza suala hili la viwanja matatizo haya kweli yapo hasa katika sehemu za maeneo ya baharini. Mhe. Spika, mimi naona serikali ipo haja kuliangalia kwa kina suala hili ili kuleta tija kwa wananchi wetu na kwa nchi yetu kwa ujumla.

Mhe. Spika, kama nilivyozungumza hapo mwanzo kwamba nimetembelea katika sehemu hizo za visiwa wale wanategemea sana utalii, na utalii ndio unajenga na unaendesha nchi ile ya Mauritius serikali katika maeneo ambayo wanayadhibiti hasa maeneo ya baharini. Mhe. Spika, sehemu hizi ni sehemu ambazo serikali inataka iziangalie sana na tukitafuta wawekezaji tusitafute wawekezaji ambao sio wakweli. Lakini tusitoe viwanja kwa wawekezaji tu kuwe na wazalendo asije tu mgeni hapa akajichukulia kiwanja. Mhe. Spika, maeneo haya nina imani kama kweli serikali au wizara italichukulia uhakika suala hili basi umasikini kwa Zanzibar utaondoka na tutapiga hatua kubwa sana kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa vile mambo mengi yameshazungumzwa hapa mimi sitaki nizungumze sana ila kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Rahaleo na mimi mwenyewe naunga mkono kwa asilimia mia mbili. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi leo kuchangia hotuba ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Lakini vile vile namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa mzima wa afya na kuweza kusimama hapa pamoja na kuijaalia nchi yetu Zanzibar kuwa

katika hali ya utulivu jambo ambalo linatuwezesha kujadili mambo yetu hapa bila ya matatizo yoyote.

Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kuandaa hotuba nzuri ambayo leo tunaijadili hapa. Kwa kuanzia moja kwa moja mimi naanza katika Mamlaka ya Maji. Mhe. Spika, kwa bahati nzuri kwanza tumpongeze Mhe. Rais kwa kutuhimiza kila siku wawakilishi wake na wabunge juu ya kuwa tutimize zile ahadi tulizoziweka, na sisi sihaba leo hapa tunatekeleza kifungu cha 88 cha Katiba ya Zanzibar ambacho ndicho kilichotupa majukumu yetu yote hapa ndio tunafanya hivyo.

Mhe. Spika, nazungumza tatizo la maji kijiji cha Moga katika kijiji hiki kuna ahadi ya Mhe. Rais aliyepita Dk. Amani Karume mwaka 2008 alitoa ahadi ndani ya msikiti wa Ijumaa wa Moga alisema kwamba mwaka unaofuata pale yaani 2009 tatizo la maji Moga litaondoka. Lakini chakushangaza Mhe. Spika, mpaka hivi sasa hakuna lolote ambalo linaendelea na ahadi ile imebakia kwenye makaratasi tu. Kwa hiyo Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri hili alione kwa sababu wananchi wetu kule zinapotolewa ahadi hasa na viongozi wakuu wanakuwa na imani kubwa kwamba itatekelezwa. Lakini badala yake panapokuwa hapatekelezwi kitu sisi tulioko kule kwenye majimbo yetu tunazidi kupata mashaka. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anambie lini tatizo hili la maji litaondoka katika kijiji cha Moga.

Mhe. Spika, pia nizungumzie tatizo la maji Chaani Masingini. Mhe. Spika, kwa bahati nzuri kisima cha Chaani Masingini kinatumiwa na majimbo karibu manne. Mahoteli ya Nungwi, Matemwe, Pwanimchangani yote yanategemea maji katika kisima cha Chaani Masingini. Lakini la ajabu kwamba Jimbo la Chaani limekuwa kivuli cha mvumo linawafunika walio mbali, ndani ya jimbo langu kuna matatizo ya maji, hapo Chaani Masingini penyewe maji hayapatikani.

Mhe. Spika, vile vile kisima hichi tangi lake linavuja kwa muda mrefu sana lakini hakuna jitihada zozote zinazochukuliwa kwa ajili ya kuyanusuru maji mengi yanayopotea. Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri atakapokuja atwambie kwamba pale halmashauri wanapata mapato na Mamlaka ya Maji inapata mapato, lakini Jimbo la Chaani lenyewe halinufaiki na chochote kazi yake kubwa ni kutoa maji tena kwa maeneo mengine.

Mhe. Spika, nizungumzie suala la maji Chaani Kubwa. Mhe. Spika, katika eneo la Chaani Kubwa kuna tatizo la maji kwa muda mrefu sana na mwaka 2008 uchimbaji wa kisima pale ulianza kwa mashirikiano ya
TASAF pamoja na Mamlaka ya Maji. Lakini hadi hivi ninavyokwambia leo kisima kimekwama *transformer* haijapatikana, tukenda Mamlaka ya Maji

wanatwambia kwamba wao wanasubiri Shirika la Umeme wakafungiwe umeme ili ifungwe mashine ya kusambazia maji. Hadi hii leo bado na miradi mingi ya awamu ya pili ya *TASAF* imemalizika sasa tunaingia katika awamu ya tatu. Kwa hiyo, Mhe. Waziri atakaposimama hapa anambie lini watu wangu wa Chaani Kubwa kile kisima chao kitamalizwa na maji yatapatikana ambayo yako safi na salama.

Mhe. Spika, nizungumzie tatizo la maji Kinyasini ambalo ni la muda mrefu nako pia huku kuna ahadi ya Mhe. Rais. Nilipouliza swali hapa niliambiwa bado mapema hata bajeti yetu haijafika lakini bajeti hii pia sijaona suala hili kutajwa. Namuomba Mhe. Waziri atuone hapa.

Mhe. Spika, mwisho namshukuru Mhe. Waziri katika suala la maji kwamba mara hii shehia yangu ya Bandamaji nimeiona humu imetajwa katika sehemu ambazo zitanufaika na mradi wa usambazaji maji vijijini. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri hili lifanyiwe haraka anione mjukuu wake kwamba napata shida kwa sababu hivi sasa watu wanataka kutupiga mawe kwa shida ya maji.

Mhe. Spika, suala la pili Idara ya Nishati na Madini. Mhe. Spika, hapa sitosema sana leo kwa sababu mwenyekiti wangu amezungumza vizuri. Lakini tatizo la uchimbaji na utafutaji wa mafuta nimnukuu Mhe. Mansoor Yussuf Himid hapa katika Baraza lililopita akiwa kama ni Waziri mwenye dhamana katika Wizara hii. Alisema kwamba "Kuhusu mafuta kuwa Baraza la Wawakilishi maamuzi ya Baraza hili la wananchi wa Zanzibar ndio yatakuwa maamuzi ya nchi yetu juu ya utaratibu, uendeshaji na mambo yote yanayohusiana na utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia."

Mhe. Spika, sijui kauli hii ni kweli kwamba sisi tumesimama hapa ni wawakilishi wa wananchi na tumesimama kwa ridhaa yao na wao ndio wanaotutuma tuseme masuala yanayowahusu wao.

Mhe. Spika, Sudan ya Kusini imepata uhuru wake juzi tarehe 9, lakini nikiangalia bajeti yao asilimia 98 inategemea mafuta. Kwa hiyo, hapa tuone umuhimu wa mafuta kupatikana. Mhe. Spika, tunamuomba Mhe. Waziri hapa kwa sababu hatutaki tena kuzungumza kwanza litolewe katika taratibu za Muungano. Tunachotaka Mhe. Spika, Mhe. Waziri atakaposimama hapa atwambie lini italetwa sheria hapa tuijadili, tuipitishe hapa na mafuta haya yapimwe kwa sababu tumechoka.

Mhe. Spika, juzi Waziri Mkuu alikuwepo nchi za nje anazungumza na wawekezaji wa gesi asilia katika Tanzania. Lakini sisi sote tuko hapa kwenye Baraza na viongozi wetu wakuu wako hapa, hatujawaona kushirikishwa

kwenda kule wakaanza kuzungumza suala la gesi asilia. Sisi tunasubiri sijui tunamsubiri nani, hakuna cha kusubiri tunachosema sisi kama ndio wawakilishi wa wananchi hapa mafuta yachimbwe hatusikii kauli yoyote tutakayoambiwa ndio kama hatujaambiwa italetwa sheria hapa.

Mhe. Spika, la mwisho Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi. Mhe. Spika, katika kitabu hichi nilichokisoma ilizungumzwa sana kwamba nyumba za maendeleo zilizojengwa na Marehemu Mzee Abeid Karume zitafanyiwa marekebisho na matengenezo. Lakini Mhe. Spika, namkumbusha Mhe. Waziri kwamba pale jirani yake Gamba ziko nyumba za maendeleo ambapo hivi sasa zinavuja kwa sababu ni za muda mrefu. Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri hili alione, pale Afisi ya Mkuu wa Wilaya tumeona imeezekwa, kwa hiyo tunaomba zile nyumba ziezekwe kwa sababu panapotezwa fedha nyingi sana za serikali za muasisi wetu.

Mhe. Spika, vile vile katika nyumba hizi suala la karo na *chamber* zake zimejengwa katika mfumo ambao sio mzuri kwa hiyo wananchi wangu wa eneo la Gamba kila baada ya mwezi wanasafisha makaro. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anipe tamaa na ahadi kwamba lini ataliona hili.

Mhe. Spika, kwa kumalizia nakushukuru na naunga mkono hotuba hii kwa asilimia 50 na mpaka nitakapoambiwa lini tutaletewa sheria ya mafuta hapa ndipo nitakapounga mkono.

Mhe. Abdulla Juma Abdulla: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu niseme machache katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Mhe. Spika, nataka nianze kwenye ukurasa wa 26 Idara ya Mipango Miji na Vijiji. Mhe. Spika, miongoni mwa kazi za idara hii kama ambavyo Mhe. Waziri katueleza hapa naomba ninukuu kidogo. Anasema "Kutayarisha mpango wa matumizi bora ya ardhi nchini *(National Land Use Plan).* Ili kufikia mpango huu idara hii itaangalia upya mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya mwambao *(Coastal Zone)."*

Mhe. Spika, nataka niseme hili kwanza kabla sijasahau, kuna matatizo makubwa sana ya matumizi ya ardhi katika ukanda wa pwani na nikisema hapa nakusudia hasa kaskazini. Mhe. Spika, wananchi wa kaskazini wamezoea na ndio asili yao kutumia maeneo yale kwa shughuli zao za maisha. Toka lilipozuka wimbi la uwekezaji wananchi wamekuwa wakikosa ardhi zao na nathubutu kusema bila ya ridhaa zao. Mhe. Spika, nakubaliana na serikali sana kwamba utalii ni nguzo moja muhimu sana ya maendeleo katika nchi yetu.

Lakini pamoja na hayo nataka nikubaliane sana na wananchi bado wana haki ya kupata maslahi ya ardhi zao hawana pengine pakwenda. Mhe. Spika,

kinachonisikitisha ni utaratibu huu unaotumika mpaka mwekezaji akapewa ile ardhi. Kuna utaratibu mrefu, ili mwekezaji awe halali basi lazima kuwe na mawasiliano kati ya mwekezaji, serikali lakini na wanakijiji ambao wengine wanamiliki zile ardhi kwa nyaraka, wengine ni ardhi halia lakini wanazitumia kwa maslahi yao kwa kilimo na vyenginevyo.
Sasa Mhe. Spika, nilikuwa nafikiria mimi serikali ingetafuta utaratibu mzuri wa kumpata mwekezaji awekeze lakini wakati huo huo kuhakikisha kwamba mwananchi nae anaridhika na anapata maslahi ya ardhi ile.

Mhe. Spika, sijafanya utafiti wa kina lakini jana nilikutana na watu wengi wa kaskazini wakaninung'unikia sana na walikuja kwa sababu bajeti ya Mhe. Waziri iko hewani. Wakanifuata wana kesi nyingi za kaskazini na wakanipa ma-*document* ambayo kama nitayasoma hapa Mhe. Spika, labda leo kutwa nzima uniachie mimi hii kazi. Sasa sitayasoma lakini ninayo haya hapa wana malalamiko mengi, kuna walionyang'anywa mashamba yao ya kurithi na nyaraka zao wanazo. Kuna wengine ni maeneo yale tunayosema ardhi halia, ni ardhi ya serikali lakini wamezuia wenyewe kutumia kwa vipando vyao vidogo vidogo kama vile viazi kwa muda mrefu.

Sasa anapotokea mwekezaji kuna wajanja kwa sababu katika maelezo haya niligundua kuna sheha anachukua mamlaka yeye mwenyewe ya kuuza maeneo tu ovyo ovyo mfano Kidoti bila ya ridhaa za wale wenyewe. Kwa hiyo, wenyewe wamefuatilia hapa na pale mara wanakwenda polisi, mara kwa Mkuu wa Wilaya, mara kwa Mkuu wa Mkoa, Wizarani lakini hatimae ufumbuzi wa matatizo yao haukupatikana mpaka leo wako hewani.

Mhe. Spika, nilikuwa nafikiri sana anapotokea mwekezaji basi ni vyema kwanza na wale wananchi ionekane maslahi yao yanakaa wapi. Mhe. Spika, ardhi inauzwa pengine mita 100 *square* kwa dola za Kimarekani 450,000 mpaka 500,000, unashangaa anaambiwa mtu anaitwa kwenda kupewa fidia shilingi 150. Kuna wengine wananambia mtu anaitwa kwa Mkuu wa Wilaya kuna fidia ya ardhi ile aliyokuwa anaitumia anapewa shilingi 20,000. Sasa huu kwa kweli si uungwana, mimi nilikuwa nafikiri sana Mhe. Waziri na nimesoma hapa kwa sababu anafanya *revision* ya mipango ya matumizi ya ardhi katika ukanda wa pwani, basi katika *revision* yake aangalie maslahi ya wananchi wa maeneo yale.

Vyenginevyo Mhe. Spika, kuna siku litakuja kutokea balaa katika nchi hii kwa sababu ardhi ni mali na wenyewe walionyang'anywa zile ardhi ambazo wamezoea kuzitumia toka enzi ya wazee wao hawakuridhika na mpaka leo wanafuatilia. Hata Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kuna *document* nyengine nimeiona kapelekewa katika masuala haya kwa hiyo naomba sana Mhe. Waziri afuatilie.

Mhe. Spika, nataka niweke azma kabisa kwamba ikiwa ufumbuzi wa matatizo haya haukupatikana basi siku za mbele kama nitakuwa bado niko hai na nimo katika Baraza hili nitakuja kuwa mtu matata sana katika masuala haya. Kwa hiyo, leo natoa kama angalizo kwa sababu sijapata muda wa kuyafuatilia nimeyapata jana tu. Lakini kuanzia sasa nitaanza kufuatilia na nione ukweli uko wapi na nione serikali imechukua hatua gani kuwarejeshea wale wananchi.

Mhe. Spika, niangalie Idara ya Mipango Miji katika suala jengine. Mhe. Spika, unajua kila uchao mji wetu unapanuka. Kuna maeneo mengi sasa wale wamiliki wa yale maeneo mashamba yao ya asili wenyewe wanawauzia watu wanajenga nyumba. Sasa pia nimeona katika hichi kitabu kwamba Wizara hii kupitia Idara hii itajitahidi kuona kwamba inaangalia upya ile mipango ya kukata viwanja katika yale maeneo ambayo mji sasa hivi unakua.

Lakini nataka niilaumu kidogo kwamba wanachelewa kwa sababu mtu anakuwa na shamba lake pengine karibu eka kumi analigawa anavyoona yeye mwenyewe. Sasa linajengwa kiholela hakuna miundombinu ya maji, hakuna barabara, hakuna umeme mtu anapenya penya tu, siku nyengine unakuwa na nyumba yako kati kati huko hata kigari hakifiki pale penye nyumba yako. Sasa nilikuwa naomba sana hii idara iwahi kufanya *survey* mle ambamo watu wanakata mashamba yao wanagawa wafike wakawapimie ili angalau wale watakaojenga pale wajenge nyumba za kisasa.

Hivi sasa kama utafanya *survey* kila pahala huoni kuna watu wanajenga, hii barabara ya kwendea Fumba ukenda mashamba huko Shakani kote watu wanakata viwanja huko lakini idara haijapita, kesho kutwa watakwenda kuwaambia mmejenga vibaya. Mhe. Spika, nilikuwa naomba sana hii idara isikae ofisini iwe sasa inapita pita. Si vibaya kama wataweka sheria hasa kwamba mtu yeyote anayetaka kuuza shamba lake basi kwanza afike kwenye wizara hii atoe taarifa. Kwa mfano, mimi nina shamba langu eka kumi nataka kuuza viwanja, sasa wizara impe watu wakampimie yule mzee ili pakijengwa pajengwe nyumba nzuri za kisasa.

Mhe. Spika, jambo jengine katika hili hili kumejitokeza manung'uniko pia, idara imekwenda imepima imeweka *beckons* kila mtu kapewa kiwanja chake. Lakini kuna wababe mtu atajenga nyumba yake anavyotaka mwenyewe akishamaliza anaona eneo lake halimtoshi kwa hivyo katika kujenga fensi anavuka mpaka kule kwenye *beckons* za watu wengine anajenga. Hili tatizo linatokea katika maeneo na linasababisha kufa kwa ile miundombinu ya barabara ambayo idara imeweka. Unakuta pahala ambapo palikuwa kwa mujibu wa *site plan* barabara inafika lakini baada ya watu kujenga sasa barabara haifiki tena. Mhe. Spika, nilikuwa naomba sana kuwe na chombo cha uratibu kwa maeneo kama haya vyenginevyo itakuwa hii kazi yetu ni bure

kugawa halafu watu wakajijengea wanavyotaka. Nafikiri Mhe. Waziri atakuwa kanisikia vizuri.

Mhe. Spika, jambo jengine niende katika ukurasa wa 55 Shirika la Umeme. Mhe. Spika, hapa nataka nisikitike kidogo kwamba waziri katufanyia hiyana na si kawaida yake kwa sababu ni mtu ninayemjua sana na ni mtu anapotoa maelezo yake huwa anatoa maelezo ya kumfanya mtu asiwe na swali la kuuliza. Lakini hapa Mhe. Spika, katufanyia hiyana kidogo, maelezo yake yamekuwa mafupi sana kiasi ambacho tuna maswali mengi ya kujiuliza.

Mhe. Spika, Shirika la Umeme bajeti ya mwaka 2010/2011 walitueleza kwamba wana mpango wa kukusanya milioni 47 na sisi tukaidhinisha hivyo, lakini katika fedha hizo zilizokusanywa ni milioni 24 ambapo ni tofauti kubwa sana si ya kawaida. Nilikuwa nadhani Mhe. Waziri asimalizie tu kutwambia kwamba wamekusanya asilimia 51, kuna asilimia 49 ziko wapi hazina maelezo, angetwambia hizi hazikukusanywa kwa sababu kadhaa.

Mhe. Spika, ndio ile hoja ya Mhe. Omar Ali Shehe kwamba ikiwa wamesema watakusanya milioni 47 lakini wamekusanya milioni 24, leo anatwambia wanataka kukusanya bilioni sijui ngapi sisi hatuamini kama wataweza na itakuwa sasa wanatudanganya. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Waziri atakapokuja kutoa ufafanuzi atwambie kwa nini asilimia 49 haikukusanywa na Shirika la Umeme.

Mhe. Spika, jengine ni mradi wa usambazaji umeme vijijini. Tumeambiwa katika ukurasa wa 59 kwamba mradi ule wa awamu ya nne umemalizika naomba kunukuu kidogo hapa “Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Umeme itahakikisha kuwa inakamilisha kusambaza umeme katika vijiji vilivyosalia kutokana na kumalizika kwa mradi ule.”

Mhe. Spika, vijiji ni vingi sana. Nataka nimkumbushe tu Mhe. Waziri kwamba pale jimboni kwangu tu pana vijiji saba havina umeme sasa hivi tena ukanda wa magharibi pekee, kuna Kilindi, Machawa, Mtemani, Kuungeni, Chanoni, Ngomeni na Banani na ninahakika kila jimbo kuna kitu kama hicho. Sasa Mhe. Waziri akitwambia kama ana mpango wa kuvimaliza vijiji vyote vilivyosalia halafu hakutuwekea hata fungu la fedha atakalotumia kufanya kazi hiyo wala hajatwambia kama kuna mhisani mwengine kaja, mimi sisemi kuwa sijaamini lakini napata mashaka kidogo.

Mhe. Spika, naomba akianza katika kuvikamilisha kwanza aje aanze kule jimboni kwangu kwa sababu hawa wananchi wana miaka 47 sasa hivi hawana umeme, hawana maji, hawana barabara na kila bajeti inasimama hapa kusema

maneno hayo. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri aje aanze kule kwa vijiji hivi.

Mhe. Spika, jambo jengine gharama za umeme sasa zimekuwa ghali mno wananchi wanashindwa kuvuta umeme, sasa sijui pengine ni kupanda kwa gharama za vifaa. Lakini naomba sana shirika lifanye huruma wale wananchi ambao wana nia ya kuvuta umeme lakini hawawezi kutokana na gharama wawakopeshe halafu watakuwa wakiwalipa kidogo kidogo.

Mhe. Spika, kwa kweli juhudi za kupata umeme mbadala zinakwenda taratibu sana na hii mara nyingi nilikuwa nikisema kwamba kuna haja ya serikali kuharakisha hili kwa sababu umeme tunaoutumia sasa hivi mimi nauita ni umeme usiokuwa na uhakika. Usiokuwa na uhakika kwanza kwa sababu Shirika la Umeme Zanzibar na *TANESCO* ambako ndio tunagaiwa umeme kuna migogoro ya hapa na pale ambayo haipati usuluhishi kila siku. Lakini la pili Mhe. Spika, huu umeme wenyewe ni ghali sana. Kwa hivyo, nafikiri serikali ifanye juhudi za makusudi za kuharakisha huu mpango wa umeme mbadala tuna *sources* nyingi tu hapa tunatajiwa kila siku. Upepo tulionao unatosha, jua tunalo hapa linatutosha, mawimbi ya bahari yanatosha, lakini kila kitu inakuwa ni hadithi iliyokuwa haifikii mwisho. Naomba sana hili lizingatiwe.

Mhe. Spika, jambo jengine watu wa Tundauwa wananituma kila mara niihimize serikali wapatiwe maji kwa sababu maji yao wanayokunywa wewe huwezi kuyatumia hata kwa kunawa uso. Sasa nimeisoma sana hii hotuba ya Mhe. Waziri lakini bado. Mwaka jana Mhe. Waziri aliyemaliza muda wake katika wizara hii alinambia kuwa atatuma watu wake waje wafanye *survey* kule waone namna ya kupata maji lakini mpaka leo jitihada zile zimeganda. Kwa hivyo, hapa leo nakumbusha tena watu wa Tundauwa wanahitaji maji.

Mhe. Spika, nataka nimalizie sikuwa na nia ya kuzungumza suala la mafuta leo kwa sababu tumeshalisema sana. Lakini kwa kweli nimetisika sana na *statement* ya Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba Mhe. Waziri Mkuu ambaye alisema Zanzibar si nchi leo anakwenda kukagua meli itakayokuja kuchimba mafuta Tanzania tukiamini kama Tanzania Bara hawana mafuta, tulionayo ni sisi Tanzania Visiwani. Kwa hivyo, maana yake anataka kuja kuyachimba huku mafuta yetu bila ya kushauriana na sisi wenyewe.

Mhe. Spika, kama hilo halitoshi kuna mtu kanihadithia. Unajua miongoni mwa maeneo yaliyo na mafuta kule kisiwani Pemba ni ule mwambao wa bahari ya kaskazini kule Kigomasha. Wale watafiti walitwambia kama kule pia wameona mafuta mengi. Sasa kuna mtu kanihadithia kama miongoni mwa watu wanaofanya juhudi ya kuchimba mafuta moja ni Kenya. Wataalam wanasema

unaweza uka-*drill* hapa *vertical,* halafu ukenda *horizontal* karibu kilomita tatu kufuata mafuta yaliko. Mkenya akikaa pale Mombasa akifanya hivyo atayavuta mafuta yetu yaliyoko Kigomasha bila ya wenyewe kujua.

Sasa Mhe. Spika, Mhe. Waziri atupe msimamo mafuta ni yetu au ni ya watu. Maana yake Mhe. Spika, juzi nilikuwa nasikiliza Bunge na nilipokuwa nachangia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais nilisema hapa kwamba mafuta tayari Baraza la Wawakilishi tumeshaamua kama ni ya Wazanzibari kilichobakia ni Wabunge kwenda kukaa kule wakalitoa katika Katiba. Lakini jambo ambalo Baraza la Wawakilishi limeshaamua halafu Mhe. Spika, jambo hili linawekwa kwenye kero za Muungano likajadiliwe tena maana yake ule uamuzi wa Baraza hauna maana.

Mhe. Spika, Mhe. Makamo wa Pili wa Rais akanijibu kwamba hili halikuwekwa kwenye kero lakini viongozi tu wa Serikali ya Zanzibar na viongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wanakaa kulimaliza.

Mhe. Spika, juzi nilipokuwa nasikiliza Bunge kuna Mbunge alikuwa anataja mambo ya Muungano na hili kalitaja tena, tena kalitaja Bungeni wala hakuna taarifa iliyotolewa pale kwamba lile suala la mafuta halimo katika kero, Bunge lote lilinyamaza kimya, mimi niliamini kama limo ndani ya kero. Sasa Mhe. Spika, Mhe. Waziri akija atwambie na hii ni kero au si kero. Mhe. Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando): Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye bajeti hii ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri kwa hotuba ndefu kabisa lakini yenye mtazamo wa kinchi zaidi. Namshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kututayarishia hotuba hii.

Mhe. Spika, wenzangu waliotangulia wameshapita sana katika hotuba hii kwa hiyo mimi nitachupia chupia tu niweke msisitizo kidogo. Mhe. Spika, nianze na ukurasa wa 14 kwenye suala la ardhi. Mhe. Spika, kumekuwa na matatizo mengi sana ya ardhi, migogoro au uvamizi wa ardhi hasa katika maeneo ya wazi na maeneo ambayo yanamilikiwa na serikali. Hili tatizo limejitokeza sehemu nyingi sana, hata wiki iliyopita nilikuwa na swali hapa la msingi nilikuwa nauliza juu ya uvamizi ambao umefanyika katika eneo la Chuo cha Utalii Maruhubi. Nilipouliza hapa jawabu nililopewa niliambiwa kwamba hapakuvamiwa.

Lakini Mhe. Asha Bakari Makame hapa aliuliza swali la nyongeza ikabidi tutoke kitume kidogo twende tukaangalie pale pahala na tulipokwenda tuliona

kweli pamevamiwa. Tukathibitisha sote akiwemo Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na maafisa wao. Sasa namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atueleze mgogoro ule umefikia wapi na hatua gani zimechukuliwa katika uvamizi ule.

Mhe. Spika, nizungumzie ukurasa wa 37 Idara ya Nyumba na Makaazi. Mhe. Spika, idara hii inashughulika na nyumba zinazomilikiwa na serikali ambazo zinakodishwa na watumishi na watu wengine. Kumekuwa na matatizo pale hasa ya ulipaji wa kodi za nyumba zile, watu wanaishi lakini hawalipi kodi na kodi yake ni ndogo sana. Maana kwa nilivyouliza kama 12,500/= kwa nyumba, hizi nyumba za maendeleo na hao walisolipa miongoni mwao ni sisi wengine viongozi wakubwa kabisa. Tuna mishahara minono na mizuri tu, tunazo nyumba nyengine karibu tatu tatu, lakini na pale tumechukua nyumba zile. Ukiangalia nyumba zile za Kwa Mchina, nilipoangalia *query* ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, tume majina ya baadhi ya viongozi hawalipi kodi.

Sasa huyo Mkurugenzi wa Idara ya nyumba atamkaba vipi waziri wake. Sina uhakika mfano waziri wake au Mhe. Waziri, atamkaba vipi. Namuomba Mhe.Waziri atupe mkakati ambao umeandaliwa na hii idara wakishirikiana na yeye mwenyewe kuisaidia hii idara ili kuhakikisha kwamba wale ambao hawalipi zile kodi basi walipe. Hizi kodi ni za serikali na ni pesa ya wananchi hii, haiwezekani mtu akakaa nayo tu. Kodi halipi na nyumba hataki kupisha, kazuia nyumba na kodi halipi. Mimi ningekuomba sana Mhe. Waziri hebu tusaidiane katika hili, umsaidie huyu mkurugenzi wako, maana huyu ni mdogo sana lakini wanaozizuia nyumba ni wakubwa. Sasa hebu tia kifua chako Mhe. Waziri ili kuhakikisha kwamba madeni haya yanalipwa haraka iwezekanavyo.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nisogee kwenye ukurasa wa 48 kwenye Mamlaka ya Maji. Mhe. Waziri kama unavyofahamu maji ni kitu muhimu sana kwa kila mwanadamu. Lakini nataka nikuambie kwamba kuna vijiji mpaka hii leo havijapata maji safi na salama huko kwetu. Huu ni mwaka wa 47 tangu Mapinduzi au mwaka wa 48 unaingia sasa, bado vijiji hivyo havijapata maji salama mpaka hii leo ninavyokuambia. Tunapata ahadi lakini utekelezaji hatuuoni.

Mimi nakuomba sana Mhe. Waziri utakapokuja hapa hebu tusaidie kwenye vijiji hivi hasa vijiji vya Muange, Kibeni Bondeni, Kibeni Juu, Kivunge Bondeni ni lini tutapata maji ya uhakika kule. Nimeshakuja kulalamika sana wizarani kwako kwenye mamlaka hii nimeshapewa maofisa nimekwenda nao kule, tumezunguka kwa miguu kule karibu toka asubuhi hadi jioni kupima maeneo tofauti, lakini sijapata jibu la upimaji ule ambao tuliupima yaani matokeo yake. Kwa hivyo, nakuomba sana Mhe. Waziri utakapokuja hapa

naomba matokeo ya upimaji ule na hatua gani ambayo Wizara yako inachukua juu ya upatikanaji wa maji katika maeneo yale.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nije kwenye Kisima cha Kiashange. Mhe. Waziri tuna visima viwili pale kuna kisima cha Kiashange kile kikubwa na kisima kidogo kinaitwa Kwa mzungu kinachopeleka maji Matemwe. Kisima kile kina zaidi ya mwaka wa pili kimeharibika *pump* yake na hakijatengenezwa mpaka hii leo. Mhe. Waziri tueleze nini hasa tatizo la kisma kile kuwa mpaka hii leo hakiwezi kupeleka maji kwa wananchi wa Matemwe kule, wanapata tabu kwa sababu kile ndio kisima pekee wanachokitegemea. Ina maana sasa tutowe maji katika kisima cha Kiashange kuwasaidia wenzetu wa Matemwe, wakati sisi wenyewe kuyapeleka huku juu yenyewe hayatutoshi, kwa sababu kisima cha Kiyashange kinapeleka maji mpaka Nungwi. Kwa hivyo, huku yenyewe hayatoshi na kupeleka kule na kule nako kugumu na hii *pump* haitengenezwi. Hetu tuambie nini tatizo la hiki kisima cha Kwa mzungu kikawa hakifanyi kazi.

Mhe. Spika, hapo hapo kwenye kisima cha Kiashange kulikuwa na jenereta ambalo lilikuwa linasaidia wakati linapotokezea tatizo la kukatika kwa umeme. Linawashwa jenereta lile maji yanasukumwa tunaendelea kupata maji. Lakini jenereta lile lilikuja likaondoshwa katika kisima hiki cha Kiashange kizima, likapelekwa kwenye kisima cha Kwa mzungu ambacho hakitowi maji. Matokeo yake umeme unapozimika kisima hiki cha Kiashange hakina umeme jenereta halipo, kwa hivyo kama hakupatikanaji maji kama ni siku mbili au ni siku tatu. Tunaomba Mhe. Waziri utakapokuja tupe maelezo ya kutosha kabisa kwenye suala hili. Kuondosha jenereta katika kisima kizima na ukalipeleka katika kisima kibovu, maana kile ndio kibovu *pump* haifanyikazi umelipeleka kule, umeondosha huku ambako ni kwenye kisima kizima.

Sasa Mhe. naomba maelezo katika hili ili wananchi wetu kule waweze kuelewa sababu za msingi. Kwa sababu hivi juzi tu tumekaa siku mbili hakuna maji, kwa sababu ya umeme tu. Jenereta lile hapo kwenye kisma cha Kwa mzungu limeshaondoshwa, maana lilipopelekwa pale liliangushwa likaharibika, kwa hivyo limeondoshwa pale halijarudishwa tena mpaka hii leo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri utakapokuja naomba maelezo ya kutosha katika hili, kama si hivyo kidogo kwenye suala hili itabidi tuzuiane ili wananchi wetu waelewe kwamba hili tatizo liko wapi. Bila ya hivyo Mhe. Waziri hapa nitakutaka radhi kidogo.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nije kwenye Mji Mkongwe, katika ukurasa wa 44 Mhe. Waziri umetueleza mengi kidogo juu ya Mji Mkongwe na mambo ambayo unategemea kuyafanya kwenye Mji Mkongwe. Mimi nakwenda kwenye eneo lile la urithi, hasa eneo hili ambalo ulizungumzia kudhibiti ujenzi

katika eneo la Mji Mkongwe. Umetoa maelezo hapa ya kudhibiti namna hatua zinavyochukuliwa za kisheria kwa wale ambao wanajenga ovyo.

Mhe. Spika, mimi napata shaka kidogo hapa. Mhe. Hamza Hassan alizungumza kuhusu suala hili, kuna ujenzi pale unataka kufanyika katika Mji Mkongwe. Pameshazungushwa mabati ambapo hapa umepaelezea kwenye eneo la Mambo Msiige, umetoa maelezo kidogo mmeshakaa na UNESCO kujadiliana juu ya jambo hilo. Lakini mimi nilikuwa napata shaka kidogo. Nahisi kulikuwa kuna jengo pale, wanaliita la Starehe Club limevunjwa kabisa, ili upatikane upanuzi wa lile eneo kwenda mpaka kwenye ile bustani. Sasa Mhe. Waziri hao UNESCO hamjakubaliana lakini nyinyi mmeshavunja kabisa pale. Je, watakapokuja kukataa kwamba ujenzi ule wao hawautaki, huoni kama serikali itakuwa imeshaingia hasara. Kwa sababu mkija kujenga hizi fedha ambazo tunazipata kutoka UNESCO kwa ajili ya urithi wa Mji Mkongwe tutakuwa hatuwezi kuzipata tena.

Mhe. Waziri, hebu tueleze sababu za msingi hasa zilizopelekea kutangulia kufanya haya mwanzo kabla kuelewana na hawa, maana hawa ndio wanaofadhili huo Mji Mkongwe. Lakini naona wizara imekuwa na haraka zaidi katika kulifanyikisha hilo ambalo hukulieleza, mimi nahisi kwamba kutakuwa kuna mwekezaji labda anataka kuekeza kwenye jambo zito kabisa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri utakapokuja kidogo naomba maelezo yatakayonitosheleza ili kuona umuhimu wa kuwepo kule tukausamehe hata huo Mji Mkongwe kwamba hautupatii kitu, labda huyu mwekezaji atakayekuja atakuwa anatupa zaidi, ingawa suala hili linaulizwa mara nyingi sana, lakini maelezo yake kidogo mimi nahisi yana utata, haupatikani ufumbuzi wake wa moja kwa moja. Tulipata jibu kwa Waziri wa Fedha hapa na akatupa maelezo mengi tu na leo hapa kwenye kitabu chako tunaona maelezo mengine kabisa. Kwa hivyo, utakapokuja Mhe. Waziri naomba sana utusaidie maelezo ya kutosha ili tuweze kujiridhisha katika suala hili.

Mhe. Spika, nije kwenye ukurasa wa 55 kuhusu Shirika la Umeme. Mhe. Waziri Shirika la Umeme linajitahidi kufanya kazi zake sana kwa kadiri linavyoweza, lakini mimi nahisi bado kuna tatizo. Tatizo ambalo tunalipata hivi sasa ni suala zima la unapozimwa umeme kutoka kule kwa wenzetu, sikioni chanzo mbadala cha umeme. Hebu Mhe. Waziri tueleze kwa kina mbadala ya umeme huu unapozimika ni umeme gani tutakaoupata, kwa sababu. Mhe. Spika, Shirika hili lilipata majenereta, kuna wafadhili huko walitupa majenereta hapa, lakini cha kushangaza majenereta yale mpaka leo hii hayajafanyakazi. Sasa sijui Mhe. Waziri atatuambiaje juu ya majenereta yale tangu yalipokuja mpaka hii leo umeme unazimwa masaa kadhaa wa kadhaa. Siku nyengine kuna maeneo siku mbili mpaka siku tatu wanapata matatizo ya umeme, lakini hatuone kufanya kazi zake yale majenereta.

Hebu tupe suluhisho la majenereta yake Mhe. Waziri, tatizo ni nini, maana tunapata maneno mengi mara mafuta hakuna, mara majenereta yenyewe nusu mabovu na nusu mazima, hebu tupe ukweli wa jambo hili, ili wananchi wapate kujua ukweli hasa wa jambo hili ni nini. Ni majenerera mabovu, wataalamu wetu haba hawawezi kuyawasha yale au tuna tatizo gani. Kwa sababu kuwepo kwake pale yale majenereta halafu huku tunaendelea kukaa kiza, ile mantiki ya kuwepo kwake haionekani au haipatikani. Sasa wananchi wanajiuliza sana juu ya suala hili. Mimi nafikiri ni wakati muafaka Mhe. Waziri ukajakutupa hasa kwa kina, usitubakishie ili tuweze kujua angalau na sisi tuweze kuwaambia kwamba jamani yee haya kumbe sio mabovu ni mazima, lakini yanatushinda uendeshaji au haa! Haya jamani hee kuna matatizo ya kiufundi yalikosewa basi tuweze kujua.

Vile vile kwenye suala zima la upatikanaji wa umeme kwenye maeneo ya vijijini. Mimi katika jimbo langu kuna maeneo hadi hivi sasa hayajapata umeme Mhe. Waziri. Tumeshaandika na tumeshakuja na wataalamu, wanakagua, wanapima sijui nguzo ngapi na waya ngapi na vitu vyengine lakini mpaka leo kimya. Sasa nimeona kuna miradi humu ya umeme vijijini, Mhe. Waziri tusaidie utakapokuja kwenye jimbo langu hasa, sikuona kutajwa nimeona baadhi ya vijiji vingine vimetajwa humu. Kwa hivyo, na sisi tueleze umetuandalia nini. Kuna maeneo ambayo umeme upo hayo hayo ya vijijini, lakini wananchi wanashindwa kwa gharama, gharama za uungaji umeme zimekuwa kubwa mno, wananchi wetu maskini hawawezi kulipa laki nne na nusu au tano kwa mkupuo.

Mhe. Spika, hebu Shirika la Umeme liangalie uwezekano wa kuwa linawawekea umeme, kwa sababu watakuwa ni wadau wao, basi waweze kuwakata kidogo kidogo kiasi cha kwamba mtu aweze kulipa hata kama atachukua miaka miwili au mitatu. Lakini kwa kusema wote wakalipe kama walivyowengine wenye uwezo inakuwa tabu. Hii nchi wenyewe tunaambiwa ni wakulima na wakwezi hawana kitu hawa. Ningekuomba sana Mhe. Waziri hebu fanya utaratibu tukaona uwezekano wa wananchi wale ambao wanahitaji hii huduma, hakuna mtu ambaye hahitaji umeme, lakini kinacho shindwa ni gharama ambazo ni kubwa mno. Aidha, kuzipunguza na huko kuzipunguza kwenyewe basi tupatiwe angalau kwa mkopo, ili wale wananchi wetu waweze kufaidika na huduma hii. Kama si hivyo itakuwa ni hadithi tu hii, kwa sababu hawawezi kuihimili hii bei ambayo ni kubwa mno ukilinganisha na vipato vyao wanavyovipata kule. Kwa hivyo, ningekuomba sana Mhe. Waziri hili mkaliangalia, ikiwezekana basi mtusaidie ili wananchi wetu waweze kupata huduma hii.

Baada ya hapo Mhe. Spika, nije kwenye ukurasa wa 61 katika Idara ya Nishati na Madini. Kwenye idara ya Nishati na Madini na mimi nisogee hapo hapo

walipogusa wenzangu, kuhusu suala la mafuta. Mimi naungana mkono na wenzangu waliotangulia wote kudai suala hili. Kwa kweli Mhe. Waziri kama hukuja na jibu la kuturidhisha hapa, mimi ni miongoni mwao ambao hii hotuba yako kwanza siendi mia kwa mia nakwenda hamsini tu, mpaka tupate maelezo ya kututosha basi na mimi ndio nitakuja huko.

Mhe. Spika, wenzetu wanaonekana hawana nia safi katika hili, tuambizane ukweli. Wamezungumza wazungumzaji waliopita hapa, ni kweli na mimi nimeiona kwenye magazeti Mhe. Pinda yuko South Korea anakagua meli ambayo itakuja kufanya uchunguzi wa mafuta katika bandari ya Pwani ya Tanzania, sijui Mhe. Waziri utakuja kutueleza nini hapa katika wizara yako, kuna maofisa wowote ambao waliandamana na Mhe. Waziri Mkuu kule kwenda kuangalia labda. Maana tunaambiwa hili suala ni la Muungano, sasa mwenyewe Mhe. Waziri upo hapa, labda kwa sababu ya bajeti. Kuna wowote ambao walifuatana na Mhe. Waziri Mkuu kwenda kule kuangalia ili labda katika meli zile na sisi tutakuwemo katika mpango huo wa utafutaji au wa ukaguzi wa hayo mafuta. Mhe. Spika, katika hili mimi namuomba sana Mhe. Waziri atutayarishie majibu mazuri mno, kama si hivyo bajeti hii hasa fungu hili basi tuna nia ya kulizuia.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, mimi naiunga mkono kwa asilimia 50 bajeti hii, nitakamilisha baada ya kupata majibu ya haya maswali yangu ambayo niliyawasilisha kwake Mhe. Waziri, hapo ndio nitatimiza kama yatakuwa yamenitosheleza hayo majibu yake, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa fursa hii. Pili nimshukuru Mhe. Waziri kwa kutusomea bajeti yake ya makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2011/2012.

Pia Mhe. Spika, niwashukuru watendaji wakuu wa wizara hii. Mimi kwanza naanza na tatizo sugu ambalo linatukabili katika mji wetu huu Unguja na hasa Mjini. Kwa vijijini nashukuru na huona choyo ninapokwenda vijijini mara nyingi maji yanapatikana, lakini katika mji wetu huu ni tatizo sugu kabisa. Sasa hivi tumekuwa wanawake tunaota vipara kwa suala hili la maji.

Mhe. Spika, miradi mingi imeanzishwa ile ya kupatikana maji, lakini bado tatizo ni sugu. Mhe. Spika, nasema maji yapo na ni mengi tu, lakini ni matatizo ya utendaji au watendaji. Mimi na Wawakilishi wenzangu wa Jimbo la Magomeni na Kwahani tulikwenda mbio sana kuhusu suala la maji, tumekwenda Mamlaka ya Maji mara nyingi kutafuta ufumbuzi ili wananchi wetu wapate maji. Tulikwenda mpaka visigino vimetaka kuchunika lakini bado mpaka leo hii tatizo la maji lipo. Mwisho tulifanya uchunguzi, tuliambiwa kuna watendaji ambao hawa wamepewa mamlaka ya ufungaji wa maji kila eneo.

Kwa mjini Magharibi na kwengineko, basi tukawaambia twendeni tukaone moja kwa moja jinsi mnavyofungua maji.

Lakini kwa bahati siku moja tulitoka nao mpaka kwenye koki ile ya maji, lakini *Wallah* walishindwa kuyafungua maji pale, tukawaambia funguweni tuone. Lakini tulisimama nao pale kwa muda wa sijui saa moja na nusu mpaka baadae sisi tukaingia kwenye magari na wao ndio wakafungua maji pale, kwa vile walivyotaka wao. Ni kwamba maji yapo lakini hao watendaji ndio waliokuwa tatizo. Kwa kweli nikisema kwamba wanalojukumu kubwa na kesho kwa Mwenyezi Mungu pia watakwenda kuulizwa, kwa sababu kuna watoto wachanga na kuna watu waliokuwa hawajiwezi na wanataka huduma hii lakini hawaipati.

Kwa hviyo, Mhe. Spika, hili ni tatizo nasema Mhe. Waziri ni lazima alifanyie kazi, kuna watendaji ambao wanafanya kwa makusudi, sijui kama ni kwa kuipaka matope serikali au vipi, ionekane kwamba haichukuwi juhudi, lakini maji yapo ya kutosha.

Suala jengine Mhe. Spika, ni Shirika la umeme. Shirika la Umeme linajiendesha kibiashara, sasa ili iboreshe biashara hiyo basi kuna mambo ni lazima wao wenyewe wayashughulikie. Tatizo lipo kwamba mimi ninapotaka kuunga umeme pengine masafa sio madogo, nitakapokwenda pale kwanza nitaambiwa nitafute nguzo, pengine itanigharimu hata milioni mbili kutokana na masafa. Kwa hivyo, ilikuwa Shirika la Umeme pale ichukuwe juhudi ili kunisogezea zile nguzo za umeme, lakini mimi wataniambia ninunuwe nguzo za umeme, nitanunua lakini wakati huo huo anapotokezea tena mwenzangu anataka umeme mimi sipati tena fidia yoyote. Kwa hivyo, hili ni tatizo, ukishauvuta tu umeme mwenzio siku ya pili anavuta na pengine ulimshauri, lakini bado hakutaka kuungana na wewe mkono, lakini ikishafika tu huduma ile pale basi utaona kila mmoja anavuta huku na kule, halafu wewe unakuwa hulipwi fidia yoyote. Kwa hivyo, ningependa Shirika hili la Umeme basi kama ni biashara kuna mambo wawe wanayasimamia wenyewe.

Jengine Mhe. Spika, niende kwenye Idara ya Ardhi na Upimaji. Kwanza nitowe malalamiko yangu juu ya idara hii. Kwa kweli suala hili mpaka jana limeulizwa na wananchi wangu. Tuliomba kujenga kituo cha polisi katika jimbo letu, lakini kwa bahati taratibu hazikukamilika, nakubali hiyo kwamba taratibu hatukuzikamilisha. Tuliona kuwa idara hii pamoja na sisi wanasiasa malengo yetu ni mamoja kwamba tunataka maendeleo ya wananchi, lakini kwa bahati mbaya au nzuri tulipoanza tu hili suala la ujenzi, walikuja wahusika wa ardhi na upimaji na wakatuambia kwamba tumevunja sheria na tulikubali. Hili suala ni mimi na mbunge wangu, hii ni ahadi ambayo aliitaka mbunge wangu na kwa sababu na mimi ni kiongozi katika jimbo hili nikasema na mimi hii ni ahadi

yangu. Tunajuana sisi wawakilishi kwamba uwezo wetu ni mdogo, lakini nikasema japo dirisha moja na mlango mmoja kwa uwezo wangu kama ni kiongozi.

Mhe. Spika, kilichonisikitisha ni kuwa idara hii inaonekana sijui kama Mkurugenzi yeye mwenyewe hana mamlaka au vipi. Mimi nilishangaa kwa sababu kila jambo linakwenda kwa daraja. Mhe. Rais amewachagua mawaziri, Wakurugenzi na Makatibu Wakuu, kwa hivyo kila mtu anakuwa na jukumu lake. Sijui leo waziri kachaguliwa na Rais halafu kila kitu akaamuwe Rais huko juu, sijui kama ni utaratibu au ndio *separation of power* au vipi. Kwa hivyo, kwanza namlaumu mkurugenzi kuhusu suala hili, kwanza ilikuwa tuwasilishane mimi na yeye sio lifike kwa waziri moja kwa moja sijui ilikuaje. Kwa sababu najua wanawake sote ni walezi na tunapenda maendeleo sana. Sijamsikia mwanamke hata mmoja kugonga kibuti hapa.

Kwa hivyo, na mimi angalau Mhe. Waziri aniambie suala langu hili limefikia wapi, niliambiwa kwamba pale pahala panataka kupita njia, lakini niambiwe hiyo njia anataka kujenga nani na inajengwa lini. Kwa sababu mimi napata maswali mengi jimboni kwangu kuhusu suala hili na hili suala limenielemea mimi zaidi kuliko hata huyo mbunge. Kwa sababu tulipoanza hili suala mbunge alikuwa hayupo na mimi nikabeba jukumu hili kwamba hili ni jukumu langu, kwa hivyo yale mabomu yote napigwa mimi, naambiwa kwa nini. Halafu wale waliokataa kwamba pale pasijengwe wale ni wapita njia tu, ni vijana ambao wanakiwanja cha mpira pale. Mimi nasema kama ni viongozi basi tupite tuone.

Mhe. Spika, viongozi tulivyoambiwa kuwa wewe mwenyewe uwe mfuatiliaji. Kwa hivyo, alivyosikia Mkuu wa Mkoa alifuatilia pale na akajakuona, akasema hapa pahala panastahiki na kutokana na matatizo mengi yanayotokea pale na hivi sasa ndio yalioko. Wanawake wanadhalilishwa. Samahanini. Keshafika mwanamke pale kafikichwa sehemu zake za siri kwa mchanga, jamani ni kweli hiyo. Kweli tunawapenda wananchi wetu, isitoshe ukipita na kibaskeli pale unanyang'anywa na kama hukupita na kitu unapigwa, unaambiwa kwa nini ukapita hapa. Kwa hivyo, lile suala ni la msingi pale pahala panahitajika. Sijui kama hao wanaokataa kwamba pale pasijengwe kituo cha polisi sijui wana nia gani. Mimi nitasema hao ndio katika wale watu wabaya na wenye dhamira mbaya.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba, kwa sababu wajumbe wengi wanaokuja hapa wanajinasibu sana, mimi nina rafiki yangu, nina swahib yangu. Mimi huyu ni mume wangu Mhe. Spika. Mhe. Waziri nasema ni mume wangu. Kwa kule kwetu Donge nasema huyu ni mume wangu na ninajua kwamba hili suala atalichukulia hatua kwa kunisaidia mimi kama ni mtu wake wa karibu, hili jambo alichukulie kwa hali yoyote na mimi naomba anisaidie.

Mhe. Spika, sitaki tufike pahala ambapo si pazuri, mimi najua atanisaidia sana na wala sina haja ya kusema kwamba nimkwamishe kwa sababu najua nikimkwamisha yeye basi nimekwamisha na Jimbo la Donge. Kwa hivyo, kwa haya machache naomba kuunga mkono hoja mia kwa mia.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, lugha za *lobbing* katika Baraza zinaruhusika sana, hata mawaziri wanapoomba bajeti ipitishwe wanafanya *lobbing* kubwa na wajumbe basi wana haki hiyo. Mhe. Fatma Mbarouk Said alikuwa anafanya *lobbing*.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kwa ajili ya kutoa mchango wangu katika Hotuba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuweka hapa tukiwa na afya njema, wazima na nguvu za kuweza kulitumikia taifa letu. Vile vile sina budi kumpongeza Waziri wetu, Naibu wake pamoja na watendaji wote kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kututayarishia hotuba hii ambayo ina mwelekeo mwema, tena mzuri. Kwa hivyo, tunaomba kwa Mwenyezi Mungu kwamba utekelezaji wa hotuba hii uwe mzuri. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi moja kwa moja naanza na ukurasa wa nane kuhusu Uendeshaji wa Kazi na Utumishi. Katika ukurasa huu Mhe. Waziri amesema kwamba ameajiri wafanyakazi kadhaa. Sasa naomba nijue wafanyakazi hawa aliowaajiri wanawake ni wangapi na wanaume ni wangapi. Hilo moja.

Vile vile katika ukusara wa tisa amesema kwamba kumetolewa mafunzo kazini, yaani mafunzo katika kazi wamepewa wafanyakazi 55 mafunzo ya muda mrefu na wafanyakazi 35 mafunzo ya muda mfupi. Vile vile katika hili naomba nijue ni idadi ya wanawake wangapi ambao wamefaidika na mafunzo hayo.

Mhe. Spika, nianze mchango wangu kwa kuzungumzia suala moja ambalo linanipa utata hasa katika umiliki wa ardhi. Kwa kweli watu wengi vijijini wanamiliki ardhi pamoja na mashamba, lakini bado kumekuwa hakuna Hatimiliki, yaani watu wengi hawajui taratibu za kupata hati wananchi na wengi wao wanapofika pale mara nyingi wanambiwa ni gharama. Kwa hivyo, mimi namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, atueleze ni mbinu gani ambazo watazitumia, ili kuhakikisha kwamba wananchi wote wanapata uelewa wa kujua vipi wataweza kupata hati zao za ardhi ambazo wanazimiliki.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nataka nizungumzie kuhusu udhibiti wa ujenzi holela. Mhe. Spika, katika ukurasa wa 22 pametolewa pale mbinu

ambazo zitatumika katika kudhibiti ujenzi holela. Kwa kweli tatizo bado hatua hazijachukuliwa na hilo ni tatizo kubwa, kwa sababu tunazungumza lakini utekelezaji ni mdogo sana na tukiupa asilimia basi labda ni asilimia 2 au 3, inawezekana hatujui wanatekeleza hatujui. *(Makofi)*

Kwa hivyo, watueleze katika udhibiti huu mambo mangapi ambayo tayari yameshafanyika. Mhe. Spika, nakumbuka kipindi cha nyuma Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alikwenda katika maeneo fulani na akazuia ujenzi, lakini sehemu zile bado zinaendelea kujengwa. Sasa nadhani ni vyema Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, akatueleza kimetokea nini hapa.

Vile vile kumekuwa na mtindo kwamba watu wanaamua tu, ikiwa anataka kujenga au kuzidisha nyumba yake basi anafanya bila ya kibali. Sasa sijui wizara yako Mhe. Waziri inachukua hatua gani kwa hili, kwa sababu haiwezekani mtu yeyote kufanya *extension* ikiwa pengine nje au hata ikiwa ndani lazima apate kibali mimi najua hivyo. Kwa hivyo, kwa nini mtu anaachiwa anafanya *extension* nje ya mipaka yake anaachiwa na anafanya na inafikia hatua pengine anachukua sehemu ya mwenziwe.

Kwa mfano, zipo kesi ambazo watu wamechukua sehemu za wenzao, yaani wamejenga na kugandanisha na wala hakuna hata nafasi ya kupita au yule mwenziwe basi ile karo yake amejenga na kuchukua karo ya mwenziwe na huo ni uonevu Mhe. Waziri. Kutokana na hali hiyo, haiwezekani tunakwenda hivyo na wala si vizuri. Kwa hivyo, Mhe. Waziri tuhakikishe kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba ujenzi holela usitishwe kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia nataka nizungumzie kuhusu ujenzi wa Hoteli za Kitalii katika fukwe zetu. Kwa kweli mara nyingi wawekezaji wakija hapa wanapewa taratibu pamoja na sheria zetu vipi wajenge hoteli zao, lakini wanakiuka zile sheria, yaani wanajenga wanaingia mpaka ndani ya bahari.

Sasa mimi nataka kujua kwa sababu suala hili limeshazungumzwa na limeshakemewa sana na hata wanawanyima uhuru wananchi wa kutumia fukwe zao kwa kuona kwamba yale maeneo wameyamiliki. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, atueleze kwamba mpaka hivi sasa hoteli ngapi ambazo zimevunja Sheria ya Ujenzi na hatua gani zitachukuliwa au zimechukuliwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa nataka nizungumzie kuhusu suala la Mipango Miji. Kwa kweli nyuma kidogo tuliharibikiwa kwa sababu tulikuwa tukijenga bila ya mipango na hivi sasa tumeingia katika karne nyengine ya *science* na *technology* tunao watu wengi ambao wamesoma, lakini bado tunakwenda vile vile, yaani ile miji yetu haina mipango na hata ile miji mipya ambayo tunaanza kuizindua

hivi sasa. Kwa hivyo, kila siku wanafunzi wanamaliza Vyuo Vikuu, lakini bado mipango haipo.

Namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, hasa katika hii miji mipya, basi tuhakikishe kwamba hata ile design ya mji tujue nyumba za aina gani zinajengwe kwenye miji ile na wala sio kila baada ya nyumba moja kuna mlango wa duka, hali hii inakera sana. Mhe. Spika, watoto wetu hawapati viwanja vya kuchezea, hakuna bustani, nadhani tutakuja kuwa kama New York tunafanya bustani za juu ya ghorofa na hivyo sivyo, kwa sababu sisi tunayo ardhi ya kutosha.

Vile vile tunasema vijana wetu wanakula unga, kwa sababu hawana shughuli za kufanya kwani michezo ni moja kati ya shughuli ambayo itawafanya vijana wasiingie katika uvutaji wa bangi na unga. Lakini leo sisi tunayoitayarisha hii mipango hatuwatayarishii hivi vitu, hivyo hizi ni athari ambazo zinazotuathiri sisi wakati wa kutayarisha mipango yetu. *(Makofi)*

Namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, alisimamie suala hili, katika miji yetu mipya lazima kuwe na viwanja vya kuchezea watoto, pia sehemu za vijana ambazo watafanya michezo yao pamoja na sehemu za dini. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi sitaki kuzungumzia suala la nishati kwa sababu tayari limeshazungumzwa sana na wataalamu. Kwa hivyo, kitu kimoja nasema kwamba hiki ni kilio na tutafute mbinu ya kulitatua suala hili, kwa sababu ni kilio na mtu mzima akilia analo jambo. Sasa ni vyema kulitafutia mbinu, ili na sisi tuondokane na umasikini, kuomba omba.

Kwa mfano, wenzetu nchi ambazo tayari zimeshachimba mafuta ingawa kuna matatizo na mimi nataka kuwaambia Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Spika, kwamba haya mafuta sio raha tupu na mashaka yamo ndani yake. Mhe. Spika, wenzetu Nigeria wanachimba mafuta na nchi nyengine wanachimba *Diamonds* mpaka wamefika kusema *Blood Diamonds*, kwa sababu watu wanauana kutokana na *diamonds*. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tuchukue hatua za taratibu, mipango mizuri, lakini tuhakikishe mafuta yetu tuyachimbe wenyewe na pia tunafaida na mafuta haya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, la mwisho kabisa nataka kuzungumzia kuhusu suala la maji. Kwa kweli kipindi kirefu sana tumekuwa na matatizo ya maji, yaani suala zito na safari hii serikali imejikita zaidi kwenye wizara hii, ili kuhakikisha wananchi wa Zanzibar wanapata maji na huo ulikuwa ni mpango wa muda mrefu.

Lakini wakati huo huo kuna mipango midogo midogo inafanywa na viongozi mbali mbali kuhakikisha kwamba wananchi wao wanapata maji. Sasa visima vinachimbwa katika maeneo mbali mbali na hasa kwenye maeneo ya mjini. Mhe. Spika nawashukuru sana viongozi ambao wanaofanya jitihada hiyo kwa ajili ya wananchi wao, wanapongeza kwa sababu hivi sasa wananchi wengi wanapata maji kutokana na visima vilivyochimbwa na viongozi wao.

Mhe. Spika, taratibu zinazotumika sizo, kwa sababu visima vinapochimbwa kuna taratibu zake na wengi wao wanasema wakipeleka wizarani hawapati majibu, sasa kama hata hawajapata majibu tayari wameshachimba. Kwa hivyo, naiomba wizara kupitia Mhe. Spika, ichukue juhudi ya makusudi kwanza ya ku-*register* visima vyote vilivyochimbwa Unguja na Pemba ni muhimu kujua. *(Makofi)*

Pili kuhakikisha wanakwenda kuangalia hali ya visima vile, kwa sababu vyengine vimechimbwa sehemu karibu na karo na vyoo na upo uwezekano wa kuripuka maradhi hapa. Kwa maana hiyo, wizara atunaiomba kupitia kwako Mhe. Spika, iwe mlevi wa hivi visima na wala tusiwaachie watu wenyewe, hili ni tatizo. Mhe. Spika, leo kwa sababu hakuna maradhi, lakini yanaweza kuripuka maradhi hapa na baadaye tuje tuilaumu Wizara ya Afya na kusema hawafanyikazi zao vizuri, lakini tatizo limetokea huku. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi sina mengi ya kusema isipokuwa ninalo ombi moja kwa Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, atusaidie wakati wa ziara zetu za kamati tumegundua kwamba wizara yake ina deni katika Idara ya Uchapaji. Kwa hivyo, naiomba tuisaidie Idara hii ya Uchapaji kupitia kwako Mhe. Spika, hivyo Mhe. Waziri limalize suala hili, ili na wenzetu wapate nguvu ya kufanya kazi zao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa niaba ya wanawake wa Unguja na Pemba naomba kuchukua nafasi hii kuunga mkono hotuba ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nilifungua mlango wa *lobbing* na nikaona ninafanywa *lobbing* kubwa sana hapa, kwa sababu wajumbe zaidi ya *list* niliyonayo wanaomba niite mimi. *(Makofi)*

Sasa naomba tumkaribishe Mhe. Ismail Jussa Ladhu na baadaye Mhe. Salim Abdalla Hamad.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia asubuhi ya leo kukutana hapa katika ukumbi huu mtukufu unaofanya maamuzi kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar.

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu huu katika Bajeti ya Wizara hii muhimu ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Spika, kabla sijaendelea na mchango wangu naomba niwaombe radhi sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Mji Mkongwe. Nawaomba radhi kwa sababu najua wanayo mambo yao muhimu na wamenipa niyaeleze hapa yanayohusu maji, nishati hasa umeme, yanayohusu masuala ya majumba yale ya Mji Mkongwe na yale ya Michenzani ambayo mimi ndimo ninamoishi.

Lakini kutokana na umuhimu wa suala la msingi linalohusu maslahi ya Taifa kuliko ya Jimbo la Mji Mkongwe, basi naomba waridhie na ninaamini kwa uelewa wao wataridhia kwamba haya yote kwa leo niyawache na nizungumzie suala moja tu linalohusu haki ya Zanzibar katika suala la mafuta. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kusema kwamba nautanguliza mchango wangu huu kwa kufanya marejeo katika Katiba ya Zanzibar nikitambua wajibu wangu kama Mzanzibari, lakini zaidi niliaminiwa na Wazanzibari wenzangu wa Jimbo la Mji Mkongwe kuwasemea katika Baraza hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Katiba ya Zanzibar ibara ya 23 baada ya kuelezea haki ambazo Wazanzibari wanazopaswa kuzipata, imeelezea wajibu ambao Wazanzibari tunao. Naomba kunukuu Mhe. Spika.

Kifungu cha 23 (2) na (3) vya Katiba ya Zanzibar vinasema hivi:-

"(2) Kila mtu anao wajibu wa kulinda maliasili ya Zanzibar, mali ya nchi na mali yote inayomilikiwa kwa pamoja na wananchi na pia kuheshimu mali ya mtu mwengine.

(3) Watu wote watatakiwa na sheria kulinda vizuri mali ya Zanzibar na kwa pamoja kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhirifu na kuendesha uchumi wa Zanzibar kwa makini kama watu ambao ni waamuzi wa hali ya baadaye ya taifa lao." *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimeona nianze na vifungu hivi kwa sababu kama nilivyosema nataka kuwakumbusha wenzangu na wananchi wote wanaotusikiliza kama Wazanzibari tunao wajibu wa Kikatiba, lakini pia tunao wajibu kama viumbe tulioumbwa na Mwenyezi Mungu kulinda kile ambacho amekijaalia kuwa ni mali yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sikusudii kulirejesha nyuma Baraza lako, kwa sababu nimesoma Kanuni za Baraza hili vizuri sana nilipoingia, kwamba haturuhusiwi Wajumbe kuzungumza au kutoa hoja ya jambo ambalo tayari limeshaamuliwa na Baraza lako.

Kwa kweli nafurahi kuwa Baraza hili Mhe. Spika, katika kikao chake cha mwezi wa April mwaka 2009 lilishafanya maamuzi ya kuliondoa suala la mafuta na gesi asilia katika mambo ya Muungano. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nirejee Hansard ya tarehe 8/04/2009 wakati huo aliyekuwa Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi ndugu yangu Mhe. Mansoor Yussuf Himid alipoliongoza Baraza lako kufanya maamuzi ya kihistoria na ya kijasiri yatakayokumbukwa maisha katika historia ya Zanzibar. Kwa hivyo, kutokana na uchache wa muda naomba moja kwa moja niende katika masuala ya maamuzi, ambayo Mhe. Spika ulibahatika kuingia kwenye historia ya kuwahoji wajumbe, naomba ninukuu.

"Pendekezo la Kwanza:

Hoja imetolewa, sasa Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na pendekezo la kwanza kuhusu Ardhi ya Bahari na ndani ya Zanzibar kwamba suala la mafuta liwe katika mikono ya Zanzibar wainue mikono.

Naona Waheshimiwa Wajumbe wote wanaunga mkono pendekezo hili. Waliokataa hakuna. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Pendekezo la Pili:

Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwahoji wale wanaokubali pendekezo la kuishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba sasa wakati umefika kuunda chombo chake cha Kusimamia Utafutaji na Uchimbaji wa Mfuta na Gesi, wanyanyue mikono.

Mhe. Spika, ukasema naona Waheshimiwa Wajumbe wote waliokuwepo wanakubali. Waliokataa hakuna. *(Makofi)*

Pendekezo la Tatu:

Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwahoji wale wanaokubaliana na pendekezo la *EEZ*, yaani *Exclusive Economic Zone* sehemu ya Bahari Kuu, serikali inashauri kwamba Wajumbe wakubali kuwa suala hili liende kwa mashirikiano ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wale wanaokubali pendekezo hilo wanyanyue mikono.

Wanaokubali pendekezo hilo wanyanyue mikono.

Wanaokataa pendekezo hilo, inaonekana kimya.

Mhe. Spika, ulisema kwa hivyo pendekezo hili lisahihishwe na inaonekana kufuatana na michango ya Waheshimiwa Wajumbe kwamba eneo hili pia liwe katika mikono ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. kwa hivyo, ni sawa hicho tunachokubali

Wajumbe: Sawa. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Wanyanyue mikono Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubali, wale wanaokataa.

Mhe. Spika: Kwa hivyo, pendekezo la eneo la Bahari Kuu inaonekana Waheshimiwa Wajumbe wote wamenyanyua mikono.

Katika suala zima la utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi liwe katika mikono ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Haya ndio mapendekezo ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar yaliyopitishwa leo hii tarehe 08/04/2009 saa 7:00 mchana.

Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni." *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimeona nitumie muda wangu huu mchache kwa ajili ya kuyasoma haya, kwa sababu ni muhimu sana. Kwa kweli kama nilivyosema hapa suala hatujadili tena kuwa tuliondoe au tusiliondoe suala la mafuta katika mambo ya Muungano. Hili tayari limeshaamuliwa. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Spika, niseme kwamba kazi hii iliongozwa kama nilivyosema na ndugu yangu Mhe. Mansoor Yussuf Himid. Kwa hivyo, nilipoona sasa wizara hii anayo kaka yangu ambaye ninamuheshimu sana na yeye anajua hivi na kwa kutambua ujasiri wake, basi nilitegemea Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati Mhe. Ali Juma Shamuhuna katika kikao hiki angetuletea sasa mapendekezo ya hatua ya kutekeleza maamuzi haya za Baraza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimevunjika moyo sana kwa sababu nimemsikiliza vizuri sana Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati katika hotuba yake kwenye ukusara wa 61 hadi 62 amelizungumzia suala la mafuta na kwa kuokoa muda sitaki kulirejea kwa sababu sote tumesikia wakati aliposoma.

Lakini Mhe. Spika, nasikitika kusema humu hamna kitu, isipokuwa haya ni yale maelezo ya jumla ambayo tunaendelea kupewa kila siku. Mhe. Spika, sisi

tunazungumza na Wazanzibari, hivyo Wazanzibari wanatwambia wamechoka kusikia maneno kama haya na wanataka vitendo. *(Makofi)*

Kwa kweli kama nilivyosema Baraza lako tukufu Mhe. Spika, tayari limeshafanya maamuzi kuhusu suala hili na maamuzi ilikuwa ni kuliondoa. Lakini kwa kuwa Zanzibar watu wake ni wastaarabu, yaani wanayo historia refu ya ustaarabu ya karne zaidi ya 20, tokea miaka 2500 iliyopita Zanzibar imeingia katika historia kupitia kitabu cha *The peripuls of the Erytherean Sea*.

Wakati huo, wananchi wa Zanzibar walikuwa wakivaa nguo tena za hariri kwa mujibu wa kitabu hicho. Kwa maana hiyo, tulifanya uungwana. Mhe. Spika, lakini inaonekana huu ungwana ndio unaotuponza sasa na mara nyengine huu uungwana ukizidi basi huwa unamdhuru yule muungwana.

Mhe. Spika, nilikuwa nikipitia hotuba ya mwaka jana ya Mhe. Mansoor Yussuf Himid wakati alipokuwa Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Kwa kweli alisema mengi, lakini ya kutokana na muda Mhe. Spika, naomba nisiyaseme yote, isipokuwa nataka nikisome kifungu kimoja ambacho kiko kwenye ukurasa wa 34 wa hotuba hiyo.

Ukurasa wa 34 kifungu cha 62 kinasema hivi:-

> "Mhe. Spika, kwa upande wa suala lenyewe la mafuta na gesi asilia hatua iliyofikiwa baada ya maamuzi ya serikali ya kupendekeza kulitoa suala la mafuta na gesi asilia katika Orodha ya Mambo ya Muungano, Baraza la Mapinduzi lilimuagiza Mhe. Waziri Kiongozi kuwasilisha barua maalum kwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kulitoa suala hilo katika Orodha ya Mambo ya Muungano, ili kuzipa nafasi hatua nyengine za Kisiasa na Kisheria kuchukua mkondo wake.
>
> Mhe. Spika, naomba kusisitiza ili kuzipa nafasi hatua nyengine za Kisiasa na Kisheria kuchukua mkondo wake. Kwa hivyo, Mhe. Waziri Kiongozi tayari amelichukulia hatua suala hilo na barua hiyo tayari imeshawasilishwa na wizara yangu inasubiri maelekezo ya Afisi ya Mhe. Waziri Kiongozi."

Sasa Mhe. Spika, nilitegemea baada ya hotuba hii ya mwaka jana, basi tungeelezwa baada ya barua hii iliyoandikwa na Waziri Kiongozi kwa Waziri Mkuu kupeleka maamuzi ya Baraza hili nini kimefuata Baraza ambalo Kikatiba hili ndilo lenye mamlaka ya kuwaamulia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, Katiba ya Zanzibar inasema wananchi wa Zanzibar watashiriki katika uendeshaji wa nchi yao ama moja kwa moja na hivi sasa tunashukuru tunao Mfumo wa Kura ya Maoni au kupitia Wawakilishi wao waliochaguliwa na wananchi ambao ndio Baraza hili Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa tumeamua na tumepeleka kwa uungwana, lakini inaonekana kuna tatizo, kwa sababu wenzetu ule uungwana wetu sasa wanaupeleka mbali sana Mhe. Spika.

Pamoja na hayo, naomba niseme kabisa kwamba mimi nitaizuia bajeti ya wizara hii isipitishwe mpaka Mhe. Waziri atupe kauli, si kauli ya maneno tena Mhe. Spika, kama iliomo kwenye hotuba hii hatuikubali hata siku moja, hatuikubali. Kwa hivyo, atupe kauli lini Zanzibar angalau kwa kuanzia itaunda chombo chake hiki kilichotajwa *Zanzibar Petroleum Development Authority*, yaani Mamlaka ya Uendelezaji, Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta Zanzibar. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu, sasa mbali ya kupitisha maazimio yale Baraza lako hili tukufu Mhe. Spika, lilipata nafasi ya aina yake kuletewa Sera ya Nishati Zanzibar. Kwa kuwa masuala ya Sera Kikatiba ni masuala ya Baraza la Mapinduzi, lakini kwa uungwana wa Mhe. Mansoor Yussuf Himid aliileta Sera hii katika Baraza hili, ili ipate baraka za Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, Sera hii kwenye Tafsiri ya Kiswahili katika ukurasa wa 28 naomba kunukuu.

> Tafsiri ya Sera kwa Kiswahili ukusara wa 28 hoja ya tisa ya sera inasema hivi:-
>
> “Hoja ya 9 ya Sera: Utafutaji wa Kiwango cha kutosha cha Hifadhi ya Mafuta na Gesi Asilia.
>
> Tamko:
>
> Zanzibar itaanzisha mazingira yake ya kisheria na usimamizi kwa ajili ya uchunguzi zaidi na utafutaji na itahakikisha udhibiti wote wa hifadhi ya mafuta katika maeneo yake yakiwemo maeneo maalum ya Kiuchumi, yaani ile *Exclusive Economic Zone*.
>
> Pili Zanzibar itaimarisha na kusimamia ugunduzi kwa juhudi zote, uzalishaji na kusambaza gesi na bidhaa za mafuta. Ugunduzi na uzalishaji huo utatilia maanani hali za kimazingira, kijamii na kiuchumi.

Tatu Mhe. Spika, Zanzibar itahakikisha ukusanyaji wa mapato na mgao wa uwiano kwa taifa na kuyatumia, ili kuleta faida kwa wananchi wake.

Nne ni muhimu sana Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi la Zanzibar litathibitisha mfumo wa mikataba yote ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia."

Sasa Mhe. Spika, sera ni ya serikali lakini imeridhiwa na Baraza, yaani imepata nguvu ya kuungwa mkono na wananchi moja kwa moja kupitia Wawakilishi wao. Kwa hivyo, tunasita nini Mhe. Spika au tunaogopa nini? Ama ndio vile tunavyoambiwa kwamba Muungano huu ni ndoa, hivyo leo nataka nisaidiwe na Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, katika ndoa hii nani mume na yupi mke? *(Makofi)*

Mhe. Spika, Zanzibar tumeolewa? Naomba tuambiwe, kwa sababu Zanzibar tunashindwa kufanya maamuzi mpaka mume atake, hayo ndio majibu ya wenzetu wakati mwengine kwamba huu Muungano wetu ni ndoa, sasa mukiwa na ndoa mnapoteza baadhi ya uhuru wenu, hivi sisi tumeolewa katika Muungano huu? *(Kicheko/Makofi)*

Kwa kweli tulipolichangia suala hili katika Hotuba ya Bajeti, tuliambiwa na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo wakati alipokuwa akifanya majumuisho alituuliza je tuchimbe kwa sababu sheria iliyokuwepo ni ya Muungano.

Mhe. Spika, mimi nataka nitafautiane na wenzangu niseme sasa nataka nimsaidie Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ambaye ni kaka yangu, basi tufanye maamuzi na wala tusipige makelele tukaonekana labda tumepoteza fahamu.

Mhe. Spika, Zanzibar inayo Sheria ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta. Mhe. Spika, mwaka 1951 palipitishwa sheria kadhaa kuna *Chapter* ya 106 katika Sheria za Zanzibar ambayo inazungumzia *Mining, (Mineral Oil) Principal Legislation*, halafu kuna *Chapter* 107 *Mineral Oil (Principal and Legistlation)*, pia kuna *Chapter* 108 *Mining (Mineral Oil) (Subsidiary Legislation)* na hii *Subsidiary Legislation* ndio imeweka utaratibu mzima wa namna ya kutafuta, mambo ya *license* na kila kitu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda nasikitika sana na nilikuomba uniongeze, lakini nimeheshimu maamuzi yako. Katika hii *Chapter* ya 107 Sheria au *Decree* iliyopitishwa tarehe 29 Disemba, 1951 na imo katika Vitabu vya Sheria vya Zanzibar Mhe. Spika, kifungu kidogo cha 3 naomba kunukuu Mhe. Spika.

Chapter ya 107 Sheria au *Decree* kifungu kidogo cha 3 kinaeleza hivi:-

> "*In order to remove doubts it is hereby declared that notwithstanding anything to the contrary in any other law contained, the property in all mineral oil existing in its in natural condition in strata in the Protectorate (including the soil and subsoil underlying the territorial waters thereof) is and shall be deemed always to have been, vested in the Government of His Highness the Sultan of Zanzibar and that any grant of mineral rights contained in any conveyance, grant, lease or licence from the Government of His Highness the Sultan of Zanzibar shall be deemed not to include mineral oil unless mineral oil is expressly mentioned as being included therein."*

Mhe. Spika, tumewapindua tukawaondosha Masultani lakini angalau walikuwa na ujasiri wa kulinda rasilimali za Zanzibar kwamba hata ingekuwa mtu anamiliki ardhi basi kama mna mafuta si yake ni ya nchi, hata katika bahari kuu. Sasa leo Mhe. Spika, tuna Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweka *record* katika mambo mengi sana tunashindwa kuisimamia ile utadhani hatuna sheria. Nataka niseme kitu kimoja Mhe. Spika, isije ikaeleweka vibaya kwamba sheria hizi zilikuwa za zama za mkoloni kwamba hazitumiki Zanzibar. Baraza la Mapinduzi lilikuwa na watu waliokuwa na akili zao.

Mhe. Spika, naomba ninukuu kidogo tu, hiki ni kitabu cha Profesa Issa Shivji aliyefanya utafiti kuhusu suala la Muungano vizuri sana. Mhe. Spika, katika ukurasa wa 58 wa kitabu hiki alipozungumzia mabadiliko yaliyotokea mwaka 1964 alisema kwamba Baraza la Mapinduzi lilitoa *notice* ya kuifuta Katiba ya Zanzibar ya 1963 ya uhuru. Lakini naomba ninukuu kidogo hapa.

> *"Another announcement dated 27th January, 1964 declared that the existing laws except the overthrown constitution would continue to apply."*

Yaani sheria nyengine zote zilizokuwepo ukiondoa Katiba iliyopinduliwa, Baraza la Mapinduzi liliamua zitaendelea kutumika. Haya ni maamuzi ya Baraza la Mapinduzi. Hii Mhe. Spika, imo katika *general notice* namba 91 ya tarehe 1 Februari, 1964, yamo katika gazeti rasmi la serikali haya Mhe. Spika.

Lakini kusisitiza zaidi hata huo mkataba wa Muungano ambao leo watu wanataka kuutumia kutunyongea roho katika kifungu cha 5 ulisema:

"The existing laws of Tanganyika and of Zanzibar shall remain in force in their respective territories."

Yaani sheria zilizopo za Zanzibar na Tanganyika zitaendelea kuwa na nguvu katika maeneo ya mipaka yake. Kwa hiyo Mhe. Spika, ninachotaka kusema kwamba Sheria ya Mafuta Zanzibar ipo na kuthibitisha hilo ni kwamba hata wanasheria wetu wanaitambua uhalali wake.

Mhe. Spika, hapa kidogo ndipo ninaposikitishwa kwamba serikali yetu inaonekana baada ya maamuzi ya Baraza la Wawakilishi ilishaanza kuchukua hatua. Mhe. Spika, ninayo hapa *"Zanzibar Petroleum (Exploration and Production) Bill 2009".* Hii ilikuwa ni rasimu ya sheria ilikwishatayarishwa ya tarehe 2 Agosti, 2009. Ilikuwaje tena Wizara hii ikaikalia rasimu hii, kumepita nini, tunatishwa na nani Mhe. Spika, sisi ni nchi huru. Kwa sababu ya kuzitambua hizi sheria ninazozisoma Mhe. Spika, ukisoma huku mwisho rasimu hii ilikuwa inazifuta na kuzirekebisha zile sheria za mwaka 1951. Kwa kitendo hichi cha kuziingiza katika rasimu, ni kwamba ilikuwa inazitambua sheria hizi zilikuwa bado ni halali Zanzibar ndio maana inakuja sheria mpya inataka kuzirekebisha ama kuzifuta zilizokuwepo zamani.

Sasa Mhe. Spika, tulifika hatua mpaka hii. Leo Zanzibar tumefanya Mapinduzi tunatishwa, tunazuiliwa. Mhe. Spika, leo anakuja Mhe. Samwel Sitta ndani ya Bunge anatukebehi na kutukejeli Wazanzibari. Tumeshapeleka barua hii ya maamuzi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, yeye anasema katika Bunge bado anatetea hoja ya mafuta kubakia katika Muungano, kama vile Serikali ya Muungano haina taarifa yoyote juu ya suala hili na huyu ni Mjumbe wa Baraza la Mawaziri wa Serikali ya Muungano.

Mhe. Spika, nachelea kusema, lakini Mhe. Samwel Sitta ni kigeugeu. Tulimwona alipokuja Bwawani pale alitoa kauli baada ya kutuonesha Wazanzibari kama vile katufahamu sana, lakini juzi karudi Bungeni anarejea kama vile hakusikia chochote cha Wazanzibari. Hivi ndivyo wenzetu walivyo Mhe. Spika. Kwa sababu ya hisia kama hizi ndipo Wazanzibari wanaposema watafika pahala watasema Muungano huu basi, wenzetu hawana nia njema na sisi. Sasa Mhe. Spika, mimi sitaki tufike huko lakini ninachosema kwamba kama tumefika hatua hizi hatuna sababu sasa ya kuendelea kusita sita.

Mhe. Spika, juzi Mhe. Samwel Sitta anasema kwamba mafuta yapo katika mpaka baina ya mkondo wa Tanga na Pemba kwa hivyo hata tukitengana kutakuwa na ugomvi. Kamwambia nani Mhe. Spika?

Mimi hapa ninayo ramani ya *licence* zilizotolewa kwa makampuni ya mafuta. Hii ni *block* ya Zanzibar na Pemba ya *on shore* ndani ya visiwa na *immediate off shore,* haipo baina ya mpaka wa Tanga na Pemba. Lakini pia ramani ya pili Mhe. Spika, ni hii hapa, hii ni ramani inayoonesha zile *block* katika bahari kuu. *Block* ya kwanza ile kuanzia Mtwara huku mpaka *block* ya 12 inayomalizikia

juu ya kisiwa cha Pemba karibu na mpaka na Kenya. Hizi *block* zote ziko upande wa mashariki wa visiwa, hakuna mpaka huku, mpaka Indonesia. Sasa unapotuambia sisi tutazozana unadanganya ndani ya Bunge kuwatisha watu na kuwapotosha katika suala hili. Mimi kwa sababu ya uungwana wa Wazanzibari tutafika pahala huu uungwana tutauweka kando, kama uungwana ndio silaha inayotumika kutumaliza tutaukataa.

Mhe. Spika, tumefika pahala sasa nimeyasema haya na nimekuja na makaratasi mengi hapa kwa sababu nataka Wajumbe wa Baraza lako wanielewe na Wazanzibari wanaotusikiliza watuelewe. Mhe. Spika, Mhe. Hassan Nassor Moyo Mwenyezi Mungu ampe umri mrefu atusaidie katika masuala haya. Yeye ni mmoja katika waasisi wa Muungano na muasisi wa Mapinduzi alisema pale Bwawani "Wazanzibari wa leo hawa wamesoma hawakubali tena kuburuzwa kama ilivyokuwa zama zetu."

Mhe. Spika, ni kweli sisi kuburuzwa hatutakubali. Mhe. Spika, leo teknolojia ya mafuta imekua, tunalia hapa tunazozana tunakwamisha bajeti kuhusu *ICU*, mambo madogo madogo ya milioni 800, pesa tunazo nilimwambia Mhe. Omar Yussuf Mzee uchumi tunao tumeukalia.

Mhe. Spika, hii ni makala iliyotoka ndani ya gazeti la *Economist* jarida maarufu duniani la tarehe 6 Machi, 2010. Linaelezea kukua kwa teknolojia ya kisasa katika uchimbaji wa mafuta hasa katika bahari kuu kwamba haihitaji miaka mingi kama ilivyokuwa zamani wala kujua uhakika wa kuwepo kwa mafuta. Mhe. Spika, kampuni kubwa kama ya Shell ambayo ni kampuni ya pili kwa ukubwa duniani na ndio yenye ku-*hold licence* katika *block* kuanzia 9 kwenda 12 haiwezekani ikang'ang'ania isipokuwa inajua kwamba mafuta Zanzibar yapo tena ya kutosha kwa teknolojia hii ya kisasa. Sasa Mhe. Spika, nasema tusiendelee kuchezewa, tufanye maamuzi.

Mhe. Spika, naomba nimalizie tokea mwanzo nimewaomba radhi sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Mji Mkongwe yako mengi ya kuwatetea lakini hili linahusu maslahi ya nchi si maslahi ya Jimbo la Mji Mkongwe. Hata haya masuala ya majumba mabovu ya Mji Mkongwe yakitaka kutengenezwa, masuala ya maji kupatikana, yote tukichimba mafuta hapa yatakwisha masuala haya. Hasa kwa sababu tumekuja na mfumo mzuri katika sera yetu kwamba tunafanya mambo kwa uwazi kwa kidemokrasi kwamba hata mikataba yote itakayotiwa saini katika utafutaji, uchimbaji lazima iletwe mbele ya Baraza lako la Wawakilishi iidhinishwe na wawakilishi na wananchi wako turidhike.

Kwa hivyo, tuna hakika yale matatizo yaliyowakuta wenzetu sisi hayatatukuta. Kwa sababu wawakilishi wa wananchi tutalinda maslahi ya Zanzibar. Sasa Mhe. Spika, nilisema tuliambiwa na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alipokuwa

anafunga bajeti yake kwamba suala hili halimo, kama walivyokuwa wakisema wajumbe katika orodha ya kero za Muungano, litamalizwa na viongozi wa juu.

Lakini nasikitika Mhe. Spika, katika jibu la Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Mhe. Mohammed Aboud Mohammed katika maswali kikao hiki hiki siku moja alipokuwa anatuorodheshea kero za Muungano zilizobakia hazijamalizwa alisema mambo hayo ni kuhusu ushiriki wa Zanzibar katika Jumuia ya Afrika Mashariki na la pili utafiti na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia.

Kalipeleka nani hili katika kero Mhe. Spika? Siku ile sikutaka kusema tu lakini palikuwa na mgongano dhahiri baina ya Makamo wa Pili wa Rais na kauli ya Waziri wake wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alituambia halimo katika makero ya Muungano linajadiliwa na viongozi wa juu, Waziri wake anatuambia limo katika kero za Muungano halijamalizwa. Hili hapa jibu lake.

Sasa Mhe. Spika, nasema tumechoka na kauli kama hizi. Nimesema katika suala hili na sitokuwa na sumile kabisa nitazuia shilingi mpaka Mhe. Waziri aje atwambie. Suala la lini tutaanza kuchimba mafuta siwezi kumsukuma huko kwa sababu najua kuna taratibu zake, lakini hili katika azimio la kuleta sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Utafutaji na Uchimbaji Mafuta Zanzibar, *Zanzibar Petroleum Development Authority,* lazima aje anijibu hapa ndani ya mwaka huu wa fedha ikiwezekana kikao cha Oktoba tuletewe sheria ya kuanzishwa mamlaka haya.

Hawa waliopewa *licence* ikiwa ni *Antrim Energy,* ikiwa ni *RAK Gas,* ikiwa *SHELL* waje waombe tena leseni zao kwa mamlaka ya Zanzibar yenye mamlaka ndani ya Zanzibar.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kusema wajibu wa kulinda rasilimali za Zanzibar katika Katiba hii ni wajibu wetu Wazanzibari kama raia na pia kama ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Tuna wajibu wa kimsingi mbali ya wajibu kama binadamu kuuheshimu utu kwamba Mwenyezi Mungu katujaalia kulinda rasilimali yetu.

Mhe. Spika, nimesema kanuni haziruhusu kurejea maamuzi, maamuzi tulishayafanya, tufike pahala sasa tu-*act.*

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo siungi mkono hoja mpaka nijibiwe suala langu. Ahsante sana.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Spika, kwanza naomba kuchangia mambo mawili kwa pamoja kuhusu maji vijijini na umeme vijijini nikihusisha hali ya jimbo langu ilivyo moja kwa moja. Mhe. Spika, katika Jimbo langu la Mtambwe ambalo ni jimbo lenye jiografia ngumu kabisa na baada ya kuona katika kitabu hiki kwa umeme vijijini Mhe. Waziri kaeleza kuwa vijiji vyote vitapatiwa umeme katika mwaka huu wa fedha kama ilivyoelezwa katika ukurasa wa 59 na 60 kifungu cha 107. Kwa habari ya maji ameeleza katika ukurasa wa 52 kifungu cha 92 pamoja na ukurasa wa 88 katika kiambatanisho (i).

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 52 Mhe. Waziri kaeleza katika kitabu chake kuhusu usambazaji wa maji vijijini kuwa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China imekubali kuchangia jumla ya dola za Kimarekani milioni 1.5 kwa kazi za uchimbaji wa visima zaidi ya 30 pamoja na ujenzi wa matangi, utiaji pampu na ulazaji wa mabomba ya inchi sita na inchi nne katika maeneo 24 ya Unguja na Pemba. Kwa maelezo zaidi katutaka tuangalie kiambatanisho hicho kilichopo katika ukurasa wa 88 vijiji 24 vipo lakini kwa Jimbo la Mtambwe kaeleza kuwa maji haya yatapelekwa Mtambwe Kaskazini pamoja na kijiji cha Kisiwani tu.

Mhe. Spika, katika Jimbo la Mtambwe kuna vijiji havipungui 13 havina umeme na yeye kachukua vijiji vilivyopo katika Mtambwe Kaskazini tu ikiwa ni moja kati ya shehia 5 ziliomo katika jimbo langu. Hivi vijiji vyengine vilivyobakia vyote ina maana vitabakia hivi hivi mpaka awamu yake imalizike. Mhe. Spika, ushauri wangu namuomba Mhe. Waziri kwa makusudi kabisa atembelee katika jimbo langu nimuoneshe vijiji ambavyo havina huduma hii ya umeme avione na hali ilivyo na kushuhudia juhudi yangu niliyoifanya katika shirika lilioko Pemba ili ajue vya kuamua vyengine. Lakini kwa kupeleka Mtambwe Kaskazini tu hili litakuwa ni suala ambalo siwezi kuliunga mkono.

Mhe. Spika, kwa upande wa maji kuna vijiji 11 havina maji bado na vijiji vilivyopo Mtambwe Kaskazini ambavyo mwenyewe anasema kuwa atapeleka maji ni vijiji vinne tu. Sasa hivi vyengine vilivyobakia saba ndio vibakie hivi mpaka lini. Kwa hivyo, naiomba serikali iunge mkono juhudi zangu tunavyoshirikiana katika kuwapelekea watu huduma hii, hivyo kwa makusudi wanisaidie kumaliza sehemu iliyobakia kuliko kuchukua sehemu ndogo na kuwaachia sehemu kubwa bila ya huduma husika.

Mhe. Spika, la pili ni kuhusu Idara ya Nishati na Madini lakini napongeza kazi kubwa iliyofanywa na Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Kwa hivyo, sina tena namna ya kuongeza zaidi ya hapo. Lakini Mhe. Spika, ili kwa kulipa taarifa Baraza zaidi na kuweza kufahamu huko tunakotoka na tulipo kwa ruhusa naomba uniruhusu kwa haraka haraka kusoma hii taarifa tuliyonayo inayohusiana kabisa na uchimbaji wa mafuta Tanzania Bara.

Mhe. Spika, taarifa hii imeandikwa tarehe 7 Julai, 2011 saa 2:25 za usiku na inaeleza kama nitakavyoisoma. Mhe. Spika, taarifa inaeleza hivi: "Waziri Mkuu Mhe. Mizengo Pinda, amesema Serikali ya Tanzania haitaingia gharama zozote wakati meli ya Poisedon itakapokuwa inafanya uchunguzi wa mafuta na gesi katika pwani ya Tanzania.

Kwa mujibu wa taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Pinda alitoa kauli hiyo jana baada ya kutembelea eneo la viwanda vya kujenga meli ili kuona hatua mbali mbali za ujenzi wa meli na kuikagua meli ya uchimbaji mafuta."

Kwa kuendelea Mhe. Spika, taarifa inaeleza kuwa "Meli hiyo ya Poisedon inajengwa katika Bandari ya Geoje, Kusini Mashariki mwa Seoul, Korea Kusini.

Waziri Mkuu anatarajiwa kuzindua meli hiyo leo saa 4:00 asubuhi katika Bandari ya Geoje.

Alisema wanachofanya sasa wataalam kutoka Kampuni ya *Petrobas* ya Brazil ni kutafiti na kubainisha maeneo mawili ambako meli hiyo itachimba endapo matokeo yatakuwa mazuri.

Tunaishukuru Serikali ya Brazil kwa kuamua kusaidia Serikali ya Tanzania kufanya utafiti huo muhimu," alisema Waziri Mkuu.

Taarifa ikiendelea inasema hivi: "Alisema hatua hiyo ni dalili njema kuwa uwekezaji unawezekana kufanyika Tanzania na kuahidi kuwa Serikali ya Tanzania itafanya kila iwezalo kuweka ulinzi wakati wataalam hao wakiwa kazini ili kuzuia hatua ya kupambana na maharamia.

Mapema, akitoa taarifa kwa Waziri Mkuu kuhusu ujenzi wa meli hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya *Petrobas* Tanzania, Samwel Miranda, alisema wanatarajia kwamba meli hiyo itafanya kazi katika ukanda wa pwani kwa muda wa miezi 20 katika maeneo ya kati ya Mafia na Mtwara.

Kuhusu utoaji ajira kwa Watanzania, alisema wameanza kutoa mafunzo kwa vijana 50 wa kike na wa kiume wa kutoka Mtwara ambao wakifaulu watafanya kazi katika meli hiyo."

Anasema “Meli hii itakuwa Mtwara na tunatarajia kuanza kazi mwanzoni mwa Septemba. Tumeanza na vijana 50 kuanzia Julai mosi, watapewa mafunzo maalum ya miezi mitatu ya umeme, umakenika na masuala ya uchimbaji mafuta na si kitu kingine.” Alifafanua.

“Mafunzo haya yanaendeshwa kwa ubia baina ya *TPDC, VETA, Petrobas* na Taasisi ya *Cenal* ya Brazil ambayo inafanana na *VETA* ya hapa Tanzania. Nia yetu ni kupata wakufunzi ambao wataendelea kufundisha vijana wengi zaidi katika fani hii,” alisema.

“Mbali na hatua hiyo, Miranda alisema wana mkataba na wahandisi wanne wa Kitanzania ambao tayari wamepelekwa Brazil kwa mafunzo ya muda mfupi na kisha watapelekwa Uingereza ili kujifunza zaidi masuala ya uchimbaji mafuta.

Meneja Mradi wa Kampuni ya *Ocean Rig* ya Uingereza inayosimamia ujenzi wa meli hiyo David Gray, alimueleza Waziri Mkuu kwamba meli hiyo yenye urefu wa mita 242 na upana wa mita 52 imegharimu dola za Kimarekani milioni 800.” Namaliza kunukuu.

Sasa Mhe. Spika, hii ndio hatua wenzetu tunaokwenda nao na ambao kila siku tunaambiwa tutajitahidi mafuta kuyatoa katika Muungano hatua waliyofikia. Hili suala linaamuliwa katika Baraza la Wawakilishi na hakuna chombo zaidi cha uamuzi kwa fani hii isipokuwa ni Baraza la Wawakilishi. Nimesoma Katiba, nimesoma kila mahala, sijaona mahala popote isipokuwa Mhe. Rais kuwa kuna mtu yeyote mwengine anayeweza akatoa mawazo mengine zaidi au maamuzi ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, sisi tumeshaamua kuwa mafuta ni ya Wazanzibari na sasa mimi binafsi nishahofia, nahofia hata wale waliokuwa wakisema si ya Muungano. Lakini ikiwa matayarisho ni haya mafuta yatachimbwa kwa ulinzi mkubwa wa majeshi hivyo sisi tutafika wapi.

Kwa hivyo, ushauri wangu pamoja na kuwa Wazanzibari ni watu wakarimu na mara zote tunakwenda katika mambo yetu kiutaalam tuone kuwa Muungano tunauimarisha lakini kwa maslahi yetu, pale ambapo tumeshashindwa tusiogope kusema kweli. Mhe. Spika, mimi sioni dalili kuwa wale Waheshimiwa Wajumbe wanaopelekwa kule kufanya kikao na wenzetu wa huko Tanzania Bara kuhusu suala hili kuwa wana uwezo wa kuona kuwa tumefanikiwa. Kwa sababu sisi tunaambiwa kuwa yatatolewa na msimamo uko pale pale lakini wenzetu wameshafanya matayarisho mpaka kununua meli inayogharimu dola za Kimarekani milioni 800.

Halafu nahofia sana Mhe. Spika, hii Katiba ya Jamhuri ya Muungano, hii Katiba ndio inayotumika na bado haijafanyiwa mabadiliko. Ukitazama kifungu cha mwanzo ambacho wanakitumia wao na nitakitolea maelezo wanasema kuwa Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano. Hii ilikwenda katika hali ngumu sana na sisi tukapiga makelele mpaka nikapiga kura ya maoni tukabadilisha Katiba, baada ya kubadilisha ndio *Alhamdulillah* baada ya zogo wametulia. Kwa nini kwa suala kama hili la mafuta tusiweze kulifanyia kura ya maoni haraka na tukaliingiza katika sehemu ya Katiba ya Zanzibar ambayo haliwezi kubadilishwa isipokuwa ni kwa kura ya maoni.

Vyenginevyo Mhe. Spika, mafuta yatachimbwa na yataambiwa si ya Muungano na kwa matayarisho sisi hatujafika walikofika wenzetu itakuwa ni hasara bure. Hata ule uwezo wa kulinda mazingira katika uchimbaji huu wa mafuta itakuwa hakuna.

Mhe. Spika, kifungu cha pili wameeleza eneo la Jamhuri ya Muungano kuwa ni eneo lote la Tanzania Bara na eneo lote la Tanzania Zanzibar na pia ni pamoja na sehemu yake ambayo Tanzania inapakana nayo. Kwa hivyo, wakitumia Katiba hii tumekwisha. Mhe. Spika, bila ya mafuta sioni kuwa Zanzibar itaweza kujitegemea kiuchumi na kuendelea.

Kwa hivyo, ushauri wangu Mhe. Spika, kwa suala la mafuta Baraza la Wawakilishi lilivyoamua ndio vile vile na nafikiri hapana haja tena kwenda kutafuta uwiano mwema wa kukubaliana, mahala ni pabaya wenzetu wanaendelea wakati sisi tunaendelea na mazungumzo hatuna matayarisho yoyote. Tutafute namna ambayo kwa yale mafuta yaliyomo katika kanda ya Zanzibar kama Mhe. Ismail Jussa Ladhu alivyoeleza tuweze kuyakabidhi katika hali yetu wenyewe. Hivi tutafanya tunao waheshimiwa wanasheria wengi humu, lakini mimi niliyekuwa si mwanasheria nasema utaratibu ufanywe, Mhe. Rais atangaze kura ya maoni kuhusu mafuta na halafu turekebishe Katiba hivyo watakavyoona kuwa mafuta yetu hayatoingiliwa.

Mhe. Spika, jengine kuna nishati mbadala. Ukiangalia ukurasa wa 57 kitabu kimeeleza kuwa Shirika la Umeme limeweza kuchukua hatua mbali mbali ikiwemo ya kufanya mazungumzo na taasisi tofauti ambazo zimeonesha nia ya kutaka kuwekeza katika uzalishaji umeme kwa kutumia njia zifuatazo. Yaani nishati ya upepo, nishati ya jua na nishati ya gesi asilia. Kwa taarifa imemaliza kuwa aidha Wizara pamoja na Shirika la Umeme tunaendelea na jitihada ya kuitafutia kampuni ya *SBE* ya Israel ambayo imeonesha nia ya kutaka kuwekeza katika uzalishaji wa umeme kwa njia ya mawimbi ya baharini.

Mhe. Spika, umeme binafsi tukitaka tusitake wakati umeshafika lazima Zanzibar tujitegemee kwa umeme, haya mambo ya umeme tegemezi unahatarisha maisha yetu.

Lakini kitabu kinasema kuwa walichukua hatua mbali mbali likiwemo kufanya mazungumzo na taasisi tofauti. Namuomba Mhe. Waziri atufafanulie ni taasisi gani kwa sababu hazikutajwa. Hizi taasisi ni zipi na kila taasisi inafikia wapi katika mazungumzo na wote kama kitabu kilivyoeleza kwamba walikuwa na nia nzuri ya kuonesha kuwa watawekeza katika nishati hii.

Mhe. Spika, jengine nishati iliyotajwa huku ni nishati ya upepo, nishati ya jua na nishati ya gesi asilia. Lakini huku vile vile kuna nishati hii ya kutumia mawimbi ya bahari ambayo naamini taarifa yake tulikwisha kuipata tokea siku za nyuma kuwa zimo sehemu zilikaguliwa na zikaonekana kuwa tunaweza kupata umeme wa kutosha kwa kutumia mawimbi ya baharini. Ningeomba Mhe. Waziri anieleze kuwa Mhe. Waziri aliyekuwepo katika wizara hii ilipokuwa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi alikuwa akitupa taarifa kila kinachoendelea.

Mhe. Spika, kidogo ninaomba radhi kwa ninavyosema. Pamoja ya kuwa namshukuru sana Mhe. Rais kwa kuteuwa mawaziri waliokuwa ni makini sana na manaibu wao. Lakini kama ingelikuwa kuna uwezekano kwa Baraza la Wawakilishi kuteuwa ningelifanya kila inavyowezekana Mhe. Mansoor akarudi katika wizara yake. Mheshimiwa alifanya kazi kubwa sana mpaka akasema Mwenyezi Mungu anijaalie mimi nisife bila ya kuona kuwa mafuta ni ya Wazanzibari wenyewe. Alikuwa anakwenda hatua kwa hatua kuona kuwa tumepata nishati hii mbadala.

Suala la kutoa mafunzo ya matumizi ya nishati mbadala haisaidii lolote. Ningelimuomba Mhe. Waziri awe *serious* kwa hili, atueleze hasa ni mpango gani madhubuti anaoufanya, mambo ya tegemezi tunayajua na athari zake. Zanzibar itaweza kujitegemea kwa umeme wake wenyewe. Vyenginevyo itakuwa vigumu na sisi kuweza kupitisha bajeti hii kama hatukupata maelekezo ya kutosha. Sisi tunakubaliwa na tunaaminiwa na wananchi kuwa tunawafanyia kazi vilivyo tuone kuwa ile kazi yetu inakwenda kwa mujibu ilivyokadiriwa.

Mwisho nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na naomba kukaa kitako.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mchana huu wa leo kupata nafasi hii adhimu na mimi nikachangia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Spika, yale maeneo ambayo nimekusudia kuyachangia wenzangu wengi wameshapitia na mimi yamenigusa sana katika jimbo langu ni vyema kutoa mawazo yangu kwa Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, ili aweze kuwaonea huruma wananchi wetu wa jimbo la Tumbe. Nitaanza katika ukurasa wa 51 kifungu cha 89. Zanzibar imekuwa ni tatizo sugu la upatikanaji wa maji safi si mjini si vijijini. Miaka mingi tokea kuanzishwa kwa Baraza hili kelele ni maji. Maji haya bado wananchi wetu wanapata tabu kubwa sana.

Mhe. Spika, kama nilivyosema baadhi ya wachangiaji hoja, leo tupo mwezi 9 Shaabani inayotuelekea hapo mbele ni Ramadhani. Ramadhani kama tunavyoifahamu ni mwanamme, vitimbi vyake ni vingi. Ramadhani maji yanatumika kwa wingi zaidi kulikoni miezi mengine. Tungemtaka Mhe. Waziri atupe changamoto zake na msimamo wa wananchi wetu ambao wana tatizo kubwa la kupatikana kwa maji.

Mimi binafsi jana katika ziara zangu nimekutia maeneo mengi watu wamekusanya vyombo vyao wanasubiri maji. Sijui ikifika Ramadhani itakuwa vipi. Si hapa Unguja tu lakini hata katika jimbo la Tumbe tatizo hili tunalo. Miundombinu imepita bomba zinapatikana zipo lakini maji hayapatikani, hasa katika shehia ya Shumbaviamboni eneo la Kikunguni. Kuna eneo limechimbwa kisima muda mrefu, Kisima hicho hakipungui miaka minane lakini hatua zinazochukuliwa na serikali ni ndogo mno. Wananchi hawa bado wanaendelea kuathirika kutokupata maji safi na salama.

Ningemuomba sana Waziri suala hili alione na alichukulie hatua za haraka. Wananchi hawa wameshachangia sana, wameshanunua mabomba na mambo mengine mbali mbali. Lakini bado kufikia kuyapata maji haya yameshindikana. Ningelimuomba sana Waziri apige jicho la huruma ili wananchi wetu wa Shumbaviamboni na wao waweze kufaidika na maji safi ambayo tayari wameshayatayarisha katika kisima chao.

Mhe. Spika, pia nichangie katika upatikanaji wa umeme. Mhe. Waziri ametueleza katika kitabu chake ukurasa wa 57 kifungu cha 102. Kuna vijiji vingi amevitaja ambavyo vitafaidika na umeme kwa kupitia msaada kutoka Japani, kuna fedha za Tanzania karibuni bilioni 55, waliobahatika na mpangilio huu ni hapa Unguja tu, bilioni zote 55 hakuna hata bilioni 5 ambazo walipelekewa ndugu zetu wa kule Pemba. Hili linauma, yapo maeneo hayahitaji hata bilioni 5 kufikisha nguvu hizi za umeme, hasa jimbo langu la Tumbe. Kuna maeneo haya niliyoyataja ya Shumbaviamboni tayari yameshapimwa yanasubiriwa kupatiwa zana tu ili kuweza kufanikisha, maeneo yenyewe ni kama yafuatayo.

1. Migombe Shumbaviamboni

2. Nyuma ya Mti Shumbaviamboni

3. Sizini umeme umepita barabarani, pale kuna maeneo yanayomilikiwa na serikali tuna shule, hospitali, lakini vijiji vyote vinavyozingirwa na Shehia ya Sizini wananchi hao hawana umeme, tayari wananchi wameshajitayarisha wanacho kisubiri ni hili. Imekuwa ni tatizo.

4. Uondwe ya Tumbe Shumbaviamboni. Hawa tayari wanasubiri maana hata ule upimaji wa umeme tayari wameshapimiwa. Bado shirika halijawafikishia suala hili. Mimi nalishukuru sana Shirika la Umeme pale Pemba kwa jitihada zao. Tumeshawafatilia mara nyingi lakini tatizo ni kwamba wanasubiri vifaa vifike, ndio jawabu tunazozipata.

Mhe. Spika, kama walivyosema wenzangu kwamba umeme umekuwa ni ghali mno kwa wananchi wetu. Nguvu zao ni ndogo mno, umasikini umewakabili. Ningeliliomba sana Shirika kwa kupitia wizara yake waangalie sana upunguzaji wa bei wanazowapangia wananchi wetu. Wananchi hawana uwezo wa kuingiza umeme ni vyema wakachukua hatua ya kuwakopesha umeme ili waweze kupata matunda haya. Namuomba sana Mhe. Waziri haya maeneo ayaangalie sana ili waweze kufaidika na suala zima hili.

Katika nyumba za makaazi zilizojengwa na Mhe. Mzee Abeid Amani Karume, katika Wilaya yangu ya Micheweni hizi nyumba zinasikitisha, tokea zijengwe hadi kufikia leo hii hakuna huduma yoyote iliofanyiwa katika majumba yale. Zinatisha nyumba hizi hazieleweki. Hazina sifa ya kuishi mwanadamu. Ni vyema Mhe. Waziri atakapokuja hapa anijuilishe nyumba zile zitahudumikiwa lini kufanyiwa angalau matengenezo. Ishakuwa ni muda mrefu na wanaoishi mle ni binaadamu kama binaadamu wengine. Naomba Mhe. Waziri atakapokuja kujibu masuala anipe maelezo ya kina kuhusu nyumba zile za Wilaya ya Micheweni.

Kwa kumalizia niseme wenzetu wamesema kuwa mafuta ndio uti wa mgongo wa Zanzibar na uchumi wa Zanzibar. Ndani ya kitabu cha Mheshimiwa wamesema mafuta ni uchumi kwa hivyo suala la uchumi halimo katika muungano. Sasa kama waziri amekiri hivyo kwamba mafuta ndio uchumi na hayamo katika masuala ya muungano, tunataka yabakie katika maandishi tu. Kama tutabakia kwenye maandishi tu huo uchumi utakuwa vipi.

Mhe. Spika, Waziri mimi najua ni kidume, anamsimamo wa dhati kabisa, hebu hili suala alisimamie na sisi Wawakilishi wake tupo nyuma. Tunamuomba sana Mhe. Waziri kutokana na kujiamini kwake basi hili suala alisimamie vya kutosha ili Zanzibar tutokane na hii hali ngumu ya maisha. Mimi naamini kama

mafuta tutayasimamia na yakachimbwa. Mhe. Hamza amesema baada ya kuomba hatutaomba tena tutakuja sisi kuombwa, baada ya kusaidiwa hatutosaidiwa tena tutakuwa sisi ndio tunasaidi. Kwa maana hiyo mimi niseme tafiti tumezioneshwa mambo mbali mbali, kinachobakia ni sisi wenyewe tu Wazanzibari kushikama na hili ili tuweze kutoka katika maisha haya magumu.

Mhe. Spika, pia tuone hizi ni neema Mungu ametupa Wazanzibari, neema hizi alipotuletea Mungu ametuletea kwamba tuzitumie. Tunaishi tunakufa, hatima yake tutamalizika katika ulimwengu huu. Tukumbuke kwamba Mungu atakwenda kutuuliza hizi neema alizotupa tulizitumiaje. Ili tuweze kuzitumia, tukose kwenda kupata masuala mazito ni kuzishughulikia neema za Mungu alizotupa ili wananchi wetu watoke katika hali ngumu ya maisha tuliyonayo katika kipindi hichi au katika Zanzibar yetu.

Mhe. Spika, mengi wenzangu wamechangia na mimi hapa nimechangia nasema panatosha. Mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Tumbe tunaiunga mkono hoja asilimia 60 mpaka pale Mhe. Waziri atakapotuhakikishia suala la mafuta kwamba liko tayri na mipango yake imeshakamilika basi tunaweza tukamkamilishia Mhe. Waziri asilimia zake zikawa *mia fil mia.*

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Kwa leo sina mchango mkubwa zaidi kwa vile wenzangu wengi wamezungumzia masuala yote ambayo tunayahitaji Wazanzibari. Mambo tunayoyahitaji zaidi ni maji, umeme na mafuta kama yalivyozungumzwa. Kwa leo mimi sina zaidi isipokuwa nachangia ukurasa wa 49 kuhusu tatizo la maji vijijini.

Mhe. Spika, tatizo la maji vijijini ni kubwa sana kwa vile vijiji vingi ambavyo katika majimbo yetu yana matatizo ya maji. Hivi sasa utakuta katika vijiji hivyo hata mabomba yenyewe ya maji bado hayajafika mbali ya kwamba tuna tamaa yapo siku yatatoka lakini utakuta hata bomba lenyewe halijatandazwa katika ardhi kuweza kupata maji.

Ukitizama kijiji changu katika jimbo langu la Koani kuna vijiji ambavyo hata maji hawayaoni hasa ya bomba au kuyafahamu yanatoka vipi. Ukitizama katika kijiji cha Mkorogo, kijiji ambacho Wazanzibari hata hawakijui kipo wapi kutokana na kusahauliwa muda mrefu. Mkorogo hivi sasa kuna matatizo mengi ya maji ambako bomba hazijafika kabisa hata kulazwa katika ardhi. Kijiji cha Manyami hivi sasa kwa muda mrefu kijiji hichi hakijapata hata mabomba kulazwa angalau kuwa na tamaa lini tutapata maji katika sehemu hizo. Ukija kijiji cha Ponge vile vile utakuta sasa hivi wanayasikia tu maji lakini mpaka leo bomba hatujalaza katika maeneo hayo.

Mhe. Spika, namkumbusha Waziri atusaidie katika jimbo letu la Koani tuwe na tamaa kuwa ipo siku tuwe na maji. Muda umekuwa mrefu, vilio vya wananchi wetu matatizo makubwa ni maji. Kijiji cha Shehia ya Tunguu hatuna tamaa ya maji kwa sababu hata bomba hazijalazwa katika maeneo hayo. Sehemu zote hizo utakuta maji ni tishio la amani la wananchi. Mbali kujua kuna tatizo la kuchimbwa mafuta lakini maji angalau wananchi wa vijijini wanataka wajue maji yakoje, halafu ndio wataanza kujua kuwa mafuta yanatakiwa zaidi hapa Zanzibar.

Wazanzibari tuna matatizo ya umeme, vijiji vingi hivi sasa havijapata umeme, hasa ukitizama kijiji changu cha Manyami kinamatatizo ya mambo yote mawili kwa pamoja. Umeme haujapatikana hata siku moja sehemu za Manyami wana muda mrefu tangu tumepata Uhuru mwaka 1964. Hivi juzi nishati hii imeanza kutaka kufikishwa umeme pale Manyami lakini tumeambiwa hata maili moja haitoweza kutandaza waya, sijui kwa nini. Umeme kutoka Manyami hadi Machui haichukui hata maili mbili, lakini haikuweza kuunganishwa.

Suala hilo hilo la umeme Tunguu kuna hospitali inashindikana kufanya kazi. Hospitali hiyo tatizo kubwa ni umeme, wakati wa usiku mtu akipata ajali inakuwa shida kwani inakuwa haifanyi kazi. Wakati wa mchana inachukua muda mrefu kwa sababu vyombo vyake vingi wanaviweka kwa majirani katika vijiji vyengine. Ni lazime waende Fuoni kuweka madawa halafu yakachukuliwe Fuoni ili yaje pale kutumika kutokana na hakuna umeme kuweza kuhifadhia dawa. Sindano hazipati kuchemshwa hadi ziende kuchemshwa kwa jirani halafu ndio zije kutumika kwa kutwa nzima pale Tunguu. Hospitali ipo lakini utakuta haitowi huduma ipasavyo vile inavyotakiwa. Namkumbusha Waziri wangu ajue kwamba jimbo la Koani lina matatizo makubwa sana nayo ni matatizo ya maji na matatizo ya umeme.

Zanzibar tumepata majenereta mapya ni mengi lakini majenereta hayo Wazanzibari wengi tunajiuliza yamefika Zanzibar kwa shughuli gani, hatujajua bado. Kwa sababu linapotokewa tatizo ya kwamba yatumike kwa shughuli zake utakuta jenereta mpya zile zipo lakini utakuta hazifanyi wajibu wake. Tunataka kujua hizi jenereta zimeletwa kwa ajili gani, kama ni maonyesho tujue kwamba tunakwenda kutizama maonyesho. Kama zimekuja kwa utendaji wa kazi tunaomba siku linapotokezea tatizo japo jenereta moja lifanye kazi. Jenereta zile tunavyoziona ukubwa wake zingelitumika mbili tu au tatu kwa Zanzibar hii tungelikuwa tunapata faida ya jenereta zile. Lakini pana jenereta zaidi ya kumi na zaidi. Lakini hata jenereta moja hupati faida yake kwa siku nzima. Tunataka kujua biashara ile imeletwa Zanzibar kwamba ni msaada au imetoka fedha ya serikali na kama imetoka fedha ya serikali imetoka kiasi gani kupoteza bure na ni nani wa kuwajibika na wa kulaumiwa, kuleta kitu ambacho hakifai au hakitumiki katika nchi yetu.

Mhe. Spika, jengine ni kuhusiana na mambo ya nishati ambayo ni mahitaji ya kila siku. Tunaambiwa kwamba tutakuwa na nishati ya upepo, nishati ya jua na nishati ya gesi. Masuala hayo kila siku tunazungumza tu katika Baraza lakini hatujaambiwa nishati gani nchi gani inatoa msaada wa nishati fulani na nchi gani inatoa nishati fulani. Imekuwa ni ndoto tu ya kutaja mpaka linakwisha Baraza hatuoni nishati yoyote inayofanya kazi. Naamini kwamba itafika miaka mitano hatuoni nishati ya upepo wala nishati ya jua wala gesi asilia wala nishati ya maji ya bahari. Hii itakuwa mpaka lini Wazanzibari kuzungumza kitu ambacho hakitekelezwi.

Kwa hayo zaidi namuomba waziri azidi kueleza ukweli kwamba tunachokizungumza katika Baraza ndicho kinachotendeka. Tusiwadanganye wananchi katika majimbo yetu kwamba tunakwenda kwenye Baraza kuzungumza, itakuwa tunakuja kwenye Baraza kuimba nyimbo lakini nyimbo zenyewe hazina muitikiaji. Kwa hivyo namuomba waziri atakapokuja kuchangia bajeti yake ya mwisho atueleze, kwamba nishati fulani tunajiamini wenyewe Wazanzibari tutaishughulikia au nishati hiyo itashughulikiwa na China au Japan na itakuwa kwa mwaka gani. Isiwe tunazungumza tu lakini mwaka hatuujui ima iwe nishati ya gesi au maji ya bahari, au nishati ya upepo. Tunayo bahati yetu kubwa tu maeneo ya Kusini. Hata sisi Wazanzibari tunaweza kufanya miujiza tukaweza kutoa nishati ya bahari. Waogeleaji wazuri wapo, wavuvi wazuri wapo na wanaijua bahari vizuri. Tusingoje kutoka nje kusema kwamba tunangoja muhisani atuchangie. Ipo siku Wazanzibari tunamaliza umri wetu hatuoni jipya.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ninachotaka zaidi utusaidii kwa mwaka huu wa 2011/2012 tujue matumizi yetu ya nishati tunayatumia vipi. Kwa leo hayo ndiyo niliyochangia katika jimbo langu la Koani liweze kupata mafanikio ya mambo haya muhimu. Masuala mengine ya mafuta hayo kama yalivyozungumzwa yatakuja kwa wakati wake. Lakini angalau majimbo yaone umeme unapatikana, maji yanapatikana. Naunga mkono mimi pamoja na wananchi wa jimbo langu kwa asilimia mia bajeti hii na iweze kupita na iweze kutekelezwa. Ahsante sana.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kutoa angalau machache juu ya hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mchana huu kwa uwezo wake na rehma. Niombe pia kukushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nianze kwa kumpongeza Mhe. Rais kwa kumuona jemedari wetu Mhe. Ali Juma Shamuhuna na kumkabidhi wizara hii. Imani yangu ni kwamba

Mhe. Rais hakufanya kosa, anamfahamu na anamuamini na sisi tunampongeza kwa uteuzi huo.

Nimpongeze Mhe. Waziri Mwenyewe, watendaji na wafanyakazi wa Wizara hii kwa jitihada kubwa wanayoifanya katika kazi ngumu wanayokabiliana nayo.

Mhe. Spika, nende moja kwa moja na Idara ya Ardhi na Usajili. Idara hii ndio pia inayoshughulika na ukodishaji wa ardhi kwa wawekezaji wanaoweka mahoteli wanaojenga vituo vya mafuta, wanaojenga minara, mawasiliano na kadhalika. Minara hii wananchi wanafika kulalamika imewazunguka mno, labda ingefaa kwenye kitabu hichi Mhe. Waziri angewaonesha Wazanzibari kwa vile viwanja vya mahoteli tumepata kiasi kipi, minara imeingiza kiasi hichi, kilimo waliochukua ardhi ya kilimo tuna hatua hii. Angalau tukajenga imani kwamba kinachotendeka tunakiona.

Mhe. Spika, suala la ardhi ni nyeti sana kwa Zanzibar na duniani kote. Kwetu hapa na kwenye kitabu kumejengewa maelezo mengi. Kuna vitengo kadhaa mapaka mwisho kuna Mahakama ya Ardhi, ukitizama kwenye kesi ndipo utakapoona kweli kuna matatizo makubwa ya ardhi. Kesi zilizofungwa, kesi zilizofunguliwa hakuna uwiyano kamwe. Rafiki yangu, swahiba wangu mpenzi, Mhe. Waziri mwenye dhamana hii anakazi ngumu sana, tumsaidieni Ishallah aweze kutenda wajibu wake.

Mhe. Spika, ardhi pia ni uhai ndio yenye chemchem ya mengi. Kuna kitengo cha usajili hapa ni kutizama uhalali wa nani anapaswa kumiliki na kadhalika. Lakini kwenye kitabu kumetajwa utaratibu ambao ndio chanzo cha matatizo ya ardhi yalikoanzia ni Sheha, Wilaya na Mikoa. Mhe. Spika, sote ni mashahidi wa hili kwamba huko kila mtu anakwambia serikali yangu mimi ya Shehia anaamua vyake, Serikali yangu mimi ya Mkoa anakwenda atakavyo huko kwenye Serikali Kuu ndiko kwenye sheria ya mambo haya na utaratibu wote kupeleka madaraka Mikoani hapakuwa na sababu ya kufikia hali iliyopo.

Mhe. Spika, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwenye hili sitaki ninukuu kauli yake, lakini nanukuu tafsiri yake kwamba amesema “walioligema walinywe wenyewe”. Mhe. Spika, hii ni kumpunguzia Mhe. Waziri kazi nzito ambayo itatupotezea muda nawaomba sana wale wote waliohusika na kuvuruga utaratibu huu wa ugawaji na kumilikisha aridhi ovyo wayatengeneze ili watupe nafasi.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye chemchem ya Mtoni na viwanja vya Garagara. Mhe. Spika, chemchem hii ni ya historia kubwa ambayo ilianza tokea mwaka 1923, chemchem hii walipoijenga Wakoloni ilikuwa inatiririsha maji Saateni

bila ya kutegemea nguvu za umeme. Pia chemchem hii bahati mbaya hapa kati kati tena ilivamia na makaazi ya watu, tukabahatika kupata mradi wa maji Mijini, mwenye mradi akatushauri kwamba ama tufunge chechem ile kwa makaazi ya watu au watu tuwaondowe wapelekwe sehemu nyengine kusudi chemchem iendelee na shughuli zake. Mhe. Spika, aliahidi watu hawa wakihamishwa atawapelekea maji huko watakakopelekwa, lakini wahamishwe kwa utaratibu unaofaa sio kudhalilishwa.

Mhe. Spika, nashukuru zoezi hili lilianza vizuri bahati mbaya sana likatokea lilotokea kuripuka kwa transfoma ile ya Mtoni sasa ikawa ni vunja vunja, utaratibu ule ukakoroga na maisha ya watu yakapotea. Mhe. Spika, baba mmoja ninaye mfahamu ambaye alikuwa na miji miwili baada ya nyumba yake kuvunjwa huko kwenye chemchem anakwenda mji wa pili kutizama watoto wake anakutana na kijana wake wa kiume na yeye anatoka kule kuja kumpa taarifa baba yake kwamba nyumba na kule imeshavunjwa. Mhe. Spika, mtoto yule kumpa taarifa baba yake basi alianguka na akapoteza maisha yake pale pale.

Mhe. Spika, nayasema haya kwamba yametokea kwa kulinda chanzo hiki cha maji kwani ni muhimu sana, meli za kigeni zilikuwa zinachukua maji hapa safi na salama. Mhe. Spika, inasikitisha leo kukatoka kibali kwenda kujengwa kituo cha mafuta eneo hili hili tulilowaondoa watu wasikae kwa uchafunzi wa maji haya. Mhe. Spika, tunawakinga watu wasijekunywa visivyonywewa kwa sababu wakaazi wa pale watajenga vyoo, leo tunataka kuwanywesha mafuta hivi kweli tunafanya nini.

Mimi naelewa wazi kwamba eneo limezuiwa, lakini aliyepewa kibali amepewa na chombo cha Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hivi kwa nini tunafika mahali tunajua hiki tunachokifanya watu watakwenda kufa kunywa mafuta taratibu maji yale yanatiririka Mji Mkongwe na maeneo mengine ndiko yanakokwenda maji haya. Mhe. Spika, naomba sana tulifahamu hili kwani kibali kimetoka kwenye Mamlaka husika kujengwa vituo vile.

Mhe. Spika, sasa niende kwenye suala ambalo nashukuru Waheshimiwa Wajumbe wako wa Baraza hili tukufu wamelieleza kwa kina na kwa hisia za wananchi wa Zanzibar kwa umuhimu na uzito wa jambo lenyewe. Pengine sitokuwa na mengi zaidi ila kuna vipengele ambavyo wenzangu hawakuvigusa ili Wazanzibari wanaotusikiliza na waliotuleta hapa kwa kaza maalum yakuwatumikia wao waweze kutusikia.

Mhe. Spika, kwa kuwa kuna sheria inaitwa *Petrolium Exploration and Production Act of 1980* masuala ya mafuta na gesi ni ya Muungano, sina utata na hili Mhe. Waziri wa Fedha alilisema na akasema tutakapoyachimba

tutayachimba chini ya sheria hii. Mimi sisemi sio sahihi nasema ni sahihi kwa sababu sheria bado haijabadilishwa. Lakini ndani ya sheria hii chombo kinachoitwa *TPDC* ndicho kinachoratibu na kusimamia shughuli hizi, ndani ya *TPDC* Wazanzibari tumo ni cha Muungano na hatuwezi kusema tu kwamba tunakisusia hiki hatutaki kushirikiana nacho, lakini hayo ni maneno tu kitendo ni hii sheria.

Mhe. Spika, kweli tukisusie chombo hiki ni lazima tulete sheria yetu hapa ndani ya Baraza hili itakayosema sasa Zanzibar wana sheria yao ya kuunda chombo chao cha kusimamia mambo ya utafutaji mafuta na gesi asilia. Vyenginevyo vyovyote bado tuko ndani ya mibano na ndio maana Mhe. Waziri Mkuu leo anakwenda kuzindua ile meli akiwa na uhakika anachofanya yuko ndani ya sheria. Kwa hivyo, hoja kwetu sisi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili ni kuiuliza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kwa nini sheria wameidhibiti kuifungia kabatini, vyenginevyo vyovyote kama bado sheria haijaletwa hapa tukaifanyia kazi basi haya mambo ni magumu kwetu.

Mhe. Spika, *TPDC* ina fedha za Wazanzibari nyingi sana, fedha zetu ziko chombo hiki kwa sababu kampuni zinazokuja zinakuja serikalini baadae wanakaa na *TPDC* kwa sasa Tanzania, *TPDC* wanatoa leseni wakishatoa leseni ndio kampuni zinatoa fedha na fedha kubwa ambayo inaniuma mimi ni ile fedha ya *training fees.* Wazanzibari wetu hawa vijana wangeweza kusoma masuala ya mafuta na gesi bila ya sisi kushughulika kwani hii fedha ni nyingi na ipo.

Mhe. Spika, watu wengine hawatuelewi wanatushangaa Wazanzibari tunafanya nini, pesa zenu hizi hamzitaki zipo leo tunasema hatutaki kushirikiana na *TPDC* kwa mkono mmoja, kwa mkono wa pili Katibu Mkuu wa wizara hii ni Mjumbe wa Bodi wa *TPDC*. Mhe. Spika, maana yake ni kusema hatutaki mchuzi tunataka ile nyama tu, hivyo tunafanya nini. Mhe. Spika, mimi sifahamu hili.

Mhe. Spika, mimi ninachoiambia serikali yao ya kisiasa yabaki yao lakini pesa zetu zilizopo TPDC tunazitaka wenyewe hili ndio la msingi, kampuni zilizoko baharini wanatafuta mafuta wamelipa, kampuni zilizopo kwenye maziwa kule Tanganyika ziwa Victoria wamelipa, kampuni zilizokuwa ardhini pia wamelipa. Mhe. Spika, kwa kweli hizi fedha ni nyingi sana hivyo mama na baba wakihitilafiana wewe baba bado hujanusurika wala huna cheti cha kuwanyima huduma watoto wako. Mhe. Spika, utafanya dhuluma kubwa na hiyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tunaiomba sana kwa heshima na taadhima Wazanzibari wana shida nyingi, hospitali kumeoza, elimu ni balaa tupu, barabara zogo. Kwa hivyo, tunaiomba ile pesa yetu iliyoko kule kwani ni haki yetu na ni damu yetu kwani kuomba mtu kitu chake sio dhambi. Kwa

hivyo, tunaiomba serikali itutafutie chetu ili lazima tuwe na chombo ambacho kitakuwa tayari kuratibu shughuli hizi, chombo hiki kinataka wasomi, wataalamu hivyo sisi tutawatoa wapi.

Mhe. Spika, walikuja hapa washiriki wa kampuni ile wakataka vijana kumi wasomeshe, hadi hii leo Mhe. Waziri hebu twambie utakapokuja ni wangapi wamekwenda kusoma kwa mwevuli wa kampuni ile. Mhe. Spika, lakini kwa nini tutegemee watu na cha kwetu kipo mimi hili naomba jibu, pesa za *TPDC* zinatutosha kuwasomesha watu wetu na tukabaki mwiku wa kufanya mwengine.

Mhe. Spika, masuala haya hayendi hivi tu kwa maneno tumeshasema sana na maandiko yapo, ndugu yangu Mhe. Jussa ameyatoa amenipunguzia kazi kubwa kwani leo nilikuwa nimejiandaa kuja kuwaonesha Waheshimiwa wako na Wazanzibari wote Katiba zote ninazo. Lakini ni kwamba mambo mengi kabisa yameshazungumzwa ninachotaka kukisema mimi Mhe. Spika, ni kwamba Wazanzibari wanataka mustakbali mwema, wanataka maelekezo na maelezo juu ya masuala mazima ya uchimbaji wa mafuta na gesi asilia. Mhe. Spika, ni kwamba hatuna nia kabisa ya kumsumbua Mhe. Waziri tunachotaka sisi ni serikali kutupa kauli tumeshaiona kuna lugha ya kiza nini la zaidi baina ya SMZ na SMT. Mhe. Spika, hili sisi halitusaidii, siasa ni wakati wa siasa lakini tunataka siasa kuutumikia uchumi sio suala jengine.

Mhe. Spika, sisi tunataka uchumi wetu Mhe. Jussa ameinukuu Katiba sitaki niirejee, tuna haki ya kulinda uchumi wetu mikononi mwetu wenyewe. Lakini labda niseme na nikumbushe kwa ruhusa yako Mhe. Spika, ni Katiba yetu ya Zanzibar ya mwaka 1984 kifungu cha 9 (1) ni kwamba "Zanzibar itakuwa ni nchi ya kidemokrasia na haki za kijamii". Kwa hivyo, hapa inaelezwa rasmi kwamba mamlaka ya kuendesha nchi ni wananchi wenyewe ambapo nguvu na uwezo wote wa Serikali kufuata na Katiba hii utatoka kwa wananchi wenyewe.

Mhe. Spika, kwa tafsiri yetu sisi tusokuwa na sheria wananchi sisi ndio wenye mamlaka ya nchi hii na sio serikali, serikali inatia mkataba na sisi. Kwa hivyo, inapotufikisha serikali mahali kama hapa tunapata wasi wasi kwa nini mkataba hautaki kuheshimiwa na kufuatwa. Kwa nini tunaiuliza hivyo? Mhe. Spika, serikali imeshindwa mimi siamini ama kuna nini kuhusu hili.

Mhe. Spika, masuala haya yako chini ya Idara ya Nishati na Maadini bahati mbaya idara hii Mhe. Waziri utanisamehe mzee wangu ndani ya wizara hii, hii idara ambayo ingepaswa kuratibu mambo haya na tungekenda kama tulivyokwishapitisha ndani ya Baraza hili idara hii imetengwa. Mhe. Spika, Idara ya Maadini na Nishati imetengwa na kwa lugha mbaya ambayo haipendezi imefanywa Guantamo, ndani ya wizara hii inasikitisha leo Mhe.

Waziri anakamilisha sijui mwezi wa saba tokea ateuliwe kupewa dhamana ya wizara, idara hii ukimuuliza Mhe. Waziri Mkurugenzi anakaa upande gani ndani ya ofisi hatojibu. Mhe. Spika, hawezi kujibu kwa sababu atayajua vipi haya tunayoyazungumza sisi na ayapate kutoka wapi.

Mhe. Spika, katika utaratibu unaoendelea inatisha na haipendezi hata kidogo ndani ya wizara moja kukaa na idara bwana na idara bibi na idara kaka hii siyo sura nzuri.
Mhe. Spika, idara hii *engineer* anapata shilingi laki moja na sabiini, Mkurugenzi ana 1.4 milioni huyu *engineer* miezi minane ndio amfikie Mkurugenzi mshahara wake. Mhe. Spika, wataalamu wote wataondoka katika sura hii na tutabaki kulaumu uzalendo una kikomo kama utadharauliwa utachoka, lakini hali ikishakufika mahali unasema basi.

Mhe. Spika, kwa uteuzi aliouteua Mhe. Rais kumpa Mhe. Ali Juma Shamuhuna wizara hii nina imani na sisi tuko pamoja nae kama atakubaliana na sisi kuitaka serikali itupe majibu tunayoyatarajia na hatutaki lugha ya siasa wala imla. Mhe. Spika, tunataka ni lini sheria itafunguliwa ofisini iletwe hapa, hapa ndio tutaweza kupitisha na kujenga chombo tutakavyokiita vyovyote ni chetu wenyewe, hilo ndio dira vyenginevyo waheshimiwa tusidanganyane. Mhe. Spika, mwenendo unaokwenda na serikali wallahi nasema tutakuja lizana machozi ya kuku kwani vizazi vyetu vitakuja kututia moto kwa kutulaani, chao kinachukuliwa na wao ni mashahidi kinachukuliwa hivi hivi. Mhe. Spika, wanaofanya wanafanya kwa kujiamini wanachokifanya, sisi tuna gati gati hivyo hapa kati kati kuna nini?

Mhe. Spika, nashindwa kusema neno nitakaloeleweka kwamba sasa tunataka hili jambo kikao hiki cha bajeti tufahamishwe. Kwanza Mhe. Spika, niseme bajeti hii mimi kwa heshima ya Mhe. Waziri nazuia asilimia 90 asilimia 10 nampa yeye kwa heshima yangu, nafanya hivyo nataka tupate maelezo Wazanzibari huko nje wanatutizama na wanatusikia, maelezo yatakayokidhi mahitaji yetu kwamba sasa tunaelekea kule tunakokutaka. Mhe. Spika, mimi nasema hatoweza kutwambia lini atachimba mafuta mimi naamini hilo, lakini atwambie lini naileta sheria kuelekea kuundwa kwa chombo hicho. Mhe. Spika, akisema hilo basi tunaipitisha bila ya matatizo.

Mhe. Spika, kinyume na hicho tunaizuia hoja hii na jibu la pesa zilizoko *TPDC* za Wazanzibari ataanza vipi na hatutaki kero kwani lugha ya kero tumechoka. Mhe. Spika, tunataka uende udai kwani ni haki yetu wanazo na zipo lakini vijana umewatia kamba wasiende, umemuachia Katibu Mkuu peke yake anaingia na mkoba kwenye mikutano, tunataka na zile ripoti za kwenye mikutano uzilete hapa Mhe. Waziri tunataka tujue kunazungumzwa nini. Mhe.

Spika, kama ni siri iwe siri ya Katibu Mkuu na *TPDC* peke yake, Katibu Mkuu ni wa wizara hii.

Mhe. Spika, kwa kadri ya maelezo nina imani yamefika sasa nimalizie Waheshimiwa Wajumbe nikwambieni hali tuliokwishafika nayo kwamba *Pemba - Zanzibar Block* kisheria hivi sasa imo ndani ya mikono ya Kampuni ya Antrim na *RAK GAS* ya Rasil kheima ambayo hivi karibuni wametiliana saini kwa mashirikiano.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako namalizia kwamba. *Stephen Greer, President and Chief Executive Officer of Antrim Energey, commented. Wwe are very encouraged by the entry of RAK GAS in to this licence. The Pemba - Zanzibar Block has enormous exploration portation, and the area has recently been attracting considerable interest from major petroleum companies. We expect these two agreements, and the participation of RAK GAS in particular, will lead to a resumption of exploration activitiy on the Pemba – Zanzibar Block in the near future.*

Mhe. Spika, hii ndio hali tunaiomba serikali itufanyie kazi iliyoahidi kwa wananchi, sisi kama wawakilishi wa wananchi umetuapisha hapo mbele na tukasema tutalinda na kuzitetea Katiba zote mbili na tukamwambia ewe Mwenyezi Mungu tusaidie. Kwa kweli tutafanya vituko tusipoyakamilisha hayo. Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunivumilia, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa kunisikiliza. Ahsante sana.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, nakushukuru kwa dhati kabisa pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema pia nimshukuru Mhe. Waziri kwa namna alivyowasilisha hotuba yake. Mhe. Spika, nitajitahidi kuzungumza haraka haraka ili kulinda muda wako na nisiwachoshe Waheshimiwa Wajumbe kwa sababu mengi yameshazungumza, watu wameshamwaga nondo, nakala zote zimeshatolewa lakini naomba nizungumze kwa ufupi kabisa kuhusu Mamlaka ya Maji.

Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Rais kwa uteuzi wa Mkurugenzi mpya wa Mamlaka ya Maji, imani yetu ni kuwa wananchi wananchi wa Zanzibar imeanza kujengeka baada ya kupata Mkurugenzi mpya. Mhe. Spika, mamlaka hii tunaizungumzia sana kwamba pamoja na jitihada za serikali, lakini tulikuwa tuna matatizo na tunatoka imani na utendaji wa kazi wa Mamlaka ya Maji. Mhe. Spika, tukisema tuna ushahidi sio tunasema labda kwa sababu hatuna imani na watu, tunazungumza kwa ushahidi.

Mhe. Fatma hapa alizungumza jinsi tunavyofuatilia masuala ya maji kwa majimbo matatu, kwa bahati pale katika viwanja vya Demokrasi tuna mradi wa

SEMUSO, mradi huu umegusa Sebleni kwa mantiki ya Jimbo la Amani, Sogea kwa mantiki ya Jimbo la Magomeni na Muungano kwa mantiki ya Jimbo la Kwahani.

Mhe. Spika, mradi ule umetumia pesa nyingi sana chakushangaza kwamba hatujui tatizo ni nini na linalotushangaza ukenda mbio basi siku ya pili yake maji yanatoka, lakini ukikaa siku tatu yanakatika. Mhe. Spika, kuna siku tulifanya utafiti wa kutosha, tukatoka na timu kama majimbo matatu tukenda kwa Mkurugenzi aliyepita tukamwambie leo tunataka utupe wahandisi wako tutoke mguu kwa mguu tufuatilie kuanzia kisima cha Amani nyuma mpaka tufike lilipo tenki. Mhe. Spika, chakusikitisha tulipofika katika kile kituo tulimkuta mwana mama ambaye ni mlinzi bila ya kujifahamu akatoa siri za watendaji wa mamlaka ya maji, akasema mashine iliyokuja kuchukuliwa juzi ilikuwa inafanya kazi vizuri lakini hii iliyowekwa sio nzima. Mhe. Spika, haya mambo kidogo yanatuumiza vichwa kuna nini na wamekosa nini watu wa majimbo haya, kwa sababu kama mashine ilikuwa nzima inachukuliwa inapelekwa kwenye maeneo mengine wananchi wa majimbo yale walikuwa hawastahili kupata maji, hiyo kauli tumeipata pale.

Sasa haya ni baadhi ya mapungufu lakini nasema kwamba leo sitozungumza sana kwa sababu nimeanza kujenga imani na Mkurugenzi aliyeteuliwa karibuni na kwa bahati nimeweza kukutana nae mara moja, najenga imani kwamba mabadiliko katika mradi huu yatapatikana ili kuondosha usumbufu kwa wananchi wetu, *tumezungumza* mengi karibuni swahiba wangu Mhe. Haji Omar Kheri alipokuwa anawasilisha hotuba yake alizungumzia masuala ya uwajibikaji, moja likaelezewa suala la kufuka kazini mapema na kuondoka kwa mujibu wa sheria, lakini haya tutakuja kuwalaumu wafanyakazi na tutakuja kuwaonea bure kwa nini tutawaonea. Mheshimiwa maji nyumbani hayatoki unatakiwa ukoge uende kazini utawahi kweli.

Mhe. Spika, tujitahidi kuondosha tatizo la maji ili tuweze kunusuru mambo mengine madogo madogo, Jimbo langu la Kwahani sasa hivi hususan Shehia ya Muungano imekuwa tunapoteza uzazi mwingi, nikizungumza hivyo kila mmoja anafahamu nini nazungumza, kuna mambo ukiyafanya lazima asubuhi unahitaji maji tuna hofu ya kutafuta watoto kwa sababu ya maji, maji ni muhimu sana na mimi nimeshauliza masuala sana hapa majawabu yanakuwa hayo hayo ya kisiasa tunajitahidi, tutajitahidi, tunatengeneza lakini hakuna kitu. Haya ni matatizo katika Shehia yangu mimi ndio kwenye kituo kikubwa cha wazega zega wameshafika mpaka kuunda timu ya mpira.

Mhe. Spika, hii kadhia ni kubwa sana na atukianza kuyachambua maji tatizo litakuwa kubwa sana ukiambiwa tu jawabu linakuja atunajitahidi, lakini kubwa utaambiwa tunatoa maji kwa mgao tumeshajibiwa hapa serikali inajitahidi na

maji inatoa kwa mgao, mgao wetu katika Jimbo la Kwahani katika siku tatu tunapata maji siku moja, kwa mahisabu ya haraka haraka kwa mwezi tunapata maji wiki moja siku nyengine tusikoge, tusinywe maji. Tunaiomba serikani na nina imani kwa ushupatu wa Mzee wetu Mzee wa Busara na hekima Mhe. Ali Juma Shamhuna atajitahidi na namuomba ajitahidi na kwa imani ya Mkurugenzi mpya ambae tumempata katibuni ajitahidi ili haya matatizo yaondoke ramadhani inakuja, Mhe. Naibu Waziri alitujibu tukajitahidi tutaleta magari ya maji hakuna magari ya maji tuambizane ukweli kabisa, mamlaka ya maji yanazuiliwa mpaka mwaka uliopita serikali au Mamlaka ya Maji ilitoa kauli kwamba waheshimiwa madiwani wasifuatilie watu wanagombana waheshimiwa kwa waheshimiwa wanagombana.

Halafu pia hatutegemei kufika katika maeneo yetu kwa sababu kwa siku unaletewa gari moja kutwa nzima kwa sababu magari hayatoshelezi, unapeleka shehia ya Muungano, Shehia ya Mikunguni wanakwembea unawapendelea Muungano Mikunguni hutuleteei, bado tatizo tujitahidi na mungu atatusaidia tutaonesha tutawezesha hapo.

Lakini nimalizie katika kilio cha wananchi Mhe. Spika, kilio cha wananchi wa Zanzibar ambao wametupa imani ya kutuchagua na kutuleta hapa nchi yetu utumi ni duni, nchi yetu ni masikini Mwenyezi Mungu ametusaidia tumeipata hii lulu, sina haja ya kusema mengi waliolia wameshalia, waliotoa nondo wameshatoa nondo suala la mafuta halina mbadala wala mjadala, vikao vilivyopita vya awamu ya sita vimefanya kazi nzuri vimeelimisha kadiri ya kuelimisha watu wa kupelekwa kwenye uelekezi wamepelekwa yaani kila jambo limemaliza tatizo liko wapi. Rasimu zimetekelezwa lini zinashindwa nini kufikishwa Barazani Mhe. Spika, tunaomba kwa dhati kabisa, Mhe. Waziri atutayarishie sheria kikao kinachokuja cha Oktoba basi iletwe hapa ili tuweze kuijadili na kufanya kazi ya kuchimba mafuta wenzetu na ndugu zetu hawatutakii jema katika suala la uchumi hata siku moja.

Tutauzungumza muungano katika mambo mengine lakini tukianza kugusa uchumi kwa wenzetu wa Tanzania Bara imekuwa tatizo, na ugomvi mkubwa wa muungano huu uko katika suala la uchumi na kelele zote tunapiga katika sehemu za uchumi, tutazungumzia *TRA* na mambo mengine lakini hapa ndio tatizo hapa tumeambiwa kero ya Muungano ya *TRA* kutoa mzigo Zanzibar kupelea Dar es Salaam limepatiwa ufumbuzi. Juzi Makamo wa Pili wa Rais nimemkabidhi *document* mtu amelipia Zanzibar na Bara amelipia *document* anayo nasubiri jawabu. Bado tatizo imekuwa tunazungumza mdomoni tu kama maneno ya msanii tu upande mwema upande mnafiki hatufiki.

Mhe. Spika, mimi naunga mkono kwa niaba yangu na wananchi wa jimbo la Kwahani kwa sababu wenzangu wengi tu wao wamepita katika upande

mwengine lakini niko nao pamoja, kwa sababu nina imani kwamba leo Mhe. Ali Juma Shamhuna atatupa tamko la kuturidhisha sina wasi wasi nae, hilo ndio linalonipa imani ya kuunga mkono hoja kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimboa la Kwani.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kwa sababu muda umeshakimbia nakushukuru sana na naomba nikae ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe nakushukuruni kwa mashirikiano makubwa katika kuendeleza mjadala wa hotuba hii ya Wizara ya Ardhi, Makazi Maji na Nishati, kabla ya kuahirisha kikao nimeombwa niwaarifu Waheshimiwa Wajumbe Wawakilishi wa Chama cha Mapinduzi wabaki humu ndani mara baada ya kuahirisha kikao hiki, wengine baada ya hapo itakuwa ruhusa.

(Saa 7.00 Mchana Baraza liliahirishwa hadi Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 Jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru sana kwa kuweza kunipatia nafasi ya kuweza kutoa maoni yangu juu ya kitabu hiki cha Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, vile vile napenda nitoe pongezi zangu kwa Waziri kwa maelezo mazuri katika kitabu chake, nawapongeza Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wote kwa kazi nzuri ambayo wameifanya.

Mhe. Spika, mimi nitaanza kuchangia kwanza katika jimbo langu na baadae nitendelea, sisi tuna barabara ambayo tunajenga kutoka Wete kuendea Konde na katika barabara hii inapotengenezwa barabara kunatokea uharibifu wa mabomba ya maji ambao tulitegemea kwa muda mrefu suala hili lingemalizika, lakini mpaka sasa hivi suala hili limekuwa gumu na wananchi wanapata usumbufu wa maji kutokana na mabomba ambayo yanahitaji kutandikwa mapema ili watu waliokatiwa maji waweze kupata maji. Kwa hivyo kutokana na suala hili muhimu ambalo wananchi wanategemea kupata maji lakini kutokana na ulazaji wa mabomba kushindwa kufikia kikomo ambacho kinatakiwa imekuwa inaleta usumbufu. Kwa hivyo ningelimuomba Mhe. Waziri katika suala hili aweze kulifuatilia kwa karibu zaidi ili wananchi wa Konde waweze kupata maji.

Mhe. Spika, sasa nataka kuzungumzia suala zima la mtandao wa maji Msuka, mtandao wa maji Msuka ni dhaifu sana na usambazaji wake unakuwa na

mashaka, baadhi ya maeneo mengi maji hayafiki sawa sawa maji yale kwa wananchi yanakuwa hayana uhakika, siku nyengine wanapata siku nyengine wanakosa na maji haya yanakuwa yanatolewa kwa muda mfupi sana kiasi ambacho hairidhishi utokaji wake. Mtando mzima huu wote hauna nguvu.

Kwa hivyo napenda kumshauri Waziri ili kuufanya mtandao wa maji ambao unapeleka Msuka suala moja muhimu kama litaweza kufanyika huu mtandao utakuwa madhubuti na hawa watu wa Msuka watapata maji, baada ya Kituo cha Polisi kile cha Konde tuna *bore hole* ya maji na *bore hole* hii mpaka leo haijatumiwa, nimejaribu kushauri mara moja kwamba mtandao wa Konde na mtandao wa Msuka ni mitandao mwili mbali mbali waweze kupatiwa maji kwa haraka kwa kuweza kuwekewa mashine ya maji katika *bore hole* ile suala hili limeshindikana mpaka leo, mashine haijawekwa bado. Kwa hivyo usumbufu unaendelea na umekuwa mkubwa sana na watu hawapati maji.

Lakini vile vile ikiwa fursa hii itaweza kupatikana itakuwa ni vizuri zaidi namuomba Mhe. Waziri kwa vile *bore hole* hii ipo na ina maji mengi ya kutosha inaweza kusaidia mtandao mzima wa Msuka pamoja na Konde yake, kwa hivyo ningemuomba hapa Mhe. Waziri atuhakikishie au atupe taarifa kwamba hili suala tunaweza kupata hii mashine ya kuweza kuweka katika *bore hole* ile pale na kupata mtandao wa umeme vile vile.

Mhe. Spika, tatizo jengine ambalo linachelewesha huo mtandao wa maji kwa jumla kutoka Konde mpaka Msuka ni suala zima la *pip lain* ambazo hizi ziko katika ujenzi wa barabara, inalazimika hizi *pip lain* ziweze kufika katika *bore hole* ile iliyopo pale baada ya Kituo cha Polisi cha Konde, ambazo *pip* hizi mpaka hivi sasa Mhe. Waziri hazijafika kama ingelikuwa *pip lain* katika barabara hii za ujenzi huu mpya wa barabara zimeshafika Konde basi tungeweza kupata maji Konde kwa watu wote na watu wa Msuka wangeweza kupata maji na kuondokana na usumbufu huu. Kwa hivyo Mhe. Waziri nakuomba hilo suala la kupatikana kwa *bore hole* ile ya Konde iweze kupatikana.

Mhe. Spika, kuna suala jengine ambalo ni muhimu vile vile nakumbuka kipindi kilichopita hapa tuliwahi kuzungumza kwamba tuna watu wenye uwezo wametia mifereji ndani ya majumba yao, na kuna wale ambao hawana uwezo wakawekewa mifereji ya nje lakini hapa ningeliomba Mhe. Waziri, katika kipindi kilchopita tulikubaliana kwamba mifereji ya nje watu walokuwa hawana uwezo wasilipe maji. Lakini cha kusikitisha katika Jimbo langu mimi kuna watu ambao wana mifereji hii ya nje tayari wameshatozwa fedha tena sio kidogo kwa sababu ya maji, sio chini ya Shs. 12,500 wanatozwa.

Sasa mimi nilitaka kumuuliza Mhe. Waziri je kuna mabadiliko ya hii sheria, kama tulivyokuwa tumezungumza kipindi cha nyuma kwamba mifereji ile iwe huru kwa wananchi kuchukua maji, lakini sasa hivi watu wanatozwa pesa kutokana na mifereji ya nje. Sasa kama kulikuwa na maamuzi katika Idara au kulikuwa na maamuzi katika Wizara sisi hatujapata taarifa hii kwamba watu watozwe pesa kwa mireji ya nje. Sasa hapa nilitaka kumuomba Mhe. Waziri atupe maelezo kama kuna maelezo ya Wizara tujue kwamba watu wote wenye mifereji ya nje walipe maji tujue kama watalipa, lakini sio wengine wanalipa wengine hawalipi. Kwa hivyo hapa nilitaka Mhe. Waziri katika majumuisho yake aje atueleze kwamba hilo sio kweli na hilo lilikuwa ni kosa, au ni sawa watu wote wanatakiwa walipe maji katika mifereji ya nje.

Jambo jengine la maji ambalo nataka kulizungumza ni suala zima la hapa mjini tulipo, sisi tupo hapa kwa wiki ya pili hii tunaishi katika Zanzibar *town* na kwa kweli hapa mjini miaka kumi hii sasa hivi bado kuna usumbufu wa maji katika majumba makubwa ya Michenzani, bado maji yana udhaifu sana hayapatikani. Hili jumba la mwisho jumba namba kumi ambalo limemalizia hivi karibuni maji hayapatikani kabisa na ikiwa yatapatikana basi ni usiku wa manane, tulitaka kumwambia Mhe. Waziri mambo mengine ni lazima uyafuatilie uyajue yanavyokwenda kwa sababu kipindi kinachokuja ni kipindi cha Ramadhani na kama unavyojua ramadhani maji mengi yanahitaji kutumika, na kama usumbufu tunaoupata mwezi wa kula mchana na Ramadhani utakuwa ni huu huu basi hali itazidi kuwa mbaya, kwa sababu itabidi watu wakatafute maji mbali sana na mwezi mtukufu kama ule sio jambo zuri.

Kwa hivyo kama kulikuwa na utaratibu wa kupeleka maji katika majumba makubwa ya Michenzani hebu utaratibu uangaliwe tena ujulikane ni aina gani ya utaratibu watu wanapata maji kwa siku ngapi, na hii isifichwe ijulikane kwamba siku kadhaa na siku kadhaa maji yatatolewa katika maeneo hayo. Kwa hivyo ningelimuomba Mhe. Waziri katika mazungumzo yangu ya maji mjini hapa aweze kuyapitia na kuweza kujua utaratibu wa maji unakwenda vipi, hali ni ngumu na sisi tunapata tabu ya kutosha.

Mhe. Spika, nitaka nizungumzie suala zima la maji, katika awamu zilizokuwa zimepita mimi katika jimbo langu niliweza kupata maji katika sehemu za Msuka, Kipange, Mtondooni na Bandari Kuu, lakini katika awamu hii katika bajeti ya Waziri sikuweza kuona maeneo mengine ambayo nitaweza kupatiwa maji na mimi nina mashaka katika maeneo yangu madogo madogo ambayo bado umeme haujapatikana kwa mfano sehemu za Ungi, Gombani na Chaleni hizi sehemu hizi bado zote hazijapata maji.

Ningekuomba Mhe. Waziri kwa vile maeneo haya niliyoyataja hayakubahatika kupata maji katika awamu hii ningelimuomba basi Mhe. Waziri katika bajeti

yake ya mara hii ya mwaka 2011/2012 angalau katika maeneo haya matatu niliyokuwa nimeyataja na wao waweze kufikiriwa angalau maeneo mawili waweze kupata maji, wasogezewe mahala walipo.

Mhe. Spika, sasa nazungumzia suala la Mkia wa Ng'ombe nimelizungumza mara nyingi kwamba watu wa Mkia wa Ng'ombe wamebahatika kupata mambo mawili muhimu, wamebahatika kupata skuli ambayo inawasaidia, wamebahatika kupata hospitali ambayo inawasaidia. Lakini tatizo lililoibuka katika eneo lile ni kwamba hawana umeme kipindi kilichopita nilijaribu kutoa tathmini hapa ya kueleza jinsi ya kupata umeme Mkia wa Ng'ombe tukajaribu kupitia kwa njia ya Bandari Kuu moja kwa moja mpaka Mkia wa Ng'ombe, tukaona gharama ni kubwa sana kutoka Bandari kuu mpaka Mkia wa Ng'ombe, lakini nijaribu kumshauri Waziri ikiwa kwa kutumiamaguzo na waya kutoka Bandari Kuu mpaka Mkia wa Ng'ombe basi waweze kupata umeme wa *solar* lakini mpaka hii leo sikupata jibu lolote.

Sasa kwa kuwa ni awamu yako wewe Mhe. Waziri hivi sasa ningeomba kwamba suala la Mkia wa Ng'ombe ulipe kipaumbele ni kwa sababu watu wako mbali na mji na wanahitaji, watu hawa wakiweza kupata umeme japo kuwa wa *solar* mambo mawili yatasaidia. Kwanza umeme huu utakaopatikana wa *solar* utaweza kusaidia maendeleo ya hospitali, kwa sababu hospitali inahitaji kupata umeme, sasa kama umeme wa *solar* utaweza kupatikana mambo ya hospitali yatakuwa ni mazuri pili wananchi wataweza kufaidika na umeme ule, kwa vile imekuwa ni gharama kubwa umeme kuutoa kule na kuuleta pale ule wa kawaida. Kwa hivyo ningekuomba Mhe. Waziri mara hii uweze kulifuatilia hilo suala angalau kuweza kupata uwo umeme wa *solar*. Mhe. Spika, suala hili ambalo namueleza Mhe. Waziri ni suala muhimu na alitie maanani ili wananchi wale waweze kufaidika.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka kulizungumza ni suala la umeme hapa Zanzibar, kwa kweli hili suala mara hii limerudi kuliko ile mara iliyopita kipindi kile kilichopita ilikuwa umeme unakwenda vizuri, lakini katika kipindi hiki cha awamu hii umeme unakwenda vibaha hapa mjini Zanzibar, yaani kila wakati umeme unazimwa na usiku unazimwa kwa masaa mengi kwa sisi ambao tuna kazi tunataka kusoma hatupati nafasi ya kufanya kazi zetu vizuri. Pili kuna wale watu ambao wanautumia umeme ule kwa shughuli zao za kibiashara kwenye sehemu za viwanda, sehemu za seremala na sehemu ndogo ndogo ambazo kuna *work shop* hawa waatu wanakosa kupata mafao ya umeme, wanahitaji umeme kwa kuleta maendeleo wapate matumizi ili shughuli za kimaisha ziweze kuendelea.

Kwa hivyo mimi sielewi kwa nini wala hatujapewa taarifa kwa nini huu umeme unakatika katika na kwa nini iwe hivyo, suala hili la umeme hapa Zanzibar

linaleta mdajala mkubwa sana kipindi kilichopita tumejaribu kushauri serikali kwamba Zanzibar kwa umeme wa kutegemea hili litakuwa ni suala gumu kwa watu wa Zanzibar, kwa hivyo na mimi nasema hili suala ni gumu kwa kutegemea umeme kutoka nje kwa Zanzibar kama tukiweza wenyewe kupata umeme mbadala ingekuwa jambo la habari. Inaonyesha kwamba hapa Zanzibar umeme ni ghali sana.

Kwa hivyo nafikiri tukipata huu umeme wetu mbadala hapa tunajua ni mbinu chungu nzima za kuweza kupata umeme kwa njia ya upepo , kwa njia ya *solar* kwa njia ya jenereta na kwa njia ya kutumia mawimbi ya bahari, kwa hivyo mimi ningemshauri Mhe. Waziri hili suala sio la leo wala sio la jana limezungumzwa muda mrefu kwa nini Wizara ina gati gati kwenye suala hili kwani kuna ugumu gani na hatutaki kufanya sisi wafadhili tunao na wahisani tunao, tunaweza kwenda kuzungumza nao tufikie muafaka ili na sisi tukapata umeme ambao utakuwa wa uhakika hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri nafikiri hilo suala mara hii labda utakapokuja utatuelelezea hali ya umeme Zanzibar ulivyo hivi sasa na nini tutafanya kwa hii hali ambayo tunayo hivi sasa, mimi nina wasi wasi siku hadi siku zitakazoendelea huenda umeme Zanzibar ukawa katika hali mbaya sana. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri achukue hizi hatua za kuweza kutafuta watu wa kuweza kutusaidia katika suala hili.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka kulizungumza ni juu ya suala la Mahakama ya Ardhi, suala la Mahakama ya Ardhi linaleta mgogoro mkubwa sana mgogoro wa ardhi kwa upande wangu mimi ni kubwa katika jimbo langu unajua mimi nina sehemu za wawekezaji wengi sana, niseme kweli nakosa umeme mkazi wa kule naelewa ni kwamba maeneo ya Makangale sio maeneo ya watu ambao wanaishi hivi sasa walioko, maeneo yale ya Makangale ni maeneo ya watu wa Msuka ndio wenye mashamba ya kule. Lakini kwa bahati mbaya unajua watu sisi ni makarimu sana anapokuja mgeni tunamwambia kaa na ishi kule kuishi watu wengine katika mashamba waliyonayo wengine wanakuwa wanazo karatasi zao za kuonyesha mashamba yao, lakini wengine ni mashamba ya kurithi ambao hawana nyaraka na hawajatengeneza nyaraka zile.

Kwa hivyo wakati wa kuchukuliwa mashamba yale na watu wengine wenye akili wanayachukua na wanakwenda kesi na matokeo yake mashamba yale wananyang'anywa, sasa katika mgogoro mmoja katika jimbo la Konde mgogoro mkubwa ni wa ardhi ambao mashamba ni ya watu wa Msuka lakini yanachukuliwa na wale watu wanaokaa katika maeneo yale, yanakwenda kesi kesi inamalizika watu wa Msuka wanakosa mashamba yao.

Kwa hivyo ningelimuomba Mhe. Waziri kwenye suala hili akajaribu kufuatilia juu ya mashamba haya ya watu wa Makangale ambao ni mashamba ya watu wa Msuka, kwa hivyo hili alione Mhe. Waziri.

Lakini jengine katika suala zima la Mahakama ya Ardhi mimi niseme tu katika Mahakama ya Ardhi kuna mambo kadha wa kadhaa ambayo yanajitokeza, kwanza kuna ucheleweshaji wa kesi, pili kuna hawa watu ambao tunawaita washauri wa Mahakama hawa wapo pamoja na Hakimu kuendeleza kesi za mambo ya ardhi. Lakini nataka niseme tu kwamba watu hawa ambao wanashirikiana na Hakimu kiuhalali kabisa, kwanza ni watu ambao wanatoka maeneo ya mbali sana wanatakiwa wafike kama Chake Chake au Wete, baadhi ya wakati watu hao wanachelewa kufika katika makazi yao na kila wakichelewa na zile kesi zinakuwa zinachelewa huo ni mmoja katika usumbufu.

Lakini la pili watu hawa sijui Wizara yako itasema nini lakini hawa watu ambao ni washauri wa mahakama hawapewi mshahara badala yake wanapewa posho, nilitaka nimuulize tu Mhe. Waziri hivyo ndio ilivyopangiwa kwamba wapewe posho au wapewe mshahara, naomba wakati wa majumuisho aje kutwambia aa hawa wanastahiki kupewa posho. Lakini la pili katika hili posho niseme kwamba hili posho wanalolipwa hawalipati kwa wakati posho linachelewa na wao wanatakiwa kufika kazini, kwa hivyo ningelimuomba vile vile Mhe. Waziri atakapokuja hapa atwambie kwamba nakuhakikishieni posho zao zitapatikana kwa wakati.

Lakini kubwa zaidi katika yote hayo ni kwamba wakati wa maamuzi hili ni jambo muhimu na hili ni suala la makubaliano baina ya washauri wa Mahakama na Hakimu, wakati wa maamuzi ya mwisho ya kesi wanatakiwa washauri wote wawepo ili ile kesi iweze kuamuliwa na wao wakiwepo suala hili halipo. Hakimu anaendelea kuamua kesi bila ya kuwa na washauri wake hili limelalamikiwa kwa hivyo hili ni lalamiko Mhe. Waziri nakupa uliwelewe na ulifanyie kazi.

Mhe. Spika, niendelee katika suala jengine ambalo huenda labda likawa la mwisho ni suala la uchimbaji wa mafuta, suala la mafuta ni rasilimali ya taifa, mafuta ni rasilimali ya wananchi, mafuta ni rasilimali ya Wazanzibari ni haki yetu kuyachimba haya mafuta, kwa sababu Mwenyezi Mungu ametupa ni yetu wenyewe sioni sababu kwa nini tubishane katika suala hili. Hakuna la kustaajabu katika suala hili, hakuna la kusita sita katika suala hili wala hakuna sababu za woga katika suala hili, lakini hapa inaonyesha kwamba suala hili ndani yake kumeingia woga sijui kwa nini.

Mhe. Spika, Zanzibar ni nchi kamili ina rais wake, Zanzibar ina baraza lake la kutunga sheria ndio tumo humu ndani na hili baraza ni baraza la wananchi na wananchi ni baraza lao hili, haya ni ya wananchi wanatutuma sisi kwa suala hili. Wananchi wanatuuliza suala hili mpaka sasa hivi likoje mbona lina gati gati, kwa hivyo Zanzibar ni mamlaka kamili na kama ni mamlaka kamili ningeliomba Mhe. Waziri hili suala asilifumbie macho hii ni haki yetu na rasilimali yetu tuchimbe.

Lakini mimi niseme tu kama tukifikiria sisi Wazanzibari kwamba kukua kwa uchumi wan chi hii bado hakujaweza kutafsiriwa katika kukua kwa bidhaa au biashara ndogo ndogo, hizi biashara ambazo tunazifanya Zanzibar ndio zitatupa haki kamili kuwa sisi tuna uchumi Zanzibar bado hatujafikia katika kiwango kwamba tukifikiria kwamba hii biashara tuliyokuwa nayo ndio uchumi mkubwa sana, au kilimo tulichokuwa nacho ndio uchumi hatujafikia katika hicho kiwango cha uchumi. Ili na wananchi wa kawaida waweze kunufaika kutokana na kukua kwa uchumi huo, kama tunafikiria uchumi huu tuliokuwa nao bado uchumi huu kwa miaka mpaka hii ya leo uchumi huu haujaweza kufikia kwamba Wazanzibari wana uchumi. Mimi nasema uchumi haupo iliyobakia ni biashara za kusaidiana hapa na pale pato la nchi hii *Revenue* inayopatikana madukhuli yanayopatikana katika nchi hii ni madukhuli ya mshahara na maposho tu lakini sio la maendeleo, kwa hivyo bado tunasema tuna kazi kubwa ya kupata uchumi, kwa hivyo tunachokitegemea kwa kuwa madukhuli yetu ni madogo na biashara zetu n indigo basi madukhuli tunayo lakini tumeyakalia. Mhe. Spika, hakuna zaidi isipokuwa mafuta Mhe. Waziri.

Mimi ninasema kama kuna kigugumizi kwenye suala hili Waziri tunasema hicho kigugumizi ukiondoe wananchi tuko pamoja na wewe, sisi kwa suala hili baraza zima liko pamoja na wewe na wananchi woe wako pamoja na wewe. Kwa hivyo tunakuomba tegemeo la wananchi wa nchi hii ni mafuta, waheshimiwa mimi nasema suala la mafuta na gesi asilia haidhuru iko katika katiba ya Zanzibar na Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Lakini kwa nini wenzetu wakawa wanafanya mambo kinyume ya haya kwa sababu ikiwe ni gesi basi Songosongo tayari iko kule zaidi ya miaka mitatu, mbona sisi Wazanzibari hatupati fedha ile iko wapi fedha ya Songosongo ya gesi.

Hivi sasa kwa taarifa yake watu wanaendelea kuchimba mafuta au kufanya utafiti na mambo kama yalivyozungumzwa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu mambo yako tayari mameli yameshafika, sisi tumelala doro tunamngojea mtu kumshauri sasa nani wa kumshauri, hakuna wa kumshauri tena tufanye hii shughuli.

Mimi sasa ninalomuomba Mhe. Waziri sisi hatungojei idhini hatuposi mke hapa, tukaambiwa tutafute idhini ya kuoa, rasilimali ni yetu wenyewe

tuyachimbe. Kwa hivyo tunachokusubiri Mhe. Waziri tunakuomba kwa hisani yako bajeti yako inamalizika kesho au keshokutwa tunataka jibu, kesho au leo wakati wa *samary* tunataka jibu sheria hii tuletee hapa na utwambie sheria utatuletea lini ya mafuta tumalize kazi. Sera tumemaliza kila kitu tumemaliza mambo yote tumeshazungumza kipindi kilichopita huu woga woga wa nini tena.

Kwa hivyo Mhe. Waziri tunakuomba utuletee sheria kwa haraka ili tuweze kuifanyia kazi, kwa hayo machache Mhe. Spika, nakuomba na nakushukuru na mimi naunga mkono hoja mia juu ya mia ahsate sana. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi jioni hii ili niweze kutoa mchango wangu mfupi kwenye hotuba hii muhimu sana ya Mhe. Waziri wa Maji, kwanza nianze kutangulia nisije nikasahau pamoja na maelezo yangu nitakayozungumza lakini siungi mkono hoja, mpaka pale ambapo nitapata majibu yatakayoniridhisha nimeona niseme mwanzo hiyo nisije kusahau, sitounga mkono hoja kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani mpaka nipate majibu ambayo wananchi wangu elfu kumi na sita wataridhika kwa niaba yao.

Mhe. Spika, kwanza niseme tu kwamba shirika la umeme wameendelea kusambaza umeme Unguja na Pemba tangu zamani mpaka *fase for* chini ya Mhe. Mansour aliyepita ambapo umeme huu Zanzibar na Pemba wamefaidika wananchi wetu kwa kiasi kikubwa, lakini sambamba na hilo Wazanzibari wamekuwa msitari wa mbele kwa msaada wa wawakilishi na wabunge wao kutafuta nguzo kwa juhudi ya kusaidia juhudi za serikali. Lakini kwa bahati mbaya Mhe. Spika, shirika la umeme bado linashindwa kuwasaidia suala la waya wananchi wale ili liishe suala la umeme.

Kwa hivyo Mhe. Spika, ninachomuomba Mhe. Waziri tu nimkumbushe kwamba wananchi wa Msengele pamoja na serikali yetu ya Zanzibar kupitia shirika la umeme wameekeza suala la umeme kule Msengele hadi hii leo halijamalizika, naomba Mhe. Waziri labda anieleze lini suala hili litamalizika kwa sababu limeanza kwa kasi lakini limevia kwa muda mfupi hivi sasa.

Mhe. Spika, jengine ZECO wametupatia majanareta 32 ambayo tulitegemea kwamba yatafanya kazi kubwa ya umeme hapa Zanzibar, lakini taarifa ambazo tunazo kwamba majanareta yale yanashindwa kufanya kazi kwa sababu serikali imeshindwa kulipia huduma ya umeme. Sasa serikali ya awamu ya saba imeamua kwamba isilipie malipo ya umeme ndani ya ZECO na hiyo imekuwa sababu tosha ya kuwa majenareta yale hayawezi kununuliwa mafuta. Sasa naomba kupata ufafanuzi wa Waziri kwamba Je, serikali ya awamu ya sita ilikuwa inalipia kwa kila taasisi je serikali ya awamu ya saba sasa wameamua

umeme wasilipie watumie nguvu za mtoto wao, kama hivyo ndivyo namuomba Mhe. Waziri anitolee ufafanuzi ili niweze kujua.

Mhe. Spika, kwa upande wa mamlaka ya maji ZAWA mimi nipongeze tu kwa upande wa jimbo langu na hasa pale nilipoona kuwa wameamua kusambaza maji kwa upande wa Mwambe ambao hadi hii leo haujapata maji, lakini pamoja na juhudi hizo niwakumbushe tu kwamba Zanzibar bado ina shida ya maji na hapa Mjini Unguja wananchi wanasumbuka sana naomba wajipange zaidi ili waendelee kusaidia wananchi kwa ajili ya kuondosha tatizo la maji.

Mhe. Spika, sasa niende moja kwa moja kwa ufupi sana kwenye suala la mafuta ambalo sitofanya haki kama sitochangia hata kidogo pamoja na michango mizuri sana ya wenazangu waliyozungumza, mimi niseme tu kwamba Mhe. Ismail Jussa Ladhu amekuwa mtafiti sana kadiri ninavyojipanga kuja kutoa mchango wangu mwenzangu amenizidi, lakini nathubutu kusema kwamba suala la mafuta tayari limezungumzwa na halipaswi tena kujadiliwa kwa mujibu wa maamuzi ya Baraza la Wawakilishi na sera tayari imeletwa hapa na tumeipitisha. Mhe. Waziri nakumbuka mwazi wa April, 2010 alituletea taarifa kwamba sheria ya mafuta itapitishwa wakati wowote. Taarifa ninazo na Mhe. Ismail Jussa bahati nzuri asubuhi ametuambia kwamba sheria wataalamu wametayari, lakini ilikwama katika ngazi za makatibu wakuu na kwa maana hiyo haikwenda Baraza la Mapinduzi.

Kwa hivyo, tunaomba tujui kwa nini sheria ilitayarishwa, wataalamu walikaa Bwawani zaidi ya wiki nzima na taarifa hizo ninazo, sheria wakaiandika lakini kwa Makatibu Wakuu pale ilikwama haikupelekwa Baraza la Mapinduzi. Sheria hii kwa nini ilikwama katika ngazi ile na kwa nini hadi hii leo kauli ya serikali haikutimia.

Mhe. Spika, kama hilo halitoshi. Nimebahatika kuangalia katika mtandano nikaona picha ya Mhe. Ali Juma Shamuhuna, Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati pamoja na Mfalme wa Ras-el-Khaima na Katibu Mkuu wa wizara hii. Mhe. Spika, naomba nikuoneshe hii picha (kaipeleka picha kwa Mhe. Spika).

Mhe. Spika, nilitegemea kwamba amekwenda Ras-el-Khaima angekuja na jibu la mafuta kuwa ni lini wamekubaliana. Lakini yale ambayo tumezungumza kwamba labda viongozi wetu wanakwenda kutembea kwa mazungumzo mengine. Mzanzibar mimi binafsi nilitegemea kuwa picha hii. Juzi alikuja mzungu hapo juu na tulimuona na leo humu yumo, nilitegemea kuwa angekuja na jibu la kuwa nini walichokizungumza Ras-el-Khaima kwa niaba ya Wazanzibar juu ya mafuta. Lakini kila tunapokiangalia kitabu hiki Mhe. Spika, hatukuona mafanikio ya wazi aliyoeleza Mhe. Waziri kulingana na picha hii ya

mtandao ambayo ni picha yake halisi na Katibu Mkuu wake pamoja na Mfalme wa Ras-el-Khaima.

Mhe. Spika, Wazanzibari wanataka wajuwe. Mimi nataka niwaambie wajumbe wenzangu kwamba mimi siamini sana kama tatizo ni Muungano. Inawezekana Wazanzibari tunawalaumu wenzetu wa Bara kumbe hawana tatizo. Kwa mawazo yangu tatizo ni sisi. Haiwezekani kwamba wenzetu tunawalaumu na tunawatukana lakini wako kimya, inawezekana sisi ni tatizo na kwa vile wamejua kwamba wale ni tatizo lao wenyewe. Kwa hivyo, tatizo ni sisi wenyewe.

Mhe. Spika, kuchimba mafuta ni muda mrefu wa miaka 10, lakini kusomesha wanafunzi ni jambo la kawaida. Mhe. Spika, mwaka juzi hapa tumesema kwamba TBC isitie mkono wake Zanzibar, nakumbuka na Hansard ipo. Wapo wajumbe waliosema kwamba hata Katibu Mkuu aondoke katika bodi ya TBC, lakini hadi hii leo anakwenda. Lakini kumpeleka mfanyakazi wa Idara Nishati ni kosa maana yake T tusishirikiane, lakini kumbakisha Katibu Mkuu kuwa member wa TBC ni halali. Ndio Mhe. Assa Othman Hamad anasema unakataa nyama lakini mchuzi unaupenda.

Mhe. Spika, tatizo ni sisi. Haiwezekani kwamba sheria imetungwa serikali imeharamika na sheria Barazani haikuletwa. Inawezekana suala hili ni ajenda ya watu Fulani na hawataki kutukwamua. Tafadhalini tusaidieni, kama tatizo lipo Mhe. Spika, Mhe. Waziri tuambie leo tatizo ni nini.

Kwa hivyo, wenzetu kule wakienda Korea wakizindua meli tusiwalaumu, wao wana haja ya fedha na sisi tunahaja ya maneno, sasa ikiwa maneno tumeishiwa basi tusemeni. Kama maneno ndio mtaji wetu tusemeni, lakini mimi naamini tatizo sio Muungano ni sisi. Siku ambayo Mhe. Spika, Wazanzibari wataamua basi hili jambo ni la dakika mbili tu. inawezekana pia tatizo sio mawaziri ni wawakilishi. kwa nini mwanadamu anatakiwa atembee juu ya maneno yake.

Mhe. Spika mwaka juzi tuliamua na wenzetu hawatekelezi bado tunawachekelea, tatizo ni wao au ni sisi, ni sisi. Mtoto akichezea kiwembe ukimwachia basi kosa ni lako wewe mzee. Sasa ikiwa serikali haitekelezi wawakilishi waamuwe kuwatekelezesha kwa nguvu. Lakini tunazungumza maneno mengi hapa, kuwa hataki mawaziri, ni sisi wawakilishi hatujaamua. Dakika moja tu tukiamua watatekeleza hawa, lakini maneno mengi ya bure, natuamuwe watekeleze *Wallah* kesho tu atatekeleza Mhe. Shamumuna kesho tu. Lakini kwa maneno ya kuzungumza tukacheka tu basi hatekelezi kweli, kwani anashida gani.

Mhe. Spika, nawaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu, kama tumeapa kwa kutumia msahafu wa Mwenyezi Mungu na kama tunaamini kuwa kuna siku tutakufa, basi tuwafanyie haki Wazanzibari. Kuna mtaalamu mmoja juzi ameniambia nyinyi mnazungumzia rushwa, watu wanaiba serikalini na nyinyi kwani wawakilishi hamuibi. Nikamwambia sisi hatuibi, akaniambia mnaiba. Akaniambia mnachukua posho hamuwatendei watu si wizi huo. Ni kweli tunachukua posho lakini watu hatuwatetei, kwa nini kwa sababu rafiki yangu asijekunilaumu.

Mhe. Spika, mimi Hija Hassan Hija pamoja na unyonge wangu niko tayari nisiiunge mkono hotuba hii peke yangu mpaka nipate jibu la Mhe. Waziri. Mimi nina watu 18,000 wanyonge sana wamenituma nije kufanyakazi hii, sikuja hapa kumlaumu mtu wala kumpendelea mtu, nipo kwenye kazi yangu niliyotumwa.

Kwa hivyo, Mhe.Spika, Mhe. Waziri nipe jibu, hakuna jibu peke yangu nitaikataa bajeti hii na wala sioni aibu, kwa nini kwa sababu sioni sababu ya kuhangaishana miaka mitatu kwa jambo dogo tu. Mhe. Waziri nakuomba sana tupe jibu la mafuta na najua utatuambia subirini keshokutwa ndio lugha zetu, lakini tuambie lini sheria hii itakuja Barazani na kwa vile tayari imeshatayarishwa kwa fedha za umma na wataamu wapo wameandika sheria na ninayo kopi hapa, lakini mmeshindwa kuileta Barazani kwa nini.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi binafsi kama hakuniambia lini sheria hiyo italetwa hapa Barazani tukaipitisha, basi sina haja ya kuunga mkono na nitaona fahari kubwa peke yangu kuilikataa jambo hili.

Jengine Mhe. Spika, ambalo nataka niliseme ni kuhusu migogoro ya ardhi. Mhe. Spika, Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar ninazo barua za Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi, alikiri kwamba wananchi wa Mtoni walivunjiwa nyumba kinyume na makosa. Wakashauriwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itawasaidia, haiwalipi lakini itawasaidia fidia kidogo. Mhe. Spika, hayo ni maamuzi ya serikali, Baraza la Mapinduzi maana yake ni serikali. Ninachowaomba Mhe. Spika, wananchi wale wasaidieni. Wasaidieni kwa sababu serikali iliahidi kwamba nyumba zimevunjwa kwa makosa na wako tayari kuwasaidia. Kwa hivyo, Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wananchi wale wa Mtoni wasaidieni nyumba zile hata kwa kuwapa viwanja, ili wapate hifadhi ya maisha yao na watoto wao.

Mhe. Spika, jengine ni suala zima la uvamizi wa ardhi ambalo hili nataka nimese kuwa Mhe. Spika, kwa mtazamo wangu kama Zanzibar kuna ufisadi mkubwa basi utakuwa ni ufisadi wa ardhi. Mimi sikubaliani na ile hoja kwamba aliyeligema alinywe, nani anayeiba akakubali kujihukumu. Hivi mimi

niibe halafu nijihukumu mimi. Kama nadharia aliyeiba ndie ajihukumu mimi sikubaliani nayo. Kwa hii wananchi ndio watuhumiwa na msimamizi wa serikali ni Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, migogoro ya ardhi ni mingi sana kwa Unguja na Pemba, na yote hayo ni kesi za ardhi watu wanalalamika kwa ushahidi wanaonewa na serikali. Kwa nini ikawa ni serikali, kwa sababu serikali inatoa vibali baadae wanafuta bila ya kuwa na utaratibu wa kisheria. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ushauri wangu ni kwamba kwa sababu serikali haiwezi kuvisimamia, Mhe. Waziri unikubalie kuwa tuunde tume ili tukusanye matatizo ya ardhi kwa Unguja na Pemba baadae tuwashauri, nyinyi hamuwezi kuyashughulikia kwa sababu walioharibu ni serikali wenyewe.

Mhe. Spika, nina barua hapa ya Mhe. Waziri ambayo alifuta ardhi bahati ni yeye mwenyewe na saini yake na jina lake. Mhe. Spika, sheria ya ardhi nambari 12 ya mwaka 1992 inasema kwamba ardhi itafutwa na kibali kitaondoshwa baada ya muomba kibali kuwa ameshindwa masharti ndani ya miaka 30. Lakini kwa mujibu wa tarehe ya *land lies* ambayo mmeitoa nyinyi wenyewe serikali, mmefuta kibali miezi 17 sababu hatuzijui na bahati mbaya amelipia dola 39,000, pesa imechukuliwa baadae ikafutiwa. Hatuwezi kuvumilia mchezo huo.

Mhe. Spika, mimi namshauri Mhe. Waziri unikubalie kaka yangu, mzee wangu kwamba tuunde tume tuwasaidie. Zanzibar kuna ufisadi mkubwa wa ardhi wananchi wanaonewa tofauti kabisa na wale wa Mapinduzi. Mzee Karume yeye katoa eka tatu, mimi baba yangu ana eka tatu. Sasa viongozi wa sasa wanawanyang'anya wananchi ardhi, Karume yeye aliwapa wananchi ardhi tofauti kabisa na malengo ya Mapinduzi. Sasa ikiwa tuna enzi malengo ya Mapinduzi basi ni lazima ardhi ya wananchi iheshimiwe.

Mhe. Spika, haiwezekani kabisa kwamba wananchi wanyonge kila siku wana lalamika. Malalamiko yote haya ni kutoka Kusini Unguja, Kaskazini Unguja, Kusini Pemba watu wanaonewa

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, dakika tano bado.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, zinatosha sana hizo. Watu wanaonewa chini ya serikali hii wawakilishi tupo na mawaziri wapo. Mhe. Spika, kwa heshima kubwa sana Mhe. Waziri ni mtu makini sana, naomba tukusaidie. Tukusaidie kwa kuunda tume ya kutafuta matatizo ya ardhi tukuletee, huwezi ukamtuma Mkurugenzi wako aliyeharibu halafu akuletee taarifa haiwezekani. Lakini ukimtuma mwengine aliyekuwa siye aliyeharibu basi atakuletea taarifa sahihi na utaifanyia kazi.

Mhe. Spika, kwa msingi huo, nakumbusha kwamba Wazanzibari wote ni milioni 1,200,000 wako chini yetu, sisi ndio dhamana na sisi ndio ambao tutawazamisha au tutawavua. Mimi binafsi Mhe. Spika, siko tayari kuwazika Wazanzibari na kwa msingi huo ikiwa serikali inashindwa kuwasimamia wananchi kwa kuoneana haya basi na wajiuzulu. Kama serikali inamuonea mtu haya kwa maslahi ya watu basi kiongozi huyo hafai na bora aachie ngazi. Tuko wengi hapa na kila mtu anataka uwaziri hapa, ikiwa wewe unashindwa kuwafanyia haki wananchi, basi mpeni Mhe. Hamza na Mhe. Hija tutawafanyia kazi wananchi.

Mhe. Spika, haitokuwa busara kabisa ikiwa kila siku maneno haya yanaendelea na watu wanaonewa tunacheka tu kwa sababu watu 80 sisi tunapata mafuta ya gari, haiwezekani sio haki. Mhe. Spika, tunajua kila mmoja ni mchunga na mbele ya Mwenyezi Mungu kila mmoja ataulizwa kile alichokichunga.

Mhe. Spika, kwa niaba yangu pamoja na wananchi wa Jimbo la Kiwani, siungi mkono hoja mpaka nipate ufafanuzi wa mafuta na tume ya ardhi kwa ajili ya kuwasaidia Wazanzibari, ahsante sana.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri. Kwanza kabisa nampongeza Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa ujumla.

Mhe. Spika, tatizo la maji Zanzibar bado linaendelea. Katika kijiji changu cha Kiuyu Minungwini tatizo la maji bado lipo. Kiuyu Minungwini ina shehia mbili. Shehia ya Kiuyu Minungwini na Shehia ya Kiuyu Kigongoni. Wana kijiji wa Shehia ya Kiuyu Kigongoni bado wanasumbuka kwa tatizo la maji. Mhe. Spika, wana kijiji wa Kiuyu Kigongoni wanapata maji usiku hadi usiku, tatizo hili linaendelea karibuni miaka mitatu. Baada yakufuatilia tuligundua mashine iliyoko pale Kiuyu Petewani haikidhi haja kwa wanakijiji wote wa Kiuyu Minungwini. Mashine ile ni ndogo haiwezi ikawaenezea maji wana kijiji wote wa Kiuyu Minungwini. Mradi wa maji ulipo Kiuyu Petewani ulipatikana pale kwa mradi wa TASAF ambao ndio uliosababisha tukapata mashine ile iliyokuwa ni ndogo. Mhe. Spika, naomuomba Mhe. Waziri alitatuwe suala hili kwa kuweza kuwatafutia mashine ambayo itaweza kukidhi haja kwa Kiuyu nzima.

Mhe. Spika, niende kwenye suala la mafuta. Suala hili ni zuri sana, namuomba Mhe. Waziri Mwenyezi Mungu amjaalie ampe nguvu, hekima na busara ili aweze kuondoa tatizo hili Zanzibar. Vijana wengi wa Zanzibar hawana ajira, wamebakia wanazurura ovyo, mara utasikia huyu kabaka na huyu kafanya hivi. Mhe. Spika, tatizo hili ni ukosefu wa ajira Zanzibar, kama ingekuwa vijana

wengi wa Zanzibar wana ajira basi wasingebaka wangekuwa wanaoa tu kutokana na uwezo wao wa ajira.

Mhe. Spika, mimi sina mengi isipokuwa kwa niaba ya vijana wenzangu wa Zanzibar naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Spika, kwanza niende moja kwa moja kwenye mahakama ya ardhi kwenye ukurasa wa 17. Mhe. Spika, mahakama ya ardhi kuna mrundikano wa kesi jambo ambalo linaleta usumbufu kwa wananchi wetu, imekuwani kero kubwa sana kutokana na mrundikano wa kesi unaoendelea siku hadi siku, hili ni tatizo kubwa. Tunamuomba Mhe. Waziri afanye kila hali jambo hili alipatie ufumbuzi.

Mhe. Spika, katika mahakama ya ardhi Pemba wana usumbufu wa usafiri hawana gari Pemba, gari lao ni bovu na liko pale Mkoani limelala tu halina kazi yoyote. Kwa vile ni mahakama ya ardhi na wakati mwengine wanataka kuendelea kwenda kuangalia sehemu zenye matukio ya migogoro ya ardhi basi hawana usafiri. Kwa hivyo, Mhe. Waziri waangalie kwa jicho la huruma gari lao ni bovu limelala pale Mkoani halina kazi yoyote.

Mhe. Spika, wazee wa Baraza hawa hapa, wana hali ngumu na wana malalamiko makubwa sana dhidi ya posho wanalopata ni dogo sana halikidhi mahitaji. Kwa hivyo, wazee wanapokuja katika sehemu zao za mahakama wanatoka sehemu mbali basi ukipanga nauli yao na posho wanalopata ni tatizo kwao halikidhi haja. Vile vile hilo posho wanalopata hawalipati kwa muda muafaka linachelewa sana. Tunakuomba Mhe. Waziri uwaangalie wazee hawa kwa jicho la huruma.

Mhe. Spika, nikiendelea katika sehemu hii kuna nyumba za maendeleo. Mimi nikiwa mwana Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi tulifika kule Kengeja, hali ya nyumba za Kengeja ni mbaya sana, wananchi wanaoishi pale wanaishi kwa hofu sana. Kwa hivyo tunaomba nyumba zile zifanyiwe matengenezo haraka sana, kama hakuna uwezo basi wafanyieni bidii wale watu muwahamishe pale yasije yakatokea mengine baadae.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nije moja kwa moja kwanye Mamlaka ya Maji kwenye ukurasa wa 48. kwa kweli hapa nitowe pongezi kweli kwali katika watu waliokuwa na shida ya maji salama na safi ni Jimbo la Kojani. Lakini tunamshukuru Mwenyezi Mungu Kojani ni kisiwa na maji yamepita chini ya

bahari na wananchi wa Kojani wanafaidika, lakini pamoja na kufaidika kwao kuna matatizo. Kijiji cha Kojani sio kidogo, kijiji hiki kinaishi watu zadii ya 10,000, lakini kuna mitaa mingine maji hayafiki ikiwemo sehemu za Ngazini, Kukiani, Binti Mkongwe na sehemu nyengine maji hayafiki kabisa. Halafu jambo la kusikitisha kabisa ni hawa watoaji maji wanatutolea maji saa saba za usiku kinyume na utaratibu, mtu saa za mapumziko, saa za kuzaa ndio wanatoa maji, hilo haliwezekani kabisa. Nakuomba Mhe. Waziri nikimaliza kuchangia tu basi nione mabadiliko makubwa ndani ya Jimbo langu kisiwani Kojani.

Mhe. Spika, tukiendelea na sehemu hiyo hiyo ya maji, kuna kijiji kimoja ndani ya jimbo la kinaitwa Jitenge. Watu wa Jitenge hawajapata maji safi na salama tena wenyewe wanasema kwamba tumewatenga sana ni jitenge kweli kweli. Kwa hivyo, naomba katika bajeti hii wasitengwe wapate maji safi na salama, kijiji hiki jitenge sehemu za maziwani Mhe. Waziri naomba kifikiriwe katika bajeti hii ili kipate maji safi na salama.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu, tunaipongeza Mamla ya Maji lakini ndani ya Jimbo la Kojani bado kuna matatizo wale watu wa mwani pale wana tatizo la maji. Mhe. Waziri naomba uwatizame kwa jicho la huruma watu wa mwani pamoja na sehemu za Masota pale.
Mhe. Spika, nikitoka hapo nije moja kwa moja kwenye Shirika la Umeme (ZECO). Mhe. Spika, katika Shirika la Umeme nilikuwa mwanakamati, lakini kutokana na hali ngumu ya wananchi wetu basi hata kama kujipendekeza kwa wananchi wapewe umeme kwa ajili ya kukopeshana kwa njia ya mkataba na Shirika hilo la Umeme ili wapate huduma hii muhimu. Ukiangalia tunapata umeme kutoka Tanga *megawatt* 20, lakini zinazotumika ni megawatt 6 tu, kwa hivyo inaonekana hata hatuutumii umeme. Kwa hivyo, wananchi hawana uwezo kabisa kwa sababu gharama ni kubwa sana. Mhe. Waziri tunaomba ulifikirie suala hii ili na wananchi wakopeshwe umeme.

Mhe. Spika, serikali siku zote huwa pamoja na wananchi wanaotumia nguvu zao na kukusanya pesa zao kwa ajili ya shughuli za maendeleo, hapo serikali huwa karibu kuwasaidia. Lakini tunashangazwa wananchi wa Mwane wana nguzo zao za umeme, wananchi wa Shengejuu wana nguzo zao za umeme, wananchi wa Kivugo wana nguzo zao za umeme, lakini nguzo zile zitakuwa mali ya baghili zitaliwa na mdudu na tayari wanaanza kuzishambulia. Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Waziri nguzo zile zisimamishwe ili muwasaidie wananchi kuwasogezea umeme ndani ya Jimbo la Kojani. Vile vile kisiwani Kojani kule katika Mji Mpya wa Makaani kule watu vile vile hawana uwezo, tunaomba uwasogezee umeme. Mwenye nguvu atavuta lakini uwasogezee kwa sababu ni masafa, Mhe. Waziri lifikirie sana hili suala.

Suala jengine Mhe. Spika, ni Idara ya Nishati na Madini, hapa katika mafuta. Nawaambieni Zanzibar ni nchi kama nchi nyengine na ipo kwa mujibu wa kuwatumikia wananchi. Ili tuwe na Rais mzuri, tuwe na Makamo wa Kwanza wa Rais mzuri na Makamo wa Pili wa Rais mzuri na tuwe na wawakilishi wazuri basi ni lazima tuwajibike Wazanzibari katika kuitetea Zanzibar. Kwa sababu gani nikasema hivyo, kwa sababu Zanzibar ni nchi na nchi ni yenye maamuzi bila ya maamuzi huwezi kufikia malengo, tufike mahali na sisi tuamuwe. Kwa sababu jambo hili limechangiwa sana naomba katika kipindi cha miaka hii mitano tuliyonayo basi mafuta yachimbwe Zanzibar ili wananchi wetu wafaidike na waweze kupata ajira.

Mhe. Spika, hakuna sababu za kukawisha tena kwa sababu hili jambo limeshapita, mimi nataka tuangalie hizi kero tunakerwa sisi Wazanzibari tu, mbona watu wa Bara hawalalamiki, tunaolalamika ni Wazanzibari tu kwa nini watu wa Bara hawalalamiki. Kwa hivyo kama ni kero na sisi tutafuteni kero tuwakere na wao walalamike, lakini jambo hili tufanikishe.

Mhe. Spika, kwa hayo machache mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kojani, naunga mkono hoja mia juu ya mia, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mlinde Mabrouk Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi jioni hii kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia angalau kidogo hotuba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Spika, mimi napenda nizungumzie mambo ambayo yako katika jimbo langu la Bumbwini. Mhe. Spika, katika Jimbo la Bumbwini, kidogo tuko tofauti na majimbo mengine, mimi katika jimbo langu kuna visima viwili vya maji. Kisima cha kwanza kiko sehemu ya Misufini baada ya kuona serikali kisima kile hakitoshelezi, iliamua kuchimba kisima chengine katika eneo la Makoba. *Alhamdulillah* tunashukuru katika kisima hicho cha Makoba kina maji ya kutosha tu. Lakini tunachoshangaa hasa wananchi wale wa Mangapwani na Zingwezingwe fursa hii hawaipati, lakini katika kisima cha Makoba kina maji ya kutosha.

Mhe. Spika, kwa makusudi watu wa ZAWA wamefunga *stopcock* pale ili maji yasiweze kuwafikia wale wananchi wa maeneo ya Zingwezingwe na Mangapwani. Mhe. Spika, mimi naomba nimuulize Mhe. Waziri hawa wananchi wana makosa gani na kwa nini katika nchi hii kuna sehemu maji yaende na kwengine yafungwe. Tunavyoelewa kisima kile ni cha serikali, kama ni cha serikali kwa nini sasa watoke wananchi washirikiane na watu wa ZAWA waweke *stopcock* pale ifungwe ili wananchi wakose maji. Mhe. Waziri utakapokuja hapa uniambie matatizo ya watu hawa, kwa nini maji yamefungwa

na mpaka leo watu wa Zingwezingwe mwaka wa nane sasa wanakosa huduma muhimu hii ya maji.

Mhe. Spika, nizungumzie tu kidogo suala la umeme. Katika Jimbo la Bumbwini nimeona hapa kuna mpango mzuri wa kuendeza umeme vijijini. Katika Jimbo la Bumbwini kuna maeneo kama Kiongwe na Pangatupu, maeneo haya hadi hivi sasa huduma hii ya umeme haijawafikia na kwa kweli kwa wananchi wenyewe hawatoweza kuuvuta, kwa sababu haya maeneo yako mbali na umeme ulipofikia. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri katika mpango wake huu wa kusambaza maji vijijini awamu hii inayofuata basi atuone na sisi wananchi wa Jimbo la Bumbwini kuwa vijiji hivi vinaweza kupatiwa huduma hii ya umeme haraka iwezekanavyo.

Labda kidogo Mhe. Spika, nigusie suala la Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO). Juzi nilikuwa naangalia kipindi kile cha ITV, wanakipindi kile cha nimekisau kidogo, lakini kulikuwa kuna viongozi fulani wanalikuwa wanajadili kuhusu jinsi Zanzibar tulivyokuwa tunadaiwa bilioni 50 na hadi hivi sasa hatujaweza kulipa, kiasi kwamba lile deni linatudhalilisha, tunaonekana kwamba umeme tunapewa bure na sisi wananchi wanakatiwa umeme majumbani, sasa tatizo liko wapi hapa. Kama Shirika la Umeme linashindwa kulipa umeme kule TANESCO, hizi pesa zinazokusanywa hapa zinakwenda wapi. Kwa kweli hii ni aibu kwa nchi bilioni 50 sio pesa kidogo. Kama hili suala sio kweli basi tuambiwe ili na sisi tupate kuridhika. Lakini kama suala lenyewe basi shirika hili kuna haja ya kuangaliwa upya, kwa sababu haiwezekani kufikia bill hii ya umeme ya shilingi bilioni 50/= na sisi wananchi wanyonge ndio tunaokatwa umeme pamoja na kodi tunalipa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia napenda kuzungumzia kuhusu suala la majanareta. Kwa kweli majanareta ya umeme tumeyashuhudia yamefungwa hii miaka ya karibuni, lakini bado hatujaona uzalishaji hasa unaotokana na majanareta yale. Hivi sasa kuna lugha wananchi wanazungumza kwamba yale majanareta kuna mambo ya kuchakachua, kwa sababu kuna majanareta kama manne tokea yamefika hadi hivi sasa hayajafanya kazi, kwamba ni mabovu.

Kwa hivyo, itakuwaje tukanunue majanareta mabovu, hivi tunapofanya manunuzi hatuangalii, kwa sababu hapa tunao wasomi ambao wamesomea masuala ya manunuzi, inakuwaje mpaka leo tunauziwa vitu vibovu. Mhe. Spika, naamini tunao *engineers* Zanzibar, hivyo ni vyema kupatiwa jawabu haya majanareta kulikoni hadi hivi sasa umeme ukikatika *TANESCO* na sisi tunakosa, kwa maana hiyo hakuna haja ya kuwa nay ale majanareta. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Bumbwini kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ametujaalia kukutana hapa jioni hii tukiwa katika hali ya uzima na afya. Vile vile nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii niweze kutoa mchango wangu japo mdogo katika Hotuba ya Bajeti hii Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, ambayo ni wizara muhimu kabisa, kwa sababu maji ni uhai na bila ya maji hatuwezi kufanya chochote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimshukuru sana Mhe. Waziri wa wizara hii pamoja na watendaji wake wote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nianze mchango wangu kwa kuipongeza wizara hii, kwa sababu wizara hii inayo majukumu makubwa tena mazito. Lakini namuomba Mwenyezi Mungu, aijaalie wizara hii yale mambo muhimu yote ambayo yamepangwa tena ni mazuri, basi yaweze kutekelezwa ili wananchi wa visiwa hivi tuweze kufaidika na huduma muhimu ambazo tunatarajia kuzipata.

Mhe. Spika, nizungumzie kuhusu Idara ya Mipango Miji na Vijiji. Kwa hivyo, naomba nimuulize Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwa nini tunapopanga mipango na baadaye mipango yetu inabakia kwenye vitabu bila ya utekelezaji.

Kwa kweli mpango wa kupanga Miji na Vijiji ni kitu muhimu sana hasa kwa karne hii tuliyonayo, tukitegemea ardhi tuliyonayo ni ndogo na ujenzi wetu umekwenda kiholela. Hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kuuendeleza mpango huu hasa tukiangalia sisi tulioko Vijijini ardhi tulikuwa nayo ya kutosha, lakini kukosekana kwa mpango huo bado tunaendelea kujenga ujenzi wetu wa kiholela na hatimaye hatujui tutaishia wapi, kwa sababu ardhi inakwisha na bado tunaihitaji kwa matumizi mengine.

Nikiendelea na mchango wangu nizungumzie kuhusu Usambazaji wa Maji. Mhe. Spika, katika usambazaji wa maji naipongeza tena wizara kwa jinsi inavyochukua juhudi ya kutekeleza pale uwezo unaporuhusu yale wanayoweza kuyatekeleza kwa wakati ule.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kuangalia sana juhudi zinazochukuliwa na wizara kwa kuangalia utendaji wa wafanyakazi wetu. Kwa kweli wakati mwengine wizara inachukua juhudi kubwa na kupanga na kutekeleza mambo muhimu, lakini kuna baadhi ya wafanyakazi huwa wanafanya uzembe wa kurejesha nyuma vitendo vya serikali. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, suala hili aliangalie sana kwa sababu kuna wakati hutokea maharibiko madogo

madogo ambayo tunaweza kukidhi kuyatengeneza. Kwa mfano, bomba linaweza kupasuka na taarifa ikatolewa, lakini kwa uzembe basi tutaliacha liendelee kuvuja maji pale kwa muda mrefu na wakati tukijua kuna watu wengine wanakosa huduma hii muhimu.

Vile vile wakati mwengine kuna taarifa tunazitoa zinaopoanguka nguzo za umeme wakati inakuwa ni suala la hatari, lakini huwa hatuchukui hatua za haraka kuweza kulidhibiti lile mpaka tunasubiri ushahidi kamili afe mtu, baadaye ndio tuweze kuchukua hatua. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, aliangalie suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa nataka nitoe wito kwa wafanyakazi ambao tumejikubalisha kuwatumikia wananchi, basi tuweze kufanyakazi kwa uadilifu kabisa, tukijua kufanyakazi kwetu pale ni faida juu yetu, lakini pia ni faida kubwa ya taifa letu pamoja na wananchi wa nchi hii.

Pia wito wangu Mhe. Spika, niupeleke kwa wananchi ambao tuko Mijini na Vijijini. Mhe. Spika, tunatakiwa sisi wenyewe wananchi ambapo serikali yetu inafanya juhudi kubwa, basi na sisi tunatakiwa tuziunge mkono juhudi zile ambazo serikali yetu inazichukua. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naweza kuyasema haya, kwa sababu sisi wananchi tuna tabia. Kwa mfano, serikali inaweza ikagharimu kuleta mabomba na kuzika, lakini bila ya kujali na kuthamini nguvu za serikali, basi mtu anaweza kwenda kuchimba shimo la mgomba pale pale lilipopita bomba na bomba lile likapasuka na maji yakamwagika ovyo.

Wakati mwengine inawezakana serikali imejitahidi imepeleka mabomba na mifereji katika vijiji yameenea, lakini mfereji umeharibika au umekatika basi tunashindwa sisi wananchi kuunga mkono juhudi zile kwamba fedha zilizotumika pale ni nyingi. Hivyo ni vyema tuweze kuthamini huu mfereji ulioharibika tuchangishane ili tuweze kuweka mwengine na kuepusha maji yale yasipotee na baadaye wenzetu wa mbele waweze kufaidika, sasa hili linakuwa linatushinda sana.

Kwa hivyo, naomba wananchi wenzangu ambao wanatusikia kupitia kwako Mhe. Spika, waweze kujua kwamba yote yanayopangwa hapa ni kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa nchi hii. Kwa maana hiyo, ni vizuri na sisi tukathamini, tukayahifadhi pamoja na kuyalinda. *(Makofi)*

Mhe. Spika, siku hizi hapa kwetu kumezuka utaratibu ambao ni mbaya kabisa hasa kwenye umeme. Kwa mfano, umeme unapozimwa tu, basi huzuuka wimbi la uwibaji wa nyaya zile za umeme mpaka serikali ikaemewa, kwa sababu

serikali inategemea mimi ninayo shida yangu imefika hapa, basi nategemea nikipata fedha nikiwezeshwa tena basi nichukue juhudi hizi nizipeleke huko. Kwa kweli juhudi hizi zinashindwa kufanikiwa, kwa sababu inabidi turudie pale pale kuanza kusambaza nyaya zile badala ya kupeleka kule ambako haujafika umeme hata siku moja.

Mhe. Spika, haya ni ya kwetu tena ni mipango tunayopangiwa sisi wananchi ni lazima tuthamini na tupende. Kwa hivyo, naomba Mhe. Spika, kwa siku nyengine za mbele wakati inapokaribia bajeti basi pia tuweze kufanya makongamano, ili wananchi waweze kujua hiki kinachojadiliwa hapa ni cha kwetu. Kwa maana hiyo, waweze kuthamini kwamba yanayojadiliwa humu ni yetu sote kwa ajili ya manufaa yetu, vizazi vyetu pamoja na wajukuu zetu ambao wanakuja. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu suala la mafuta. Waheshimiwa Wajumbe wengi wamechangia suala hili na wameeleza vizuri, kwa sababu wao walikuwepo katika kipindi kilichopita kwa hiyo wanajua vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Spika, yalipokuwa yakielezwa mimi nilikuwa nahisi ah! ni ndoto za mchana, hivi haya mafuta kweli yapo, yaani nilikuwa nikijiuliza suala hili. Lakini kwa kupata uthibitisho kwa kuingia na mimi katika Baraza hili, basi nimejua kweli mafuta yapo. Sasa kwa nini tusifaidike wananchi wa nchi hii kupitia rasilimali hii? *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunaelewa mafuta yakipatikana, basi nchi hii yaani wanawake wa nchi hii kwanza tutang'ara sisi, watoto wetu pamoja na wajukuu zetu watakaokuja. Kwa kweli haya hata sisi pengine tusiyawahi, lakini naamini yakifikia katika hatua nzuri basi kizazi chetu kitaweza kufaidika, watoto wetu wataweza kusoma vizuri, watapata ajira nzuri ambapo hivi sasa tunasumbuka. *(Makofi)*

Hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho, atueleze nini kinachokwamisha mpaka tunazungumza kila siku suala hili kwa hili, au Mhe. Waziri aweze kutupa sababu nzuri ama maneno mazuri ambayo yataturidhisha kuna haya si ya kuondoa kinu juani, isipokuwa haya yatakuwa kweli ni ya utekelezaji na yanaweza kutekelezeka na sisi tukitia maanani. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mafuta yakipatikana katika nchi hii basi lazima Unguja tuweze kufikia mafanikio makubwa tena kwa muda mfupi sana. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwa sababu Waswahili wanasema "penye wengi hapaharibiki neno". Kwa maana hiyo, Mhe. Waziri alipokwama

atueleze na hiki ndicho chombo tunachokitegemea, hivyo alipokwama atueleze, ili tuweze ku-*push* kwa pamoja. *(Makofi)*

Sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la Hatimiliki. Mhe. Spika, Hatimiliki kitengo hiki nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, akiangalie sana, kwa sababu kitengo hiki hutusababishia migogoro na wakati mwengine huwa inasababishwa kutoka wizarani. Kwa mfano, najiuliza inakuwaje mtu anaweza kupewa Hatimiliki kwa maaana tayari nimeshamiliki pahala, lakini pahala hapo nilipopamiliki akaweza tena kupatiwa hati mtu mwengine inakuje.

Kwa upande wa suala la kumbukumbu zinaonesha kila kitu, kwamba hati hii amepewa fulani na yupo pahala fulani na kiwanja kiko pahala fulani, hivi inakuwaje anapewa mtu mwengine hati nyengine ya kiwanja kile kile.

Kwa kweli suala hili namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, aliangalie sana kwa ajili ya kuepusha migogoro na kuianza yeye wizarani, nadhani ni vyema migogoro kuanza kwa wananchi wenyewe na kuliko kuanza ndani ya ofisi yake. *(Makofi)*

Vile vile katika Hatimiliki tunayo Ofisi yetu ya Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini "A" Gamba pale ambayo inajengwa. Kwa kweli ofisi hii namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwa kuwa ni Ofisi ya Serikali na wala bado haijapata Hatimiliki. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aione Ofisi ya Mkuu wa Wilaya aweze kuipatia Hatimiliki kwa ajili ya kuweza kumiliki sehemu ile kwa uhalali.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, niseme nashukuru na ninaipongeza wizara tena naitakia kila la heri, hasa tukizingatia upatikanaji wa mafuta katika visiwa vyetu, ambapo tunajua tunaweza kukwamuka kwa masuala mengi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, vitabu vyetu vya bajeti vinakuwa vinaonesha *billions*, tunataka tuone *trillions* baada ya kupatikana mafuta. Baada ya kusema hayo na mimi naunga mkono hoja hii pamoja na Wanawake wa Mkoa wa Kaskazini kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Bisillah Rahmani Rahim. Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijaalia jioni hii kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Kwa kweli wizara hii imechukua mambo makubwa, muhimu tena ni magumu.

Pili nimshukuru Mhe. Waziri wa wizara hii kwa uwasilishaji wake hotuba hii kwa umakini, upole pamoja na utaratibu mkubwa sana. Pamoja na pongezi hizo pia nimpongeze Mhe. Waziri aliyetangulia nyuma wa Afya kwa ujasiri wake

akiwa ni waziri wa kwanza kwa Zanzibar kutangaza kama ataweza kujiuzulu pindipo jambo fulani halikutendeka. *(Makofi)*

Hali hii inaonesha kuwa ni makini na yuko tayari kufanyakazi pindipo serikali ikimuwezesha kufanyakazi na kama haikumuwezesha, basi yuko tayari kuacha kazi. Ahsante sana Mhe. Waziri kwa uamuzi huo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo fupi kwa mawaziri hawa wawili, nianze mchango wangu katika Mamlaka ya Maji, mimi nilikuwa mwanafunzi zamani, wakati nilipokuwa darasa la saba Mwalimu wetu wa Somo la Kiingereza alituangikia *Composition* kuhusu Maji.

Kwa hivyo, naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika, sehemu ya *conclusion* ya *Composition* hiyo ambayo inasema hivi: "Ni wale tu, kwa wakati huo waliokuwa wakiishi majangwani ndio waliokuwa wakijua umuhimu wa maji katika thamani yake halisi.*" (Makofi)*

Mhe. Spika, na sisi tuchukulie kama tuko jangwani, kwa sababu kila Mzanzibari sasa anajua thamani ya maji na wala hakuna hata mmoja ambaye hajui umuhimu wa maji. Vile vile yeyote yule atakayekuwa akipita mitaani akagundua maji yanamwagika ovyo basi anachukia, kwa sababu tayari kila mmoja wetu anajua thamani ya maji.

Lakini sina hakika kama serikali au wizara yenye kama inajua kwamba kweli maji yana thamani? Je, wanajua kwamba kila mtu anahitaji maji? Je, kila kinachoishi kinahitaji maji, ili kiweze kuishi? Mhe. Spika, sijui kama wanajua hivyo. Mhe. Spika, *pipes* za maji takribani zimesambaa katika nchi nzima, lakini sio kama kila kwenye *pipe* ya maji kuwa maji yanapatikana.

Kwa kweli huu mtindo tuliouzoea wa kuwa japo wiki mara moja. Mhe. Spika, maji hayataki wiki mara moja, kwa sababu maji yanahitajika masaa 24. Sasa ile hali ya wiki mara moja sijui tunaonesha nini, jambo ambalo inalazimu tukaliwekea wakati kuwa angalau tunapata wiki mara moja au mbili. Kwa hivyo, maji hayataki hivyo, isipokuwa kuna haja wakati wote kupatikana maji, kwa ajili ya maisha ya wanaadamu, wanyama pamoja na mimea.

Mhe. Spika, leo sisi watu wanashukuru kwa kupata maji wiki mara moja si vibaya. Lakini je ndivyo inavyotakiwa? Kwa maana hiyo, niseme kwamba maji ni muhimu na Mamlaka ya Maji ijue hivyo kuwa maji ni muhimu.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha uliopita wamesema kwamba walikusanya shilingi milioni 655,000,000,/=, ambapo matarajio yao walikuwa

wakusanye elfu 2,000/= na milioni 51,000,000/=, lakini hawakufikia, kwa nini? Kwa sababu watu hawapati maji na hivyo hawalipi.

Kwa kweli watu hawawezi kulipa maji kwa sababu kuna *pipe* kwenye nyumba yake, isipokuwa watu watalipa maji kwa kuwa wanapata maji. Kwa hivyo, Mamlaka ya Maji wafanye watu wapate maji na waone kwamba watu hawatolipa maji, kwa sababu wanataka pesa wakati watu hawapati maji na wala watu hawatolipa, kwani watu watakilipia kile ambacho wanakitumia.

Mhe. Spika, katika Jimbo langu la Mtambile na kwanza nije Kengeja. Kengeja katika Jimbo la Mtambile ni sehemu moja ambayo ina maji zamani sana tokea enzi zile tulizokuwa tukitawaliwa, yaani Kengeja ilikuwa inatumia maji ya pomba kuanzia mwaka 1958, hali kadhalika miaka hiyo walianza kupata huduma ya umeme.

Sasa nirudi kwenye huduma ya maji. Kwa wakati huo kisima kilichokuwepo kilikuwa kinakidhi haja ya watu wanaotumia maji ya bomba na kisima kile kilikufa. Kwa hivyo, wizara hii imechimba kisima chengine mkabala na Chuo cha Ufundi cha Kengeja. Kisima hiki hakikidhi haja ya maji kwa Kengeja, kwa sababu watu wanaweza kupata maji kwa mgao na mara kwa mara mashine yake inaharibika kutokana na maji yake kuwa si safi.

Lakini pale pahala pa awali Mjiweni penye kisima cha awali pa ni sehemu nzuri tena maji yapo, isipokuwa waliamua kuchimba sehemu nyengine. Mhe. Spika, kuna tetesi kwamba kuna mchezi ulikuwa unachezwa, yaani kulikuwa kuna maslahi fulani watu walikuwa wanafuatilia kuwa pindipo wakichimba kisima pale kilipo cha zamani tayari kile kijumba cha machine kipo kuna fedha watu watazikosa.

Kwa hivyo, wakaamua wakachimbe kule na hicho kibanda cha maji ambacho kilitumia kama shilingi milioni 10/=, basi hiki ndicho kilichofanya watu wakachimbe kule haidhuru watu wakose maji, lakini watu wengine kidogo wapate chochote, inasemekana hivyo. Mhe. Spika, kwa ufupi maji Kengeja hayatoshi.

Kwa kuwa Mhe. Waziri kama alivyotuambia anategemea kuchimba visima kama 30, basi ninamuomba kwa kupitia kwako Mhe. Spika, kwa hisani yake na sisi watu wa Kengeja atuonee huruma na kutuchimbia kisima na machine zake, ili watu waweze kupata maji angalau kama watu wengine wanavyopata, yaani kama hawakupata kila siku basi jambo kama wavyopata watu wengine.

Kwa kweli hayo yaliopo basi kuna vijiji havipati maji. Kwa hivyo, imani yangu kama kutachimbwa kisima chengine basi pale ambapo kipo kisima cha asili uwezo wa sehemu zote za Kengeja kupata maji utakuwepo.

Nikiendelea na mchango wangu nizungumzie kuhusu Shirika la Umeme. Mhe. Spika, nimetizama kwenye mapato yao waliyoyataja kwa mwaka uliopita pamoja na matumizi yao, nimeona kuwa wametumia zaidi ya kile walichokusanya.

Kwa hivyo, hapa wameonesha wamekusanya shilingi bilioni 24,688, 305,373.98/=. Lakini walizokusanya ni shilingi bilioni 24,149,483,454/=. Mhe. Spika, nilikuwa mwalimu lakini si wa Somo la Hesabu, naomba hapa kuna zaidi ya shilingi milioni 500 walizotumia ambazo sikuziona wamezichuma wapi.

Namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, anioneshe hizi za ziada zilizotumika zimetoka wapi? Sasa kama hili shirika linajiendesha, basi ina maana halina uwezo wa kujiendesha, kwa sababu wametumia zaidi ya kile walichokichuma na mimi kile kilichozidi sikuona kimetokea wapi.

Mhe. Spika, Shirika la Umeme ni Shirika la Biashara zaidi kuliko huduma. Lakini ule mfumo wa kibiashara bado hawajauweza kama ilivyo, kwa sababu mwananchi anaweza kuomba kuungiwa umeme naomba nitumie Lahaja ya Kipemba anatimbwa, yaani anahangaishwa na suala ni la biashara, lakini hiyo dhiki atakayopata haina mfano.

Vile vile hata hiyo huduma ikimfikia baada ya kufanya mambo yake yote, basi kuutoa umeme kutoka kwenye nguzo kwenda nyumbani mwake, imani yangu hivi sasa sisi watu wa vijijini hatumudu tena kuingiza umeme katika nyumba zetu.

Mhe. Spika, kabla sijataja hapa kuna mtu mmoja nyumba yake na ilipo nguzo ya umeme ni mita ishirini, sasa alijikaza katika kuunga umeme, akaja mtu wa shirika kwa ajili ya kufanya mahesabu na kumwambia atalipa shilingi 547,200/= mtu ambaye kunywa chai hamiliki. Kwa hivyo, bado hili shirika linafanya biashara katika hali hiyo.

Mhe. Spika, wako waliotangulia mwanzo walisema kama hali ndio hii basi angalau hawa watu waweze kukopeshwa na kulipa kwa awamu. Sasa watu watu huduma wanaitaka, lakini Mhe. Spika si mchezo kutoa fedha hizo kwa ghafla kwa watu wengi ambao wanaoishi vijijini, watu ambao wanakaa wanamsubiri Mheshimiwa wao wampigie hodi. Kwa hivyo, shirika lazima lijue kuwa biashara hii wanaidumaza ndio nikamwambia Mhe. Waziri kwa kuwa

shirika ni la kibiashara kuna msemo wa watu siku hizi unasema mteja ni mfalme, kwa hivyo tunaomba mufanye kwamba mteja ni mfalme na tunapopata wateja ndio tunaisaidia serikali tusiwafukuze wateja, tuwaiteni wateja. Wanzetu wengine pahala mtu akipimiwa kiwanja tu watu wa umeme wanaanza kuleta huduma hata nyumba haijajengwa sisi tunajenga mtu anataka huduma anahangaishwa sijui kwa nini.

Mhe. Spika, kuna usambazaji wa umeme vijijini nami ningemuomba Mhe. Waziri katika mradi huu wa kusambaza umeme vijijini anisaidie katika vijiji vya Jimbo langu ambavyo bado huduma hii haijapatikana, kuna vijiji kama Mkungu, Jaani, Bitatudi, Kidutani, Mabweni vijiji vyote hivi havina umeme. Kwa hivyo ningeomba na wao pia wapatiwe huduma hii ya umeme.

Mhe. Spika, nije katika Ardhi mara nyingi mimi huja Zanzibar kila sehemu ya ardhi inamiliki kama tunamjua kama hatumjui, kama anayemiliki anajua au hajui, lakini kila senti mita moja ya ardhi ya Zanzibar ina mwenyewe hata zile ambazo serikali imetaifisha kwa sababu ilikuwa ina mwenyewe, kwa hivyo katika kujenga taasisi zetu serikali kwanza ningeomba tuhakikishe kuwa tunajenga katika ardhi ambayo tayari ni milki ya serikali. Ili kuepusha mizozo na mivutano na wananchi watu wana nyaraka za shamba zao, watu wananyaraka za kila kitu wakijua hapa ni kwangu kama pametaifishwa anajua lile lilikuwa shamba langu lakini serikali imechukua.

Sasa pale ambapo hapajachukuliwa halafu sisi tu tukaweka taasisi yetu tunajenga mahusiano mabaya na wananchi wetu, serikali ipo kwa ajili ya watu na ipo kwa ajili ya kuwatumikia watu ndio kazi yake iwatumikie tuwathamini raia wetu, tuwafanyie haki raia wetu ili wawe na imani na serikali yao, tusiwajenge raia wetu na wananchi wetu tunaoongoza wakawa hawana imani na chombo kinachowaongoza, wametupa ridhaa zao halafu sisi tukawafanyia kinyume. Tukapoteza uungwana kwa kima fulani.

Mhe. Spika, nimalizie kwa suala ambalo limezungumzwa sana kwa kitaalam na watu mbali mbali wenye hekima na ujuzi na wenye kupekua mambo mbali mbali la nishati ya mafuta, katika Afrika moja katika nchi ambayo inazalisha mafuta ni Nigeria na jimbo moja la Mashariki ndio linalozalisha mafuta kwa wingi katika miaka ya 1960 na mwanzo wa 1970 nchi ile imeshuhudia mapinduzi ya mara kwa mara, kuna kipindi fulani hili jimbo la mashariki hili ambalo ndio lenye kutoa mafuta kwa wingi lilikuwa mdhamana wake ni mwanajeshi Kanal Ojuki kwa kuwa jimbo lake ndio linatoa mafuta kwa wingi lakini halifaidiki na mafuta hayo aliamua kujitenga katika serikali ya Shirikisho ambayo ina majimbo kumi na mbili, yeye akaliengua jimbo lake katika shirikisho lile lakini serikali kuu haikukubali kwa hivyo ukafanyika mzozo

wakauana barabara lakini hatimae alishindwa na jimbo likarudi katika mamlaka ya Nchi.

Kuna msomi mmoja aliuliza kwa mwenzake *What is the worst calamity of man* akamwambia *the worst calamity of man is to have eye but can see*. Kuwa na macho lakini haoni sisi tusiwe hivyo sisi tuna macho na tuoneni, tukikubali kubakia hivi tulivyo wenzetu watufunge shemere itakuwa tuna macho lakini hatuoni, mafuta yaliyokuwepo Zanzibar ni ya Wazanzibari, gesi iliyokuwepo Zanzibar ni ya Wazanzibari na sisi tuna macho tunajua kuwa ni haki yetu. Kwa kuwa sisi humu sote ni Waislam tutafanya kosa ikiwa tutakwenda kinyume na dini yetu tunatakiwa mtu atetee haki yake mwisho wa uwezo wake. Sisi wawakilishi mwisho wetu ni kuiambia serikali kwamba mafuta ni yetu, nanyie serikali muwaambie wenzetu mafuta ni ya Wazanzibari umefika wakati tuache hii hewala bwana itatuweka pabaya.

Mhe. Spika, Zanzibar yenye watu katibu milioni moja na nusu ikawa tunaishi maisha duni kuliko wengine wowote katika Afrika ya Mashariki, wakati ambapo Zanzibar ilikuwa ni nchi kabla ya muungano ilikuwa ni nchi ya pili kwa utajiri ukiondoa Uganda, Zanzibar katika Muungano tumesarenda kiti chetu cha umoja wa mataifa tulikuwa na kiti sisi cha umoja wa mataifa tumekisarenda kwa muungano, hawa wenzetu hisani hii hawaioni.

Mhe. Waziri kwa heshima kubwa sana na kwa kuwa ni mtu makini mzalendo, mwenye kupenda maendeleo ya Zanzibar, Mzanzibari halisi sidhanii kuwa utakuwa tayari uje ukaulizwe pahala ambapo jibu la mchezo halitokubalika, kwa sababu viungo vyote vitakuwa haki ya kusema, mdomo utafungwa. Serikali nataka ijue hivyo iko siku sisi na nyinyi tutahojiwa midomo itafungwa, viungo vyote vitasema sasa tutasema nini pindipo rasilimali ya Wazanzibari kuacha kutumiwa na watu wengine bila ya kuipatia ufumbuzi.

Mhe. Spika, hili jambo ni muhimu kwa maendeleo ya nchi na wananchi wake, tusiwafanye watoto wetu wakaja kutuona kwamba wale barazani walikuwa wakifanya nini, tusifanye watoto wetu wakaja kufunga vibwanga kutafuta haki yao bado tunayo nafasi ya kutafuta haki yetu juu ya meza na tukikazana tutachukua juu ya meza.

Mhe. Spika, naona umeshawesha taa yako kuashirika kwamba nimemaliza muda, kwa hivyo pamoja na kuwa ombi langu hujalikubali na kwa kuwa mimi nafasi yangu ya kusema ni ndogo ndogo kutokana na maumbile yangu kwa sababu nataka nifahamike, nikisema kama anavyosema Mhe. Hamza Hassan Juma hata neno moja hamtolisikia. Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, ahsante sana na nitaunga mkono hoja pale ambapo nitapata ufafanuzi way ale ambayo nimeyazungumza.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia bajeti hii ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Mimi moja kwa moja nitakwenda kwenye suala la maji au Mamlaka ya Maji.

Mhe. Spika, kwanza maji ni muhimu kwa kiumbe chochote kile iwe mmea, iwe binaadamu mwenyewe au mnyama ni muhimu sana sasa mimi nazungumzia kuhusu kisima cha Kiashange yaani cha mzungu hicho, kisima kile wamekwenda wataalam na wamesema kina maji ya kutosha, kwa maana hiyo namuomba Mhe. Waziri baada ya kuwa watu wameshakwenda na wataalam wao wamekwenda kinyemela nyemela na wameligundua hilo namuomba na yeye aende na wataalam wake nadhani anao wataalam hao, ahakikishe hili suala ni kweli au sio kweli.

Lakini cha kusikitisha Mhe. Spika, kwanza nasema ni jambo zuri lakini pia sio zuri kwanza tumiliki tuliyokuwa nayo tuyafanyieni kazi tuhakikisha je kuna tatizo jengine, ndio tuanze kuchimba visima vyengine nadhani tumeshapewa taarifa kisima hicho kina maji ya kutosha tatizo ni *pump* naona ajabu kuwa vinachimba visima vingine si tutafute hiyo *pump* yenyewe ili tujue tatizo *pump* au kisima chenyewe au tatizo ni kitu gani. Sasa namuomba Mhe. Waziri kabla hajatuchimbia hicho kisima tunacholetewa misaada na hao watu kwanza ahakikishe kisima cha Kiashange tatizo lake likamilike kuwa ni *pump* hakuna tatizo jengine lolote Mhe. Spika, maji yapo ya kutosha na yana uhakika wa Matemwe nzima kutumia maji yale kwa maoni ya wataalam.

Mhe. Spika, sasa nije kwanye kisima cha Kandwi ambacho kinapeleka maji shehia ya Pwani Mchangani, hapa kwanza napongeza sana kwa kuzindua hiki kisima lakini naumia sana Mhe. Spika, kuwa wananchi wa sheria ya Pwani Mchangani wamekula kazi ya kuchimba mtaro ule, tena tumetumia nyundo na nondo masururu na kila kitu zana za kuchimbia, leo hii anaonekana mwananchi sio bora kupata maji kuliko muwekezaji wakati wana uwezo wa kununua maji kuliko wananchi wetu.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri hili akafanye uchunguzi wa kina wawekezaji wanayavuta maji kwa kutumia mota zao, wananchi wanakosa maji na wananchi wamekula nguvu kubwa ili kuondoa tatizo lile la maji wamejitolea kwa hali na mali, sasa namuomba Mhe. Waziri kwa kuwa watu wanasema serikali ni watu na watu ndio sisi tunapoleta malalamiko yetu yafanyiwe kazi na serikali kuu jamani.

Mhe. Spika, sasa hivi nakwenda kwenye umeme katika jimbo la Matemwe kuna baadhi ya vijiji bado havijapata umeme, lakini cha kushangaza Mhe. Spika, umeenda kuchezwa mchezo wa danganya toto mchezo wenyewe

wamekwenda kupimiwa kule ikesha hakuonekani lolote, lini watafanyiwa hiyo kazi ya kuwekewa hiyo nishati ya umeme wakajisikia hasa na sisi tuko katika serikali yetu hii ambayo inatuthamini, viongozi wanatuthamini. Namuomba Mhe. Waziri mchezo wa dana dana usikuwepo kwa wananchi wetu, sasa hivi wananchi wanapoamua jambo na wanapotaka jambo watekelezewe kusiwe mbele na kinyume inakuwa sio jambo zuri jamani, Serikali iwaone wananchi tena sio wa kijiji changu tu au jimbo langu tu yaani majimbo yote au vijiji vyote vilivyokuwa havina umeme, vipatiwe kwa sababu maendeleo ni umeme na umeme una mambo mengi unaleta neema kubwa. Halafu pia serikali inafaidika kutoka kwa wananchi kupitia kwenye njia za umeme kwa sababu wananchi wanachanga mle sidhani kama umeme wanatiliwa bure tena wakasema huu ni wa bwanyenye lazima wanalipia.

Sasa tufanyeni hii kazi tupate mapato kwa wananchi na serikali, hapo hapo kwenye umeme namuomba Mhe. Waziri watu wanasema bora kinga kuliko tiba, na ujenge ufa kuliko kulijenga lile jumba zima.

Sasa Mhe. Spika, jimbo hilo hilo la Matemwe hivi vijiji vilivyobahatika kupata umeme Mwenyezi Mungu atujaalie atuondoshee yasija yakatokea maafa, lakini maafa mengine mbona kama serikali inachangia kwa sababu kuna nguzo zina muda wa miaka mitatu zimeanguka chini, namuomba Mhe. Waziri anieleze nguzo zile zinaenda kufanyiwa marekebisho lini mimi sizuii chochote lakini anipe uhakika tu, anambie kama tarehe 20/1/2011 na ikifika tarehe ile mimi nitamfuata huko huko aliko. Nitamwambia tarehe uliyoniahidi imefika naomba ukaniwekee zile nguzo kwa sababu ikitokea athari sio kwa wananchi wa sheria ile tu ya jamii nzima au serikali.

Kwa sababu yakitokea maafa lazima serikali itawagusa au haiwagusi jamani, sasa naomba Mhe. Waziri kwa kuwa nguzo zile ziko muda mrefu zina miaka mitatu sasa, namuomba Mhe. Waziri sitaki aniambie miezi mingapi anipe siku chache kabisa aniambie Jumatano nakwenda kukubadilishia nguzo zako, kwa sababu nasema hivi hili ni jambo la hatari na likitokea tumeathirika zote au serikali nzima imeathirika. Nguzo zimelala chini nyengine zimeunganishwa na minazi, nyengine zimeegemea nyumba, nyengine zimelala, sasa tufanye marekebisho madogo madogo tusingoje kujenga nyumba wakati tunauona ufa, bora tuzibe ule ufa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakuja kwenye mafuta na mimi kiduchu watu wanasema hivi unapoona watoto wanalia ujue wana njaa, sasa hivi na Wazanzibari wana njaa ili iondokane hii njaa Mhe. Spika, tuchimbiwe mafuta yetu mimi naamini tunasema Zanzibar ina umasikini, lakini Zanzibar tukitaka iondokane na umasikini tuchimbe mafuta yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, vijana wengi wanadhurura ovyo wanaranda ovyo wanajihusisha na mambo yaliyokuwa hayana maana wanalewa, wenye kujitoga sindano mtu yuko Zanzibar hapa anakwambia nipo Nairobi tatizo ni hilo, lakini tukishakuchimba mafuta yetu mimi naamini vijana wengi watapata ajira. Kwa maana hiyo Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri hili suala tulifanyie kazi asitwambie mpango mpango huu mpango sio matumizi, tufanye kazi Wazanzibari na sisi tubadilike na ili tubadilike tuchimbiwe mafuta yetu, haya mafuta hayako kwenye Muungano tushaambiwa hapa sasa mnatwambia nini sisi vijana hatusikii kitu tuchimbiwe mafuta Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nitaunga mkono pindipo Mhe. Waziri akinambia mwezi ujao nguzo zangu zinaenda kufanyiwa marekebisho. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu katika bajeti hii inayoendelea kuchangiwa, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na wataalam wake wote walioandaa bajeti hii nzuri na sisi kupata muda wa kuichangia.

Mimi nitachangia sehemu nne tu sehemu mbili nimetumwa na wananchi na sehemu mbili mawazo yangu kwa jumla kwenye bajeti hii, kwa hivyo kwanza nitaanza na mradi wa maji Vijijini ukurasa 52 kifungu cha 92. Katika jimbo langu la Mfenesini tumebahatika kupata mradi unaoitwa ACRA na mwaka jana ulitiwa kwenye bajeti, lakini mwaka huu sikuuona wala haukusemwa kitu, lakini nashukuru kwamba ule mradi umeshafikia hatua za mwisho ambao utatoa huduma kwa jimbo langu la Mfenesini, Jimboa la Kitope na Jimbo la Bubwini na tayari visima vyote vimeshachimbwa Mfenesini, mashine zimeshafungwa tangi limeshajengwa Michungwa miwili, mabomba yameshasambazwa mote. Taaria tuliyopata ilikuwa huu mradi ufunguliwe mwezi wa tano mwaka huu, lakini mwezi wa tano umeshapita sasa tunakwenda kwenye mwezi wa nane kwa sababu wa saba tumeshauanza.

Tulijaribu kufuatilia tukasikia kwamba kilichobakia hivi sasa ni kuwekwa mifereji ya nje kwa sababu huu mradi ni endelevu, tayari wameshafunzwa vijana, mafundi wa kuendesha huu mradi kwa kukusanya mapato kwa uchangiaji ili ukiondoka mkono wa wadau tuweze kuendesha wenyewe kwenye majimbo matatu, kwa hivyo wataalam wapo wanasubiri kazi. Lakini tunasikia kwamba vifaa vya mwisho vya kumalizia mradi huu ya ni ya kufunga mifereji ya nje pamoja na wanaotaka kutiliwa ndani ya majumba kwamba meli ya vifaa hivyo imetekwa nyara na Wasomali.

Sasa tunajiuliza kwamba mradi umebakia sehemu ndogo sana ya kuweka mifereji tu ya nje basi serikali haiwezi kusaidia kwa kuwa vifaa vimeshatekwa

nyara au ni maneno ya mitaani tu, sasa namuomba Mhe. Waziri atujibu kwamba kweli mradi umeshakwama vyombo kweli vimetekwa nyara au haujafika siku ya kufunguliwa tu, ili wananchi wapate faida na wajue mradi wao utaanza lini, kwa sababu huko tunakokwenda hivi sasa ni mwezi mtukufu wa Ramadhani na mwezi unaotumia maji kuliko miezi yote.

Sasa namuomba Mhe. Waziri mwenzangu sana jirani yangu atupe muda wa kufunguliwa mradi huu ni kweli vifaa vimetekwa nyara ama bado tu mradi haujakamilika.

Suala la pili usambazaji umeme vijijini, ukurasa wa 59 kifungu 107 hapa imesungumzwa jumla jumla kwamba vijiji vyote vilivyosalia vitamaliziwa kusambaziwa umeme, mimi nashukuru na naipongeza serikali katika jimbo langu shehia zote saba umeme upo imebakia sehemu ndogo ndogo na sehemu kubwa ambayo sasa hivi ina dhiki ya umeme ni kutoka Mndo kuja Mkanyageni njia ya Mwakaje, tayari kumepelekwa wataalam wamefanya makisio yao na wametaka milioni mbili tumeshazikabidhi Wizara, lakini nguzo zilizokuja zimepanda bei kwa hivyo mradi haukuweza kutekelezwa kwa sababu zinatakiwa pesa za ziada.
Sasa namuomba Mhe. Waziri kwa kuwa sisi wananchi na viongozi tumeshapeleka mchango wetu kwa hivyo hizo ziada basi katika huo mradi wa vijijini usambazaji wa umeme watumalizie wao, kwa sababu sisi tumeshaonyesha nguvu zetu, chakusikitisha zaidi ni kwamba tulikuwa tayari tumeshanunua nguzo za kusambazia laini ndogo ndogo nguzo thalathini, sasa hivi huu mwaka ziko chini zimekaa hazijachomekwa wala hazijafanyiwa huduma yoyote. Kilichokuwa kinasalia ni laini kubwa Kutoka Mndo kuja Mkanyageni hiyo ambayo tumeichangia sasa tunamuomba Mhe. Waziri atusaidie ili hizi nguzo tulizokwisha kununua zisiweze kuharibika.

Lakini pia mradi wa pili wa kusambaza umeme uko Kama kijiji kipya kwa Mzee Kidishi unatoka JKU unakuja kwa Mzee Kidishi na pale wamefanya thamani ya Shs. 2,800,000/= wanakijiji na viongizo wameshachanga Shs. 1,800,000/= imebakia milioni moja, sasa pia naiomba kwa kuwa kuna fedha za usambazaji umeme vijijini basi naomba tukimaliza bajeti unipe watu wako wanaohusika ili na hili tatizo la Kama mpaka kwa Mzee Kidishi tukaliondoe, sehemu zilizobakia zote tunashukuru ikianguka nguzo tunatoa taarifa na wanakuja kutengeneza fyuzi zikiripuka tunakuja kutengenezewa tunashukuru sana. Sasa naomba hii miradi yangu miwili ya umeme Mkanyageni/Mndo na JKU kwa mzee Kidishi tusaidiwe ikisha bajeti hii na wananchi hawa nao watoke kwenye matatizo haya hayo ni maagizo ya jimbo langu.

Sasa naomba niingie kwenye bajeti kijumla kwenye ukurasa wa 58 kazi za maendeleo imetajwa hapa kuna kazi za maendeleo mbili, moja ilikuwa ufungaji

wa mita za tukuza ambao nashukuru sehemu nyingi wanaotumia umeme wa tukuza wanakuwa hawana kero wala adha, unatia pesa zako unatumia kwa mujibu wa pesa zako. Bajeti iliyopita ilizungumzia kwamba maeno ya Bubu kitajengwa kituo cha kuuzia umeme pamoja na Kwerekwe, nashukuru Kwerekwe kituo kimejengwa na sasa kinatoa huduma. Sasa ningeliomba kuuliza je hii Bububu imeondoshwa katika mpango huo au imo katika huu mpango wa tukuza wa kwenda kufunga mita Bububu, namuomba Mhe. Waziri anipatie jibu atakapokuja ili wananchi wale pale Bububu, Mtoni na wao waweze kupata hizo *TUKUZA* na wapate kituo cha kununulia umeme Bububu ili waondokane na kero ya kuja kusomewa mita.

Mhe. Spika, wanzangu walizungumza umeme mbadala kwamba hivi sasa lazima kama kisiwa na sisi lazima tumitahidi tuwe na umeme wetu na wameshakuja wawekezaji wangi kujaribu kwa njia ya upepo, njia ya jua na njia ya maji ya bahari, lakini tunavyosikia baada ya kutolewa taarifa zao kwamba umeme huo unaweza kupatikana lakini una gharama kubwa na wananchi watashindwa kuuhudumia na kuununua. Sasa ninavyoshauri mimi na hii *TANESCO* ina gharama kubwa na serikali inatoa nusu na wananchi nusu, sasa kwa nini tena hao wawekezaji tushindwe serikali kutoa nusu na nusu wakatoa wananchi.

Mimi nashauri kwamba kama wawekezaji basi serikali itie mkono wake ili tuondokane na tatizo la umeme kila siku kuzimwa, mara maji yamekauka, mara laini zimeharibika, mara waya umekatika ndani ya bahari watu miezi mitatu hawana umeme. Naomba serikali itizame ifanye mahesabu kama wafadhili watawekeza umeme wa kudumu basi tuupunguze kasi ili wananchi waweze kuutumia.

Sehemu nyengine ya jumla kwenye mchango wangu nije kwenye urithi wa Mji Mkongwe tumebahatika katika dunia mji wetu umekuwa ni mji wa urithi. Lakini hivi sasa imekuwa kama kichwa cha Mwendawazimu, kila mtu anayetaka lake anafanyia Mji Mkongwe. Nitatoa mfano, hoteli kule mwanzo zilikuwa Africa House na Zanzibar Hotel ni mbili tu. Zikaongezeka Tembo, Serena, sasa hivi ukenda ukifanya hesabu kuna hoteli zaidi ya thalathini. Kila nyumba inayoanguka ikinyanyuka hoteli, mwisho watu wa Mji Mkongwe watahama na ziwe hoteli tupu, wakati maeneo ya kujenga hoteli za kitalii zipo nyingi tu.

Naishauri serikali tukiendekeza tamaa ya hoteli basi katika urithi wa Mji Mkongwe tutatolewa na tutakosa mengi. Naomba wanaohusika hoteli ambazo sasa hivi ambazo zinaanza kufanyiwa marekebisho nyumba za zamani zingesimamiwa wangeachiwa wananchi wakakaa, ili ile hadhi ya mji wetu wa urithi tukabaki nao.

Suala jengine linaloharibu mji wetu, wataalamu hawajafanya utafiti lakini naomba kama wapo wafanye. Bahari yetu iliyokuwa ya mvungu bandari ilikuwa inasaidia kuepusha kuathirika kwa mji wetu. Lakini tangu ilipojengwa bandari ya tuta kuzibwa ile mivungu sasa maji yote yanakuja katika ukuta wa Mji Mkongwe na baadhi ya sehemu imeshaanza kupasuka na unavunja na barabara inayopitia magari kuja kwenye Mji Mkongwe.

Sasa ningeshauri serikali na hilo wakalitizama, tungejaribu kujenga ukuta madhubuti zaidi ili mji wetu nao usiathirike. Kitaalamu walisema kwamba bandari ya tuta italeta athari kubwa kabla ya miaka michache tu mbele. Naomba na hili kabla haijatuathiri ningeliiyomba serikali ikatafuta watafiti ikaona kama kweli kuna tatizo basi tukalihami kama walivyosema wenzetu kwamba kwanza tuzibe ufa kabla hatujajenga ukuta. Nadhani hilo litasaidia katika kuweka mji wetu katika hadhi yake, ili tupate faida kama miji mengine ya kilimwengu.

Mwisho Mhe. Spika, kwa kuwe mengi yameshazungumzwa nije katika upimaji wa viwanja. Upimaji wa viwanja hivi sasa unafanywa sehemu ya Tunguu. Tunashukuru kwamba vinafanywa viwanja kwa uzuri na watu wanajenga. Tatizo lilokuwepo, vikishakupimwa viwanja barabara hazioneshwi mwanzo ili mtu akajua hii nyumba ninayojenga huku ninakojenga ni nyuma au ni mbele. Utakuta sasa hivi barabara zinapitishwa nyumba keshaiweka mgongoni ndio inapita barabara kwa nyuma.

Ningeshauri kwamba vikipimwa viwanja umeme upelekwe, barabara zitengenezwe kabisa pamoja na maji ili watu waweze kufanya ujenzi wa uhakika. Hivi sasa watu wengi waliojenga kule kina mmoja ana kisima chake ndani ya nyumba, ni hatari. Ningeshauri serikali viwanja kama vile vinavyochimbwa sasa hivi basi wapeleke maji, wapeleke umeme na barabara itambulikane kabisa, ili isileta matatizo. Hata hivyo tungeshauri pia wanaojenga kule kwa sababu wengi wana uwezo basi angalau tungejenga nyumba za ghorofa.

Sasa hivi wenzetu Dar-es-Salaam wameamua Kigamboni kote wananchi nyumba pale zinunuliwe zijengwe nyumba za ghorofa kuanzia mbili kwenda mpaka ishirini, wanauita mji mpya. Na sisi tungependekeza Tunguu sehemu iliyobakia basi wangetafutwe wenye uwezo zikajengwa nyumba za ghorofa kuliko kuendelea kwenda nyumba za chini tutaweza kufuka Bungi kesho kubwa. Tukifika Bungi tena itakuwa hakuna eneo la kulima. Nawashauri serikali na hilo wangelilitilia maanani ili tukaweza kujenga mji wa kileo eneo dogo lakini wakakaa watu wengi, kama mfano Michenzani. Michenzani nyumba ni chache lakini wanaoishi ni watu wengi, halafu hazikuchukua eneo

kubwa. Ningeshauri na hilo lizingatiwe na Tunguu ili tuweze kupata mji mpya tusije tukafika Bungi kwa muda mfupi.

Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nakushukuru sana.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi fursa hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, jioni hii.

Mhe. Spika, kwanza napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa hotuba yake iliyomo ndani ya kitabu chake hiki cha Bajeti aliyoiwasilisha kwa ufasaha na ufanisi katika kitabu hiki. Mimi kwanza nataka nigusie kwenye Shirika la Umeme.

Mhe. Spika, Shirika la Umeme tunaliona kuwa linachukua juhudi kubwa katika kutekeleza malengo yake ya azma ya kuwafikishia wananchi katika vijiji ili kunufaika na maslahi haya ya umeme. Bado tuseme katika Shirika la Umeme kuna mambo ambayo yana usumbufu kutokana na wateja. Usumbufu uliyokuwepo utakapokwenda katika Shirika la Umeme tayari unapatiwa fomu kujaza na kutaka upatiwe huduma ile. Lakini tatizo lilokuwepo unaweza ukachukua muda mrefu pale hujapatiwa huduma ile. Sijui tatizo lipo wapi.

Mhe. Spika, ukenda unaambiwa mara hakuna mita, siku ya pili ukifuatia tena mara hakuna hichi, ilimradi inakuwa wewe pesa ile unaijazia fomu tu. Hapo bado hujapimiwa na kuunganisha ndani ya nyumba yako, pesa zitazidi pengine 50 nyengine kwa kufatia, unakwenda na kurudi kwa kutaka kuunganishiwa umeme ndani ya nyumba yako. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri Shirika la Umeme waweze kujipanga uzuri ili kuwapunguzia wananchi matatizo kama hayo madogo madogo.

Mhe. Spika, la pili nende kwenye suala la maji ukurasa 48 Mhe. Waziri hapa katutaka wawakilishi kumsaidia wananchi katika suala zima la ulipiaji wa maji. Kwanza naomba serikali isichoke kutoa taaluma kwa wateja wao. Hapa mimi ninaloliona tatizo kubwa sio wale wanaoungiwa maji ndani ya majumba yao. Tatizo lililopo ni watu wanaotumia mifereji iliyokuwepo nje ambayo kuwa imetiwa pengine niseme na watu wawili. Kwanza serikali kupitisha mabomba yao ndio walioweka mifereji ya nje. Wa pili ni watu wasamaria wema wanaosaidia vijijini mwao katika tatizo la maji kuwapelekea mifereji. Wale hawajui ni mfereji upi ambao kuwa unapaswa ulipiwe. Mifereji ile iliyotiwa na serika ndio ambayo kuwa haitakiwi kulipiwa au na ile wanayotia pengine mbunge au mwakilishi unatakiwa ulipiwe.

Tunamuomba Mhe. Waziri atwambie ni mfereji upi ambao kuwa unatakiwa ulipiwe. Kwa sababu wale wao wakishakwenda kutiliwa pale kama ni TASAF kama ni Mbunge au Mwakilishi pia na wao huona ni serikali tu, sasa huwa wana matatizo sana ya kulipa. Naomba na mimi hili nipatiwe ufafanuzi.

Mhe. Spika, jengine la tatu mimi nataka niseme katika kijiji changu cha Tumbe ninachoishi, tunakisima ambacho kuwa kina maji ya kutosha. Tatizo lilopo maji yanayotoka ndani ya kisima kile tunasema kuwa hayapo safi na kama sio safi basi yatakuwa hayana usalama. Hili nishalizungmza kwa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alivyotoa hotuba yake nilipochangia nililizungumza na yeye mwenyewe Mhe. Waziri nishamueleza tatizo hili.

Sasa nataka kuchangia makusudi kutokana na tatizo hili. Ni tatizo ambalo hatujui hatima yake ni nini, maji yale tuliyonayo ndani ya kisima kile. Maji yake mpaka leo hii, watu tuliokuwepo katika kijiji kile hatuyatumii kwa kunywa. Tunapelekea kutumia maji yaliyokuwemo katika mashimo kwa kunywa. Kutokana na usumbufu wa maji yale tuliyonayo ni mengi tu lakini hayana ubora. Kuendelea kutumia maji hayo hatujui baadaye tutatokewa na tatizo gani. Hii si mara ya kwanza, nilipompigia simu Sheha alinambia kuwa hata Waziri aliyepita wa maji alikuwa analijua tatizo hili. Badala ya kwisha kutoa malalamiko yetu ufatiliaji haufuatiliwi, ndio tatizo. Namuomba Mhe. Waziri na hili anipe ufafanuzi kidogo.

Mhe. Spika, nitakuwa mwingi wa fadhila kama sikugusia suala zima la uchimbaji wa mafuta. Katika Wilaya yangu ndio wilaya ambayo kuwa ni nyonge sana. Nikisikia katika kisiwa chetu cha Zanzibar kuna maslahi kama haya na ikabidi serikali bado wanatutia huku wakitutoa huku basi tunaona serikali haipendi wananchi wake. Kuna usemi ambao Waswahili wanasema kwamba **"**mtoto haambi nyama hata akiamba nyama anakuwa keshaiyona" (Makofi).

Tunaiyomba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kupitia suala hili hebu Mhe. Waziri tuonee huruma, watu wanatusikiliza huko, watu wanatupigia siku saa 24 kutokana na suala hili. Mhe. Waziri tunakuomba tena utuonee huruma leo hii hatukusudii kukuzuilia fungu lolote katika bajeti yako lakini tunataka na wewe uturidhishe. Namuomba Mhe. Waziri atupe majibu mazuri katika suala hili.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naunga mkono mimi pamoja na wananchi wangu wa Wilaya ya Micheweni kwa sababu tuna dhiki kidogo mimi naunga mkono asilimia 80 ishirini nasubiri jawabu. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuchangia jioni hii muda huu. Mimi nitagusa zaidi kunako mwimbo wa taifa wa nchi hii. Wimbo wa taifa wa nchi hii ni maji hakuna jengine Mhe. Spika.

Kama tunavyojua maji ni uhai na bila ya maji huwezi kufanya chochote. Huwezi kulala bila ya kusalimiana na maji kwa siku nzima. Tatizo hili limekuwa sugu na limeota mizizi na sijui dawa yake ni nini. Wazee wetu, wajomba zetu, bibi zetu, wajomba zetu, shangazi zetu, wote wameshaota vipara kwa tatizo hilo sugu. Sijui matatizo haya yatamalizika lini. Tatizo limekithiri kupita kiasi. Juzi nauliza swali kuhusu maji naambiwa kwa asilimia 80 tayari maji yanapatikana. Tunaomba uthibitisho, hakuna. Kwa kweli ni suala ambalo linataka kufanyiwa kazi tena nzito. Narudia tena Wizara ya Ardhi, Makaazi, Majenzi na Nishati, ni wizara kubwa na ni mzigo mkubwa tuliomtwika Mhe. Ali Juma Shamuhuna tusiwe ni wenye kumlaumu. Hii wizara ni kubwa tena kubwa, hatuwezi kumlaumu wakati mwengine.

Mhe. Spika, nafikiri tokea kuteuliwa kwake labda siku moja tu kakutana na wafanyakazi wa Idara ya Maji kwenda kujitambulisha. Wananchi wetu majimboni shamba sisi wanapata shida sana kufatilia matatizo ya maji, mpaka wakati mwengine tuiingie na sisi wanasoka uwanjani tuweze kutroti. Huja wakapoteza nauli kutoka Jambiani mpaka Msikiti Mabuluu Shs 3,000/- kwenda na Shs 3,000/- kurudi. Anakuja pale hapati mtu wa kuonana nae anarudi tena shamba, anakutafuta mwakilishi. Wawakilishi tuna kazi ngumu majimboni. Sisi ndio walimu, sisi ndio baba, sisi ndio mama, sisi ndio madaktari. Si kazi ya kuchezea uwakilishi, tuna wizara zaidi ya 16 zilizoundwa majimboni kwetu.

Mhe. Spika, ninachotaka kumueleza Mhe. Waziri nasaha zangu kwake yeye ningemuomba akaanzisha vituo vidogo vidogo vya Wilaya ili kupunguza wanachi wetu wasipate shida kuja mjini. Ili mwananchi akipata shida ya maji asogee kituoni. Vitendea kazi wizara ya maji hawana. Leo kama si ukarimu wa Mhe. Mansoor mafundi wangeliumia sana. Mhe. Mansoor kafanya kazi ya ziada kuhusu Idara ya Maji. Nafikiri mwenyewe Mhe. Waziri halijui hilo. Ana gari ya Craner ndio inayosaidia pale Wizara ya Kilimo kwenda kupelekea mota kwenye visima. Leo gari idara nzima haina mota, gari milioni ngapi? Tuchukue milioni 50 kama itafika, leo wananchi wanateseka kwa gari ya milioni 50 na ambapo haiwezi kufika bei hiyo. Utaambiwa leo gari imekwenda wapi sijui, labda jimbo la Donge. Wananchi huku waumia, hata ikirudi kule siku mbili. Kuna mota nyengine zinataka zikafungwe. Si kazi nyepesi nduguzanguni, majukumu mazito haya tuliyopewa jamani, hasa sisi viongozi wa majimboni tuna kazi kubwa sana.

Mhe. Spika, leo inashangaza kwenye kitabu hichi ukurasa wa 48 tunaambiwa tuwaelimishe wananchi wetu namna gani ya kuchangia maji. Bidhaa si ipo

dukani inapatikana kama inapatikana watu wapo tayari kulipa. Leo kijiji cha Pete miaka mine hawajapata maji. Zile paipu wameshafanya antena za TV sasa hivi. Tutawaambia nini wananchi, uwaambie wachangie au walipe si watakufukuza, wataona tumechagua mwakilishi mwenda wazimu sisi, anatwambie tuchangie huduma na wakati huduma yenyewe haipatikani, hili suala ni nyeti.

Mhe. Spika, niamini kuwa hapa kuna kutiana mchanga wa macho. Hivi pamoja na matatizo makubwa ya maji tunaambiwa maskuli watajengewa vyoo na maji. Tokea lini! Ukurasa wa 53 unasema kuwa kuna usambazaji wa maji, ujenzi na vyoo, maskulini Unguja na Pemba. Maji hayapatikani leo tutawapeleka kule wanafunzi skuli. Hili suala ni zito na nyeti si suala la kulifanyia mas-hara ni suala la kukaa na kuliangalia. Kuchangia mtu huduma kama anaipata si tatizo.

Nirudi kwenye ukurasa wa 109 upatikanaji wa nishati mbadala. Tumeelezwa kuwa wizara inashiriki katika kusimamia miradi ya maendeleo mbali mbali. Ni miradi gani hiyo, iko wapi na hivi sasa ipo katika hatua gani, muelekeo wa kufanikiwa ukoje.

Mhe. Spika, tumeelezwa kuhusu Sera ya Mafuta ya mwaka 2010 tumeelezwa kuwa suala hili limeshazungumzwa na viongozi wetu wa Baraza lililopita. Nafikiri hili suala limeshapita pahala chapta imeshafungwa tusubiri maamuzi ya Mhe. Waziri kusubiri lini sheria itapitishwa hapa. Nafikiri hili suala tumpe muda Mhe. Waziri ili atuletee sera tuweze kuifanyia kazi. Naona haina haja kulirudia tena suala hili tena mara kwa mara.

Mhe. Waziri mimi nipa pamoja na wewe ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Rashid Seif Suleman: Ahsante sana Mhe. Spika, baada ya kumshukuri Allah na napenda nimshukuru Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake wa kitabu hichi. Mhe. Spika, bora niunganishe. Kwanza naunga mkono fikira zote zilizotoka kuhusiana na Mhe. Waziri kuja kutupa ufafanuzi wa suala la uchimbaji na ufafutaji wa mafuta Zanzibar.

Mimi nina mambo mawili, wale wanaojiuliza ni kwa nini vitu vyote vilivyokuwepo Tanzania vyenye kutoa uchumi havikutiwa katika suala la muungano likatiwa jambo hili tu. Historia yake iko wapi, watu wa histori ya uchimbaji wa mafuta wanasema kwa Tanzania utafutaji na uchimbaji wa mafuta ulifanywa katika miaka ya 50. Mafya kilichimbwa kisima cha mwanzo mwaka 1954, Unguja ilichimbwa 56 na Pemba visima 5 vilichimbwa mwaka 56. Matokea ya haya ndio yaliyowafanya waliingize hili tu katika muungano. Kwa sababu hii kazi ilikuwa imeshafanywa.

Mhe. Spika, la pili mimi nimetizama katika internent nimeona kwamba gesi asilia huko zamani yaani miaka ya nyuma ilikuwa haiyonekani kwamba ni gesi inayoweza kutumika kwa manufaa ya kibiashara. Walivyokuwa wakigundua gesi katika vile visima walikuwa wakiichukuliwa kwamba ni jambo labda lipo tu. Baada ya miaka hii kuanza kupanda bei za mafuta ndipo gesi ilipoanza kutafutwa kwa kutumika kibiashara. Ndio maana Tanzania ikawa pamoja na hayo ya kusema kwamba mafuta na gesi ni mambo ya muungano. Walipoanza kupata gesi wakashtuka wakasema looh! Tushayaingiza haya ndani ya Muungano na sisi tushapata gesi. Wakaanza kuziba kila kitu. Hiyo gesi haijulikani Kampuni gani imepewa, haijulikani inachimbwa kiasi gani, haijulikani fedha zinakwenda wapi. Mimi nasema kwamba sisi tunakila aina ya ushahidi wa kutetea haki yetu. Tunamuomba Mhe. Waziri aje atueleze kajipanga vipi kuitetea hiyo haki yetu.

Mhe. Spika, hapa ninayo karatasi ambayo Mhe. Jussa aliitaja, lakini mimi nimeona katuwekea kitu. Sisi tumeshapitisha hapa, suala la mafuta katika mwezi wa April 2009 liondolewe katika suala la Muungano. Tanzania ikaingia mkataba kwa kupitia shirika lake hili na kampuni kwa kuchimba na kutafuta mafuta Zanzibar. Mwenye kutoa hii *internet* analijua hili suala, hii karatasi ya mwanzo, alipoandika kuhusu Pemba–Zanzibar akai–bold huku mwisho shirika gani linalosimamia kai-bold na vile vile *Tanzania Petroleum Development Cooperation (TPDC)* pia kai –bold.

Sasa kama kwamba na sisi anatufahamisha kitu. Hayo mafuta mnayosema ni yenu sio ya Muungano Shirika lililotia sahihi ni la TPDC. Kwa sababu paragrafu nzima hii haikuwa *bolded* isipokuwa mambo mawili haya. Pemba Zanzibar na shirika linaloshughulikia TPDC.

Mhe. Spika, ndio nikasema kwamba si kwa sababu yakusema kwa hamasa, au jazba au nini. Lakini kweli tutafute ushahidi gani tena uliokuwa wa kuona kwamba hii mali inataka kuchukuliwa. Lakini hili la mwisho Mhe. Spika, kwa suala hili la mafuta nataka nimalizie hapa kwa sababu kuna kitu kidogo nataka nikitaje katika hizi dakika zangu kumi.

Mhe. Spika, hii meli iliyokwenda kuundwa hii ni meli ambayo inachimbua mafuta yakapakiwa kwenye meli nyengine moja kwa moja bila ya kupitia mahali pengine. Kwa sababu mimi mwenyewe nimeona katika *Channel* ya *Discovery* ambayo ni *very strategic channel* kwa mambo ya kiutaalamu. Namna gani meli ile inafanya kazi, namna gani meli nyengine za mafuta zinavyokuja. Kwa hivyo haina haja ya kufanya mambo mengine meli ile ile inachimba mafuta meli ile ile inatia kwenye meli mengine na inasafirisha. Kwa hivyo wewe ukiwa unangoja huku, unawangoja wao wanakuja wanachukua mafuta na meli zinakuja kuyasafirisha. Sijui tunangojea ushahidi gani. Nasema

Mhe. Spika, Mhe. Waziri aje na jibu zuri sana la kuturidhisha ili tuende pamoja.

Mhe. Spika, nije kwenye hii Idara ya Nishati kama nilivyoanza, Katika utaratibu wa kuagiza haya mafuta yaliyokwisha kusafishwa, tuna makampuni mengi tu yanaleta mafuta kama manne sasa hivi. Kila moja ukenda katika Kamati wanasema mafuta yao wanayoagiza ni bora zaidi kuliko ya mwenzake. Mhe. Waziri mimi membera wa kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Suala hili tulilileta katika meza naona humu sijaliona. Je, unautaratibu gani wa kuanzisha chombo cha ku- *regulate* hayo mafuta badili yakuwa kusema kila mmoja anajigamba kwamba miye naleta mafuta bora zaidi. Kuna utaratibu gani wa kuanzisha chombo ambacho kitatoa viwango vya haya mafuta na wao chombo hicho ndio kitakachosema.

Hii Idara inaitwa ya Nishati lakini biashara ya mafuta inashughulikiwa na Wizara ya Fedha. Ni kwa nini Wizara hii isikabidhiwe kila kitu kuhusiana na hii biashara ya mafuta ili ikawa wao ni mas-ul wa kuulizwa kuhusu kila kitu kitakachotokea. Mhe. Waziri kwa hivyo kama uliomba huko hebu njoo utueleze umekwama wapi, umakataliwa vipi hata ikawa suala hili la nishati lipo sehemu mbili. Huku lipo Idara ya Nishati, lakini suala linashughulikiwa na Wizara ya Fedha.

La mwisho kabisa niseme kwamba matatizo na migogoro ya ardhi tunaiomba sana wizara iweze kukabiliana nayo. Sasa hivi tunaanza na mkakati mpya kama alivyotuanzishia Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, tujipange upya ili tupate suluhisho la muda mrefu la migogoro ya ardhi. Hata kama kutakuwa na chombo maalum kabla ya kufika Mahakamani. Kiutaratibu Mahakama ni chombo cha mwisho, na sisi ikishakwenda kesi Mahakamani hatuna tena ruhusa ya kuisemea. Sasa ikiwa inaonekana kwamba migogoro ya ardhi ni mingi na inaweza ikatafutiwa suluhisho basi kiundwe chombo cha kutatua migogoro ya ardhi ili itakayokuwa hawaiwezi ndio inapelekwa Mahakamani.

Kwa hili Mhe. Spika, pamoja na kwamba muda ni mdogo naomba niseme naunga mkono hoja kwa asilimia 75 na ishirini na tano nangoja jibu la mafuta tu basi ndio ninalongoja. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Ahsante Mhe. Spika, Magharibi haya na mimi kunipa fursa kidogo yakutia tia chanja katika moto ambao umeshaanza kuwaka. Kwanza nawashukuru wale watendaji wakuu wa Wizara hii ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa kuona maeneo mengi nakujipanga kwamba mwaka huu wanataka kuyafanyia kazi. Mhe. Spika, mimi nasema tu kwamba mwizi siku zake ni arubaini, sitaki niondoe shilingi wala sitaki nipige buti mwaka huu nawasubiri kuona utekelezaji wao utakuwa vipi.

Mhe. Spika, hivi sasa kuna mazungumzo ambayo kila mtu anayazungumza kuanzia kwenye Baraza mpaka ukifika kwa wananchi, na mazungumzo hayo yanatugusa sote kwa sababu yanatuhusu kujaza tumbo. Kwa maana ya kuwa watu wana imani kubwa kwamba nchi yao ina rasilimali muhimu sana iliyowaondosha akina Sayyed bin Said na wengineo kurejea katika nchi zao za Maskati kwa sababu wao walikuja hapa zikiwa nchi zao masikini, lakini wakarejea kuona kwamba nchi zao ni matajiri hivi sasa. Mhe. Spika, nishati hii imekuwa ni gumzo kubwa na sisi tunapata mitihani ya kila leo, wananchi wanataka kujua kwamba je nishati hii ipo, nishati hii ni ya nani, na nishati hii itachimbwa lini. Kwa sababu njaa zimeshakomoa hawawezi tena kustahamili.

Mhe. Spika, sisi tuliopo hapa tumepewa ridhaa na wananchi, na hao viongozi wetu Mhe. Rais, Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais wote wamepewa ridhaa na wananchi ndio wamekuja hapa. Huu ni mwezi wa nane tu tokea kupewa ridhaa hiyo, tulipata ridhaa hiyo kwa kuaminika. Hivyo leo wananchi na wao wanasema kwamba suala hili sisi tunataka liwe letu kwa hiyo wametutuma tuje tuwaambie hili suala wananchi wanataka mulishughulikie.

Mhe. Spika, ule wakati wa kusema kwamba tunakwenda mbio hatuutaki tena, tunataka mukae kitako mtafakari je hili suala lina umuhimu kiasi gani kuhusu maisha ya wananchi wetu wa Zanzibar. Mhe. Spika, ili yasijeyakafikia mengine kwa sababu sisi tunao uwezo wa kuwashawishi wananchi tukawaambia sasa fanyeni kama yaliyotokea Tunisia. Kwa hivyo, mheshimiwa yasitokee yale na hiyo ni kwamba serikali haiko wazi sisi tunataka itupe uwazi kuhusu suala hili, je vipi? Ikifikia hatua hiyo naona wananchi wataridhika. Kwa hivyo, ili wananchi waendelee kuipa ridhaa serikali yao basi hili suala lifikie uamuzi haraka ili wajue kwamba yapo au hayapo. Mhe. Spika, hizo meli zikifika labda zichimbie huko huko lakini kama suala limeshaamuliwa basi litekelezwe haraka kwani kipi kinachotusumbua hivi sasa.

Mhe. Spika, tulipokwenda *OIC* tumetolewa lakini Mwalimu Nyerere alikuja tuunganishe chama tukakubali, tuondowe nafasi ya Rais wa Zanzibar kuwa Makamo wa Kwanza wa Rais tukakubali. Kwa hivyo, hili suala limeshafika kwenye Serikali ya Muungano na wamelifikia hatua gani. Mimi naomba tuwe makini katika suala hili ili tusijetukafika wananchi wetu wakafanya *up rising* wakenda barabarani, na wakenda barabarani tutawapiga risasi kwa sababu hawana silaha yoyote, hivyo naomba tuwe na uwazi kwenye suala hili.

Mhe. Spika, mimi nilibahatika katika raia wa Zanzibar walioishi katika nchi ambazo zinazalisha mafuta na zinauza mafuta. Nilibahatika kuishi karibu miaka mitano nimeona yale matunda waliyonayo kule, na mimi kidogo nilipata pepo pepo za matunda yale. Kwa hivyo, nikisikia kwamba rasilimali hii tunayo na

bado sisi tunasema kila siku kesho kesho, hivyo mpaka lini. Mhe. Spika, mim napendelea kuona na sisi tunaitumia rasilimali hii, mtoto wangu tena akenda skuli asikae katika vumbi apate kiti.

Mhe. Spika, uzoefu nilioupata kule ni kwamba hawa raia wa nchi zile huwa wanatuona sisi tunakwenda kwa wingi kutoka nchi za Kiafrika kwenda kuomba misaada. Kuna mwaka nilikuwa nchini Algeria ikaja *delegation* kutoka Tanzania Mhe. Spika, ilipoondoka *delegation* ile ikawa pana gumzo vyuoni, jamani kuna nini naona kumetoka *delegation* kutoka Tanzania. Mhe. Spika, ikabidi tutafutwe sisi kwa sababu tulikuwa wachache tukawaeleza kwamba imekuja imetaka msaada huu na huu. Kwa hivyo, kutokana na kwamba nchi yao ni mwanachama wa *OPEC* nchi zinazozalisha mafuta kwa wingi, basi wale wakaona wao mbona tunasikia nchi hii ya Zanzibar inazalisha mafuta mbona hawayachimbi wanakuja kutuomba sisi.

Kwa hivyo, wakaaza kuleta wasi wasi wakasema serikali kama itafanya suala kama hili basi na sisi tunaweza tukenda barabarani tukasema hatutaki. Wanafunzi wa Vyuo Vikuu hao kwa nini kwa sababu wanaona nishati tunayo na rasilimali tunayo lakini bado tunakwenda kuwaomba wao, wao wenyewe bado hajamaliza matatizo yao. Kwa hivyo, mimi nachelea kwamba haya mataifa ambayo yanaendelea kutusaidia ikaja ikafika wakati wakaona hivyo tuwasaidie hawa wakati rasilimali yao wanayo itakuwaje tuendelee kuwasaidia watu hawa wakati rasilimali yao hawataki kuitumia. Mhe. Spika, ili kuyaondosha hayo basi tuwe wakweli katika suala hili, tuseme kwamba siku gani na siku gani tutafanikisha suala hilo.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri hakutwambia hapa ametwambia kuhusu suala la maji kwamba tumepata msaada lakini kwenye umeme tulikuwa na Shirika la Norenco ambalo linasaidia kusambaza umeme vijijini. Mhe. Spika, Mhe. Waziri kwamba huu hakutwambia lolote kuhusu shirika hilo kwamba ni vijiji vingapi vitatiwa umeme katika bajeti yake, mimi nachelea kwamba na wao wameshachoka kutusaidia wakijua kuwa rasilimali hii ipo lakini hatutaki kuiendeleza.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa nakwenda kwenye Shirika la Umeme. Mhe. Spika, serikali ina mpango tosha wakulifanyia *reform* Shirika la Biashara ya Karafuu kwa maana ya kwamba limeshindwa kuzalisha. Kwa hivyo, na hili Shirika la Umeme nalo linahitaji reform hivi sasa linakwenda *as if* ni watu tu wamekaa pale lakini sio shirika la kibiashara. Mhe. Spika, unaweza kwenda pale ukamkutia mwananchi amejitolea nguzo kumi kupeleka umeme sehemu, lakini mwananchi yule baada ya kuufikisha umeme katika sehemu husika wananchi wengi wataunga umeme katika sehemu zile.

Lakini yeye bado ataendelea kutonzwa haambiwi kwamba leo wewe umeshachangia nguzo kumi, umesaidia transofoma, umesaidia na waya zimeshafika hapa, hivyo wewe hebu kaaa katika mfumo huu wa malipo. Mhe. Spika, mambo kama haya yanarudisha nyuma wananchi unaposikia mwananchi amechangia kwenye masuala kama hayo basi afikiriwe aonekane kwamba huyu ameshalisaidia shirika. Leo ukenda katika shirika kuna zile wanazoziwekea umeme juu zinazopitia waya ukenda kwa duka la muuza maji ananambia ni shilingi elfu arubaini.

Lakini kile kipande kinachokatwa na Shirika la Umeme kwanza hawakubali utoe wewe lazima watoe wao, ukenda pale utaambiwa hii kinakatwa vipande vitano kila kipando ni shilingi elfu arubaini, lakini ukenda ukenda dukani unakutia inauzwa shilingi elfu arubaini tu. Kwa hivyo, hilo ndio itakuwa tunaboresha au tunarudisha nyuma wananchi wetu, leo ukenda kutaka kuungiwa umeme utaanza kuuza mayai basi yatamaliza, utaanza kuuza kuku wamalize, uanze kuuza mbuzi na ng'ombe wao hawajafika kukuungia. Mhe. Spika, wao bado hawako katika kiwango wao ni watu wa biashara wanavyotakiwa hivi sasa nakuomba Mhe. Waziri hili shirika unatakiwa ulifanyie *reform* yakutosha.

Mhe. Spika, leo tumepata mita zimekuja mita miaka mitano iliyopita na wala hatujui ipi ni nzuri sijui kama ni hii ya digital au hii mita ambayo inatumika ya analog. Mhe. Spika, unakwenda majumba mengine yana mita hizi na majumba mengine yana mita hizi. Kwa hivyo, kama shirika lina uhakika nini wanachokifanya hivyo kipi kinasaidia katika kupata faida, mita ile au ni mita hii. Mhe. Spika, kama ni mita hii kwa nini hawajatuwekea mpaka leo wakajua shirika linafaidika na litamuondoshea mwananchi usumbufu.

Kwa hivyo, hili shirika linahitaji *reform* ya hali ya juu, ukija kwenda kwenye malalamiko hakuna hata raia mmoja aliyekwenda kwenye shirika akasema mimi nimetiliwa bili utakutia wengine kama wana kiwanda. Mhe. Spika, hili shirika linahitajika hivi sasa liende na wakati na bila ya hivyo basi usumbufu utaendelea na umeme utaendelea kukosekana.

Mhe. Spika, nakwenda kidogo katika Idara ya Maji, mimi najua natoka kijijini nikitajiwa haya mapesa naona sijui kama kitu gani. Mhe. Spika, kuna mradi wa Wajapani ulikuja mwaka juzi na mwaka jana Julai ukamaliza kazi yake ukatumia bilioni 19 ukajenga visima Dole na maeneo yanayoshukia hapa Welezo na mradi huu tukaambiwa kwamba wananchi watapata maji eneo la Bububu, Mfenesini, Dole na Mtoni. Mhe. Spika, baada ya kuondoka wafadhili tu ndani ya miezi miwili wananchi wa Mtoni maji hamna.

Mhe. Spika, hii inasababishwa na nini? Mhe. Spika, ni je utaalamu wetu ni mdogo, je, tunapofanya hii *feasibility study* inakuwa hatujui au ni vipi. Kwa nini ndani ya miezi miwili maji yakosekane wakati miundombinu tayari imeshatayarishwa sehemu ile. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri akae na watendaji wake wakuu waangalie kwa nini kunakuwa na ukosefu wa maji katika eneo ambalo tayari miundombinu imeshapita na tayari wenzetu Wajapani wameshatoa mabilioni ya mapema.

Mhe. Spika, nimalizie katika suala la ardhi, suala hili la ardhi sasa hivi limekuwa na migogoro mengi kila unapokwenda mgogoro lakini mengi tunayasababisha sisi. Mhe. Spika, sijui kama Mhe. Waziri kama anajua katika eneo la Mtoni kuna uwanja ambao wananchi walikuwa wanautumia kwa ajili ya watoto wao kwenda kufanyia sikukuu na vijana wanacheza mpira. Mhe. Spika, leo wamekwenda vikosi vya SMZ wamejenga kuta huna hata pakupita, vijana wale hawana pakucheza mpira. Mhe. Spika, ukenda kuuliza unawakuta na mtutu wao mlangoni.

Mhe. Spika, kwa kweli hii migogoro tunaisababisha sisi mimi nakuomba Mhe. Waziri unipe maelezo kidogo huu uwanja ilikuwaje hawa vikosi wakenda wakauvamia wakawadhulumu vijana na wananchi kwa jumla hata pakupita hawana. Mhe. Spika, mimi kama nilivyosema mwanzo sitaki niondowe shilingi nakupeni muda kuhusu hili. Kwa maana hiyo mimi naendelea kukuunga mkono, Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Spika: Mhe. Spika, Mhe. Abdi Mosi Kombo nikuombe radhi kwa sababu muda uliobakia ni dakika kama tano tu ambao ni muda mfupi mno hutoweza kuchangia sehemu kubwa. Waheshimiwa Wajumbe tumetingwa sana na muda na tuko nyuma ya wakati tulipaswa wizara hii tumalize jioni hii ya leo, lakini kwa kuwa Wizara ya Afya ilichukua muda zaidi ya uliopangwa kwa hiyo sasa tuko nyuma ya wakati. Niwaombe Waheshimiwa Wajumbe tunapochangia tujitahidi kupanga *points* zetu vizuri ili kuhakikisha kwamba tunakwenda kwa mujibu wa ratiba, tumelazimika kuzitumia baadhi ya Jumamosi na Jumapili ili kuhakikisha kwamba tumaliza shughuli yetu kunako tarehe 31/07/2011 kwa sababu baada ya hapo mbele kuna mambo mawili makubwa.

Kwanza kuna shughuli moja kubwa ya serikali lakini pili kuna mwezi wa Ramadhani ambao tulifikiri kwamba tungefungia kila mmoja nyumbani kwake. Kwa hivyo, tujitahidi na kuna miswaada miwili ambayo tayari imeshagaiwa nayo tunataka kuipitisha kwenye mkutano huu. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe wale ambao wamekosa nafasi akiwemo Mhe. Abdi nasikitika sana nilimtaja lakini mheshimiwa aliyemaliza amechukua zaidi ya dakika kumi, pamoja na Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Ashura Sharif Ali niwaombe radhi sana kwamba muda kwa kweli umetutinga mno.

Lakini kesho asubuhi Mwenyezi Mungu akipenda itakuwa ni zamu ya mawaziri na watakaopata nafasi ya kucnangia kesho asubuhi mara baada ya kipindi cha maswali ni Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati pamoja na Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum Mhe. Haji Faki Shaali. Baada ya hapo nitawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe tukubali tuje tumkaribishe Mhe. Waziri ili kuweza kufanya majumuisho anahitaji muda mkubwa kidogo kwa yale ambayo mmeyazungumza kwa kina na yaweze kujibu kwa utulivu, kwa ufasaha ili tufikie pahala tuelewe tunachokipitisha katika Baraza letu hili.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo machache niahirishe kikao hiki hadi kesho tarehe 12/07/2011 saa 3:00 asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa hadi kesho tarehe 12/07/2011 saa 3:00 asubuhi)